# STORIES AND TRANSLATIONS IN SWAHILI.

# MAMBO NA HADITHI.

LONDON:

SOCIETY FOR PROMOTING CHRISTIAN KNOWLEDGE;

NORTHUMBERLAND AVENUE, CHARING CROSS, W.C.

1884.

Digitized by Google

# CONTENTS.


| | PAGE |
|---|---|
| Mambo ya Ulimwengu ... ... ... ... | 1 |
| Habari za Babel ... ... ... ... | 5 |
| Sultani Nebukadnezar ... ... ... ... | 7 |
| Sultani Kuro ... ... ... ... | 9 |
| Sultani Kuro Alivyokufa ... ... ... | 11 |
| Sultani Dario ... ... ... ... | 12 |
| Sultani Dario na Wasikuthi ... ... ... | 13 |
| Sultani Dario na Wayonani ... ... ... | 15 |
| Sultani Serkisi na Wayahudi ... ... ... | 16 |
| Sultani Serkisi na Wayonani ... ... | 20 |
| Habari za Wayonani ... ... ... ... | 23 |
| Hadithi ya Ulisse ... ... ... ... | 23 |
| Kroiso na Solon ... ... ... ... ... | 41 |
| Lukurgo na Wasiparta ... ... ... | 44 |
| Masultani wa Wayonani ... ... ... ... | 47 |
| Waatene ... ... ... ... ... | 48 |
| Sokrati ... ... ... ... ... ... | 50 |
| Iskander ... ... ... ... ... | 53 |
| Visa vya Iskander ... ... ... ... | 56 |
| Warumi (Romulo na Remo) ... ... ... | 58 |
| Mji na Mwili ... ... ... ... ... | 60 |
| Koriolano ... ... ... ... ... | 62 |
| Kinkinato ... ... ... ... ... | 63 |
| Wagallo na Mabata ... ... ... ... | 64 |
| Purro Myonani ... ... ... ... ... | 65 |
| Tabia ya Warumi ... ... ... ... | 65 |


Digitized by Google

| | PAGE |
|---|---|
| Njia na Makolonia ... ... ... ... | 66 |
| Wakartagini ... ... ... ... ... | 68 |
| Regulo ... ... ... ... ... ... | 68 |
| Hanibali ... ... ... ... ... | 70 |
| Kaisari ... ... ... ... ... ... | 71 |
| Petro Mtume ... ... ... ... ... | 72 |
| Blandina ... ... ... ... ... | 74 |
| Sapritio ... ... ... ... ... | 77 |
| Mashahidi arobaini ... ... ... ... | 78 |
| Kufunga na Kufungua ... ... ... | 81 |
| Mjinga na Mwalimu ... ... ... ... | 84 |
| Michezo Mibaya ... ... ... ... | 86 |
| Watu waliosinzia Miaka Miteen ... ... ... | 87 |
| Juma ya pili ya Mitende ... ... ... | 92 |
| Wenseslao ... ... ... ... ... | 95 |
| Melkior kasisi ... ... ... ... | 96 |
| Wavuvi ... ... ... ... ... ... | 99 |
| Buibui ... ... ... ... ... | 101 |
| Abdallah na Sabat ... ... ... ... | 103 |
| Msafiri ... ... ... ... ... | 105 |
| Kristofer ... ... ... ... ... | 116 |
| Makario na kitwa ... ... ... ... | 118 |
| Na tena? ... ... ... ... ... | 119 |
| Mkuu katika barra ... ... ... ... | 119 |
| Dawa ya ugomvi ... ... ... ... ... | 120 |
| Kungu ... ... ... ... ... | 120 |
| Sultani Hakkum ... ... ... ... ... | 122 |
| Sultani Orungzebi ... ... ... ... | 122 |
| Sultani Mahmoud ... ... ... ... | 123 |

Digitized by Google

# MAMBO NA HADITHI.

## MAMBO YA ULIMWENGU.

ZAMANI za kale, imepata miaka kama elfeen na hamsi mia, Muungu alimfunulia nabii Daniele mambo ya ulimwengu, yatakayokuja toka siku zilezile mpaka siku za mwisho. Akamfunulia hivyo.

Palikuwa na Sultani wa Babel, mji wa Waajjemi, jina lake Nebukadnezar. Akaondoka akiendea Yerusalemi, mji mkubwa wa Wayahudi akiutwaa, akachukua mfalme wake na wakuu wake na mashujaa wote, watu elfu kumi, na mafundi wote na wafua chuma, hawakubaki illa wanyonge wa watu, nao si wengi. Akachukua na mtoto Myahudi, jina lake Daniele. Yule mtoto akakaa nyumbani mwa Sultani, akalewa vizuri, akapata kuwa waziri wake Sultani wa Babel.

Sultani akaota ndoto. Alipoamka assubui, amekwisha kuisahau kabisa, akaona uchungu kwa roho yake akaagiza watu wake wenyi akili na ilmu wamkumbushe ndoto yake wakamfasirie wasiweze. Naye Daniele mcha Muungu sana, akawa nabii, Muungu akamwezesha kumjulisha Sultani habari ya ndoto na tafsiri yake pia. Na ndoto ile ndio hii. Ikatokea sanamu ya mtu mkubwa na mrefu,

ikisimama mbele ya Sultani, iking'aa sana, na namna yake ya kuogofya, yenyi kitwa cha thahabu safi, kifua na mikono ya fetha, tumbo na mapaja ya shaba, miguu kwa juu ya chuma, kwa chini ya chuma kilichochanganyika na udongo. Hatta baadaye tazama jiwe lisilokatika na mikono, likaipiga sanamu katika miguu ya chuma na udongo, likaivunja vipande vipande. Nacho chuma na udongo na shaba na fetha na thahabu zikavunjika vipande vipande pamoja, zikawa kama makapi penyi kutwangia ngano, hatta baridi ikazipeperusha zisipopata tena pa kukaa, jiwe lile lenyi kuipiga sanamu likawa lima kubwa, likajaza dunia yote pia.

Tena Daniele naye akaona ndoto, na tazama, pepo 'nne za mbingu zikishindana juu ya bahari kuu. Nyama wanne wakubwa wakapanda baharini, nao mbalimbali wao kwa wao. Wa kwanza kama simba, mwenyi mabawa ya tai. Hatta mabawa yake yakanyonyolewa, akainuliwa katika inchi akasimamishwa kwa miguu ya binadamu na kupewa moyo wa binadamu. Na tazama, nyama mwingine wa pili kama dubu, akajiinua upande mmoja, na mbavu tatu kinwani mwake katika meno yake, wakamwambia, ondoka kale nyama tele. Halafu yake tazama mwingine kama chui, akawa na mabawa ma'nne ya ndege maongoni mwake, nyama huyo naye mwenyi vitwa vinne, akapewa mamlaka. Halafu yake tazama nyama wa 'nne, mwenyi hofu na kuogofya na kuweza mno ajabu, akawa na meno ya chuma makubwa, akameza akavunjavunja akakanyaga mabaki na miguu yake. Huyo mbali na nyama wale wote waliotangulia, akawa na pembe kumi. Daniele akaziangalia zile pembe, na tazama, ikapanda katikati pembe ngine ndogo, mbele yake pembe tatu za kwanza zikang'olewa, na katika pembe hiyo macho kama macho ya binadamu, na kinwa chenyi kunena

Digitized by Google

makuu. Hatta viti vikawekwa taratibu, naye Mzee wa kwanza ameketi, nguo yake kama theluji nyeupe, nyele za kitwani kama sufi iliyosafika, kiti chake kama ndimi za moto, gurudumo zake moto uwakao. Mto wa moto ukatoka ukipita katika mbele yake, elfu elfu wakamngojea, majeshi ya majeshi wakasimama mbele yake, hukumu ikatengenezwa, misahafu ikafunuliwa. Daniele akaangalia, kwa sababu ya sauti ya maneno makuu iliyoyanena pembe, hatta yule nyama akauawa, mwili wake ukaharibika, ukatolewa kwa moto uwakao. Nyama wale waliobaki, nao wakatwaliwa milki zao, wakipewa kukaa kwa muda na wakati. Na tazama, Aliyefanana na binadamu akaja kwa mawingu ya mbingu, akamjia Mzee wa kwanza, wakamkaribisha mbele yake. Akapewa enzi na utukufu na ufalme, watu wote na mataifa na lugha wamtumikie, enzi yake ndio enzi ya milele isiyopita na ufalme wake usioharibika.

Nabii Daniele akaota ndoto ngine, akiwako kando ya mto Kuran, jina lake la kwanza Ulai. Palikuwa na mbele ya mto ule kondoo mume anasimama naye mwenyi pembe, zile pembe zikawa ndefu, lakini moja ndefu kupita mwenzake, iliyo ndefu ikaota baada yake iliyo fupi. Na tazama, mbuzi mume akatoka magaribini, asipogusa inchi na miguu, akawa na pembe moja nzuri kati ya macho yake. Akamjia kondoo mume mwenyi pembe, aliyesimama kando ya mto, akamrukia kwa nguvu na hasira nyingi. Akamkaribia kondoo mume akamkasirikia kwa ukali sana, akampiga, akimvunjia pembe zake mbili, yule kondoo mume hana nguvu ya kushindana naye, akamtupa chini akamkanyaga, wala hakuna awezaye kumwokoa kondoo mume katika mikono yake. Bassi yule mbuzi mume akakua sana, alipokwisha kupea, pembe iliyo kuu ikavunjika, zikaota pembe 'nne nzuri kwa huko na huko na huko na huko.

Digitized by Google

Na katika pembe moja ikatoka pembe ngine ndogo, ikakua sana kwa kusini na kwa mashariki na kwa inchi yenyi kupendeza. Ikakua hatta kwa jeshi la mbingu, ikatupa chini wa jeshi lile na za nyota, ikazikanyaga. Kumbe akajitapa hatta juu ya mfalme wa jeshi, naye akatwaliwa ibada ya killa siku, na hekalu lake likaangushwa chini, pembe ile ikatupa yaliyo kweli chini, ikatenda kazi ikafanikiwa.

Daniele akasikia watakatifu wanazumgumza wakiulizana, Hatta lini bassi mambo haya mabaya-mabaya? Akaambiwa, kwa muda wa siku elfeen na thelatha mia. Ndipo hekalu litakapotakaswa.

Daniele akafunuliwa tafsiri za ndoto hizi, na tafsiri zao sawasawa. Sanamu ile ndio falme 'nne kuu za dunia, na jiwe lile ndilo ufalme wa mbingu. Nyama wale ndio wafalme wa dunia, naye Mzee wa kwanza ndiye Muungu mwenyiezi. Bassi ndivyo yalivyokuwa mambo ya ulimwengu, ndivyo yatakavyokuwa yaliyosalia.

Falme za dunia zilizo kuu, ndizo hizi 'nne.

1. Ufalme wa Babel, na mfalme wake Nebukadnezar, kama kitwa cha thahabu kwa fakhari yake, na kama simba kwa kuwa mkali, na kama tai kwa kwenda upesi katika vita.

2. Ufalme wa Waajjemi, na mfalme wao Kuro, kama kifua cha fetha na kama dubu na kama kondoo mume, kwa maana ya kuwa hodari sana na uzito wake ndio nguvu yake, ukashinda mataifa matatu, wala haukupata fakhari kama wa kwanza.

3. Ufalme wa Wayonani, na mfalme wao Iskandro, kama chui na mbuzi mume kwa kugundua na kushinda adui zote kwa gháfala, naye akashika Europa huko na Asia huko kwa nguvu zake, kama tumbo hushikavyo mapaja huko na huko, nalo kati kati.

4. Ufalme wa Warumi, watu hodari kuliko wote,

Digitized by Google

wakavunja na kuponda na kukanyaga mataifa yote ya dunia, wasiweze kuyasuluhisha illa kadiri tu, kama chuma na udongo hazichanganyikani: mwisho wakatengwa wenyewe mafungu mawili.

Mbalimbali Ufalme wa mbinguni, na mfalme wake Isa Masiya. Huo ulioanza siku ya Pentekote katika Yerusalemi, si kwa mikono ya watu illa kwa nguvu ya Roho Mtakatifu, umepata sasa miaka themantashara mia na hamsini, ukienea pote ukitiisha mioyo ya waana Adamu, wala hauna mwisho.

## HABARI ZA BABEL.

INCHI ya Babel ndio inaokwitwa sasa inchi ya Waajjemi. Ndipo waana Adamu walipopata kwanza kujua desturi na mathehebu za kiungwana na kuihtimu ilmu nyingi na kazi nzuri nyingi. Naswi hapa tumepata kutambua mambo yao hivi. Watu wa inchi ile wakatwaa udongo, wakaufinyanga, wakafanya matofali, wakapiga chapa maneno mengi na mazuri katika matofali hayo, habari za mambo yao yote, na desturi zao na ilmu pia, habari za miji na mashamba na vita na ibada na sheria na lugha na miti na nyama na ilmu ya nyota na ya kuhesabu nyingi. Matofali hayo yaliyopigwa chapa, yakachomwa moto. Yalipokwisha kuchomwa moto, yakawekwa katika vyumba vikubwa na vizuri, walinzi wakayangojea, na killa tofali limeandikiwa hesabu yake. Bassi watu wakitaka kusoma, huingia chumbani, huuliza mlinzi matofali, huletewa taratibu, husoma. Kiisha soma huenda zao. Hatta miji ya

Digitized by Google

Babel ilipoharibika, na matofali hayo yakapotea yakistirika na taka na mchanga na magugu katika maanguko ya miji, inchi ikageuka kuwa nyika, hamna hatta watu, siku nyingi nyingi zikapita.

Hatta siku hizi watu hodari wenyi akili wakasema, Twende tutafute mahali pa miji ile iliyoharibika zamani, tupate kujua habari zao. Wakaenda wakitafutatafuta wakichimbachimba katika nyika, na tazama, matofali mengi mengi yakaonekana mazima. Wakafurahi. Hivyo tulivyopata habari za inchi ile.

Tunazo habari tena kwa Maandiko Matakatifu, kama hizi. Watu wa kwanza wakatoka katika milima ya Asia kwa mashariki, wakaona inchi nzuri na pana na sawa yenyi mto mkubwa ndio Frati, wakakaa humo, wakajenga miji na mnara kwa matofali na lami. Kazi ile ya kujenga mnara haikumpendeza Muungu, akaizuia akiwatawanya watu. Na inchi hiyo ndipo alipokaa kwanza Ibrahimu na jamaa yake, akaitwa na Muungu kuko huko akatoka akiacha ndugu zake na jamaa yake akienda kwa inchi ya Kanaan.

Masultani wa Sham waliomiliki Babel na inchi yake siku nyingi. Hatta mwisho wakashindwa na Sultani wa Babel, Babel ukakua ukawa mji mkubwa sana kuliko miji yote ya dunia. Na Sultani wake aliye mkuu, ndiye Nebukadnezar.

Digitized by Google

## SULTANI NEBUKADNEZAR NA MJI WAKE BABEL.

Palikuwa na Sultani wa Babel, jina lake Nebukadnezar, naye hodari sana. Kwanza akawashinda Wamisri, tena akawashinda Wayahudi, akateka Yerusalemi akachukua watu wake wote. Akafanikiwa sana.

Alipokwisha kurudi kwake akauongeza mji Babel, akaujengea kuta kubwa, akaupamba sana na majengo mengi mazuri na hekalu na mnara na jumba na bustani. Habari za mji wake tumeziletewa na mtu Myonani, aliyekwenda kutazama mwenyewe, akarejea kwake akaandika mambo yote aliyoyaona katika kitabu, kitabu kile kikawapendeza sana Wayonani, sifa zake zikaenea katika ulimwengu wote hatta kwa leo. Na habari zake ndizo hizi.

Babel ni mji mkubwa sana ajabu. Umejengwa hivi. Mwenyi boma pande zote, huko na huko na huko na huko, na pande zote 'nne zimenyoka sawasawa, na urefu wao mmoja, killa upande urefu wake kama mwendo wa saa sita, upande huu na upande huu na upande huu na upande huu, zote sawasawa. Na boma hilo ajabu pia. Umejengwa kwa matofali na lami pia, lenyi kwenda juu mikono miteen, na unene wake mikono hamsini. Hatta na nyumba zimewekwa juu yake huko na huko, na kati ya nyumba njia pana juu ya boma, gari la frasi wa'nne halikosi nafasi ya kupitia njiani katikati ya nyumba zilizoko juu ya boma. Na katika boma milango ya shaba mia na minara mengi mengi. Tena pambele ya boma pia kwa nje shimo limefanyika, limechimbiwa chini sana, na pana, limejaa maji kama mto. Ndizo habari za boma la Babel. Na ndani yake mashamba mengi na makoonde na majengo na nyumba. Njia zote za mji zimenyoka sawasawa. Tena mto mkuu na

Digitized by Google

mzuri ukiingia katika mji upande mmoja ukipita katikati yake, ukitoka upande wa pili. Na kingoni mwa mto kuta huko na huko, na katika kuta hizi milango mengi ya kupandia mjini. Hatta daraja kubwa na refu la kuuvukia mto, watu wapite upesi kwa miguu ng'ambo ya pili.

Sultani Nebukadnezar akaupamba sana mji, akazinyosha njia zake, akajenga hekalu kubwa kwa muungu wake, na jumba kwake mwenyewe, akafanyiza tena bustani. Hatta bustani ile imeshinda zote kwa kazi yake ya ajabu. Imetegemea yote nguzo na matao, ikafika juu kwa madaraja mengi, juu kwa juu, kama kilima chenyi kwenda juu mikono miteen, na katika madaraja miti yote iliyojulika, namna zote, na jamii ya maua mazuri, na njia za kutembelea huko na huko kwa kujifurahisha na manuka ya maua yale na matunda ya miti na uvuli na kupepewa na baridi, ziko na nyumba za kupumzikia na kutazamia mji umetanuka chini na uzuri wake wote na kazi zake zote. Na hiyo ajabu. Bustani ikanyweshwa maji kwa bomba. Bomba ikayavuta maji ya mto upitao chini, ikayapandisha juu, maji yakatoka juu tele, yakainywesha bustani pia.

Sultani Nebukadnezar alipomaliza kazi hizi zote, siku moja akapanda darini kutembea, akatazama mji wake na jumba lake na mali zake zote, akajivuna sana rohoni mwake, akasema, "Tazama mji huu Babel, nilioujenga mimi kwa nguvu ya enzi yangu na kwa heshima ya utukufu wangu." Akisema haya, marra akageuzwa moyo, akili zake zikampotea, watu wakamfukuza, akala majani kama ng'ombe, akipata miaka saba kwa hali hii. Hatta baadaye akainulia macho yake mbinguni, akili zake zikamrudia, akawekwa katika ufalme wake vilevile, akamshukuru Muungu.

Digitized by Google

## SULTANI KURO NA BABEL.

Palikuwa na Sultani wa Waajjemi, jina lake Kuro. Akaondoka akawashinda Wamedi. Alipokwisha kushinda Wamedi, akawashinda Waludi, taifa kubwa la Anatolia, akamiliki Anatolia yote pia. Akafanya jeshi kubwa, akafika kwa Babel, akataka kuutwaa. Alipokaribia boma lake akasangaa, akaingiwa na mashaka, akiona lilivyokwenda juu sana wala halivunjikani, wala hakuna kulitoboa ginsi lilivyo nene mno, wala hakuna kuwashindisha watu kwa njaa, kwa sababu ya kuwa mashamba mengi na makoonde mengi ndani ya boma, hatta vita haithuru, watu wakilima vilevile na kupanda na kuvuna na kukaa raha na salama. Yule Sultani akafanya shauri. Akagawanya watu wake wote makundi matatu, akaweka kundi moja kuko huko mto ulikoingia mjini kwenda kupita katikati yake, na kundi moja kwenyi kutokea kwake. (Na mto ule mkubwa, ukipita katikati ya mji toka upande huu hatta upande wa pili, mwenyi kuta huko na huko kingoni mwake na milango ya kupandia mjini katika kuta). Akaamuru makundi yale mawili, akisema, mkiona maji ya mto yamepunguka sana, mwingie mtoni mwende mbio ndani ya mji, mkautwae. Alipokwisha kuwaagiza haya, akatwaa mwenyewe kundi la tatu, ndilo watu wasiofaa kwa kupigana, wazee na watoto na walio thaifu, akaenda zake kando la mto kwa kaskazini, ndipo mto ulipotoka, hatta akafika ziwa kubwa, nalo karibu ya mto. Na ziwa lile limekauka, hamna maji illa kidogo tu. Kuro akafanyiza njia ya maji tokea mto hatta kwa ziwa, akangojea siku kuu ya Wababel, marra akauziba mto akayachurukiza maji yake yote kwa ziwa. Bassi watu wale waliongoja

Digitized by Google

kule karibu ya mji wakauangalia mto, na tazama, maji yamepunguka hatta kwa kati ya paja, wakaondoka wakaingia mtoni makundi yote mawili, wakapita mbio ndani ya boma, wakakuta milango ya kingoni mwa mto huko na huko imeachwa wazi, kwa maana watu wanafanya siku kuu, wakautwaa mji, wakamwua liwali wake ndiye Belshazzar. Yule Belshazzar akawa anafanya karamu kwa siku kuu, na wakubwa wengi, akaamuru watumishi wamletee vyombo vitakatifu, Sultani Nebukadnezar alivyochukua katika hekalu la Yerusalemi, akanywa navyo. Marra ukamtokea mkono wa mtu, ukaandika maneno katika ukuta yasiotambulikana. Sultani akasangaa na wakubwa wake akatafuta mtu mwenyi kufasiri maneno yale, asipate, illa nabii Daniele ndiye aliyemfasiria maneno. Na maneno yaliyoandikwa ndio haya, Mene, Mene, Tekel, Ufarsin, na tafsiri yao, mamlaka yako imehesabiwa, imepunguka, imevunjika. Bassi usiku uleule ndipo Waajjemi walipotwaa Babel kwa hila, wakamwua liwali Belshazzar. Na kwa sababu mji ule kuwa mkubwa na mrefu sana, nao watu wakikaa mbalimbali, watu wengi hawajasikia habari kama mji umekwisha kutwaliwa.

Kuro huyo anaye sifa nyingi katika maneno ya manabii. Isaya alimnena jina lake na kazi yake miaka mia na arobaini kabla hajazaliwa, na ginsi atakavyoshinda mataifa, na upungufu ule wa maji, na kuwaagiza Wayahudi warejee kwa Yerusalemi. Tena Yeremia alitoa habari nyingi ya ukuu wake Babel na ubaya wake na kuharibika kwake.

Digitized by Google

## SULTANI KURO ALIVYOKUFA.

SULTANI Kuro alipokwisha kuutwaa Babel na kutiisha Washami, akakaa siku nyingi akakusudi kuondoka kwenda pigana na Wamassageti. Nao wakakaa upande wa pili wa mto Aras, karibu ya bahari Kaspiani, na Sultani wao ndiye mwanamke, jina lake Tomuri. Kuro akatuma mjumbe aende amtake mwanamke yule amwoe. Naye akakataa, akiona kama jambo hili ujanja tu apate kumua. Kuro akaondoka akafika hatta mtoni, akafanya vita kwa wazi. Sultani mke yule akatuma mjumbe, akisema, "Angalia, usitende haya. Hufanikiwi. Nenda kwako, kasterehe. Usipokubali, nakutolea mambo mawili. Nikuache wewe kuvuka mto, kuja huku kwetu mwendo wa siku tatu, ao uniache mimi kuvuka kule kwako sawasawa? Bassi chagua." Kuro akafanya shauri akamjibu, "Nivuke mimi kwenu." Akavuka akaenenda siku moja. Tena akaweka tayari vyakula vingi na vizuri, akaacha watu wake wasio na nguvu wala kufaa, akaenda zake. Wakaja Wamassageti, kundi moja, akawapiga walioachwa wakajinyosha kwa chakula. Marra akarudi Kuro, akawagundua katika karamu, akawashinda sana, akachukua wengi sana wamefungwa, na mtoto wa Sultani, jina lake Siparagapisi. Yule Sultani mke akaghathabika sana, akatuma mjumbe, akisema, "Ee mnywaji damu, nakutolea mambo mawili. Uniachie mtoto wangu, uende kwako kwa salama, ao nikushibishe damu?" Hakuyaangalia maneno haya hatta kidogo. Na mtoto yule wa Tomuri akaomba kufunguliwa kidogo, akipata ruksa akajichinja mwenyewe. Kuro akaondoka, akapigana sana na Wamassageti. Kwanza wakapigana na

Digitized by Google

mishale, halafu yake na mikuke na panga. Mwisho watu wa Kuro wakakimbia, naye mwenyewe akauawa. Bassi yule mwanamke akatwaa kiriba cha ngozi, akakijaza damu ya watu, akatia kitwa chake Kuro, akisema, "Ulipomua mtoto wangu, umeniua mimi. Nami nimekushibisha damu. Hiyo ndiyo niliyosema. Bassi."

## SULTANI DARIO.

BAADA ya Sultani Kuro miaka si mengi, kulikuwa na Sultani wa Waajjemi, jina lake Dario. Akianza kumiliki, rayia zake wakamwasi, akawapiga, akawatuliza. Kiisha akatengeneza kwa akili milki yake yote, akaitengeneza hivi. Akagawanya milki yake mafungu asharini, yaliyokwitwa satrapia, na liwali wake killa satrapia kuitwa satrapi. Killa satrapi kama sultani katika milki yake, hutosha watu ushuru, humpelekea Sultani Dario. Tena Sultani Dario akafanyiza njia kuu, yenyi nyumba za kupumzikia, na wajumbe wengi, kazi yao kupita huko na huko upesi kwa frasi katika ufalme wake pia, kupeleka barua za Sultani na kutangaza amri zake na kumpasha habari za milki yake yote. Jambo la tatu, Sultani Dario akapiga chapa vipande vya fetha na thahabu, killa kipande chenyi sanamu ya mtu na uta wake, vipande hivi vikatumika kwa fetha katika ufalme wake. Akasitawi, akataka kuzidisha ufalme wake, akafanya vita tatu, ya kwanza na Wahindi, ya pili na Wasikuthi, ya tatu na Wayonani. Akaondoka akawapiga Wahindi, wakamlipia ushuru.

Digitized by Google

## SULTANI DARIO NA WASIKUTHI.

Sultani Dario akataka kupiga Wasikuthi. Akatwaa watu elfu mia saba, akaondoka katika mji wake Susa, akafika hatta kwa Bosporo, ndio mlango mwembamba yatokapo maji ya Bahari Nyeusi karibu ya Stambuli. Akavukisha jeshi lake kwa daraja lililotegemea mashua mengi, akashika njia akafika mtoni Istro, unakwitwa sasa Danubi, akavuka akaingia inchi ya Wasikuthi.

Wakuu wa Wasikuthi wakakusanyika wakafanya shauri, wallakini wangine hawakukubali. Shauri lao ndilo hili, kwanza kumkaribia Dario tena kumkimbilia, marra kumkaribia marra kumkimbilia, marra nyingi vilevile, nao wakichukua mali zao zote na vitu vyote na watoto na waanake katika magari, wakiharibu tena majani na miti na vyakula vyovyote,—hivyo kumvutavuta Dario kwa nyika kuu, wapate kumshindisha kwa njaa kumpoteza jangwani yeye na watu wake. Ndivyo walivyofanya. Dario akawafuata, nao wakaendelea nyuma, wakamwongoza kwanza makusudi katika mashamba ya wakubwa wale wasiokubali shauri lao, wakawauthia sana. Kiisha wakamvuta siku nyingi hatta kufika nyikani. Dario akachoka, akafanya uchungu mwingi, akatuma mjumbe kwa sultani wa Wasikuthi, akisema. "Gissi gani kukimbia tu? Usipoogopa, tupigane. Ukiogopa, niletee maji na udongo, mimi bwana wako." Yule mfalme akamjibu, "Hatta sikimbii mimi, natembea tu. Desturi ya Wasikuthi kuhama huko na huko sikuzote. Hatuna miji, wala mashamba. Bassi hatupigani nawe. Zawadi nitakazokuletea mbalimbali. Si wewe bwana wangu." Wakafuliza kumvuta Dario kwa

Digitized by Google

nyika, hatta Dario akashikwa na matata na hatari na misiba mengi. Wasikuthi wakampelekea zawadi, ndege mmoja na panya mmoja na chura na mishale mitano. Maana ya zawadi hizo haikumwelea vema, akafanya baraza ya wakubwa akasema, "Nathani zawadi hizo ndio Wasikuthi kujitolea kabisa, kwa sababu maana ya panya ndio watu wakaao inchi hii, na ndege ndio frasi wao, na chura ndio maji ya mito na visima, na mishale ndio selaha za vita." Lakini waziri wake, jina lake Gobiria, akasema, "Nami naona zawadi hizo ndio kunena, 'Ee Waajjemi, hamna buddi ao kuruka juu kama ndege, ao kufukua chini kama panya, ao kujitupa majini kama vyura, ao kuuawa na mishale hii.'" Marra Wasikuthi wakakaribu kwa kupigana. Na tazama, sungura akaruka katikati yao, Wasikuthi wakaacha kwenda pigana, wakapiga kelele wakimfukuza sungura. Ndipo Dario akashangaa, akafanya ajabu mno, akasema, "Tazama watu hawa wanitharauvyo kabisa. Kuliko sungura, mimi si kitu." Moyo wake ukageuka, akafanya shauri la kukimbia. Akaacha kuko huko watu wake wasiofaa wala hodari kwa vita, akawaambia, "Kaeni papa hapa, naenda kutafuta Wasikuthi." Akatwaa wote wenyi nguvu akakimbia, nao walioachwa wakapatwa na Wasikuthi wakauawa. Dario akafika mtoni Istro kwa shidda, akavuka akaokoka.

Digitized by Google

## SULTANI DARIO NA WAYONANI.

Zamani za kwanza Wayonani wakakaa katika Uyonani, ndio inchi yao katika Europa, wakakaa pwani ya Anatolia (Asia Minor) kwa magaribi, wakakaa katika visiwa vyingi vya bahari iliyo katikati, inaoitwa Arkipélago. Nao wa pwani wale wakaondoka wakateka mji mkubwa Sardisi, wakauteketeza moto. Na Waatene, ndio watu wa mji ulio mkuu katika Uyonani, wakawasayidia. Sardisi mji wa Waludi, lakini siku zile Waajjemi walioumiliki. Bassi Sultani Dario alipoletewa habari kama Sardisi umeharibika pia, akafanya hasira sana. Nao Wayonani wa Asia hakuwaangalia hatta kidogo, kwa maana kitu chepesi kuwapatiliza mambo hayo. Lakini Waatene ndio aliowachukia sana, naye hajasikia habari zao, sababu wametoka mbali, akauliza, "Watu gani hao wageni?" wakamwambia. Akatwaa upindi akatia mshale katika uzi akapiga juu kwa mbingu, akisema, "Ee Muungu, unijalie niwalipize kisasi Waatene." Akaagiza mtumishi wake amwambie killa siku saa ya kula jioni, "Ee Bwana, usiwasahau Waatene."

Kwanza akapeleka mkwewe, jina lake Mardonio, awapige Waatene. Naye Mardonio akakusanya watu wengi na merikebu nyingi, akavuka Bosporo, akashika njia ya kwenda Uyonani, asifanikiwe. Washenzi wa barra wakapigana sana naye, wakamzuia njiani, merikebu zake zikavunjika na thoruba kuu karibu na mlima Atho. Akarudi kwake na watu wake.

Tena Dario akatuma wakubwa wawili, Dati na Artaferini, wakapita baharini njia ya kunyoka, wenyi merikebu nyingi na watu wengi, wakashuka

Digitized by Google

pwani katika Marathona, mji mdogo wa Waatene. Nao Waajjemi wengi sana, na Waatene haba. Waatene wakaogopa, wakuu wao wakafanya shauri wakimbie. Hatta palikuwa na mtu mmoja mkuu, jina lake Militiadi, na mtu huyu mshujaa sana na mwenyi akili, akawashawishi Waatene wakae wapigane kuko huko. Bassi wakaenda mbio wakarukia Waajjemi. Hatta Waajjemi wakastaajabu, wakiona watu haba walivyowarukia nao kwa miguu tu, hapana mwenyi frasi, wakawacheka kuwa na wazimu. Wakapigana saa nyingi. Waatene wangawa haba wakipigana taratibu na kwa ushujaa wakaweza Waajjemi wengi wengi wasiopigana kwa akili, illa vivi hivi tu kama nyama za mwitu. Waajjemi wakapigwa sana, wakauawa zayidi ya elfu sita, wakafukuzwa kwa vyombo, wakapanda wakaenda zao.

Sultani Dario akaingiwa na uchungu mwingi, wala hakukubali kushindwa na Wayonani. Hatta akipatikana na farathi, akafa.

## SULTANI SERKISI NA WAYAHUDI.

Dario alipokwisha kufariki, Serkisi mwanawe alikuwa Sultani wa Waajjemi. Akakaa miaka miwili akawatiisha Wamisri waliomwasi. Mwaka wa tatu Sultani Serkisi akaita barazani maliwali wake na wakubwa wake wote, waje kwake katika mji Susa, wafanye shauri la vita kwa Wayonani. Wakakusanyika, wakafanya shauri, wakatazama mali za Sultani zote siku mia na themanini. Kiisha Sultani

Digitized by Google

akawafanyia wote karamu kuu ya siku saba katika bustani yake. Karamu ile ikapambwa vizuri ajabu. Bassi siku ya saba Sultani akanywa mvinyo, akawaita watowashi wake saba, akawaamuru wamletee malkiya ndiye Vashti, awaonyeshe watu uzuri wake. Naye mwanamke yule mzuri sana. Mwanamke yule akakataa, akisema, "Sitaki." Sultani akafanya ghathabu, akamwondoa katika kuwa malkiya.

Baada ya siku nyingi akatafuta mke awe malkiya yake mahali pa Vashti. Palikuwa na mtu Myahudi, jina lake Matakasi (Mordecai), mngoje mlango wa jumba la Sultani. Akawa na mtoto mmoja, jina lake Ester, binti ya nduguye, akimtunza akimpenda sana. Na yule mtoto mzuri sana, akatafutwa akaletwa kwa nyumba ya waanake wa Sultani. Akakaa humo miezi kumi na miwili. Kiisha akavaa mazuri akapambwa vizuri akaingia nyumbani kwa Sultani. Yule kijana akampendeza sana Sultani, akawa malkiya yake.

Hatta siku zile watowashi wawili wa Sultani, wangoje mlango, wakafanya shauri la kumchinja. Jambo lile likajulika na Matakasi, akampasha Ester habari, naye akamjulisha Sultani. Wakatafuta watu wale wakawasulubisha.

Siku zikapita, Sultani akazidishia mtu, jina lake Hamani, kuwa waziri wake, watu wote wakamsujudia Hamani, illa Matakasi tu, naye hakumsujudia wala kumheshimu. Hamani akaona uchungu mwingi, akafanya shauri awaue watu wote pia walio Wayahudi kwa ajili ya Matakasi. Akaenda kwa Sultani akamwambia, "Ee Sultani, wako watu wabaya katika milki yako, wanakaa huko na huko mahali pote, nao mbali na watu wote, wala sheria zako hawaziangalii. Bassi naona heri wachinjwe wote pia, nami nitaweka fetha yao nyingi katika hazina za Sultani." Sultani akakubali, akatuma



Digitized by Google

wajumbe killa mahali na barua kwa maliwali, Wayahudi wote wauawe mwezi wa kumi. Yule Matakasi akapasua nguo zake akavaa sako akalia kwa sauti chungu mjini, Wayahudi wote wakalia na kufunga na kulalia sako na majifu. Matakasi akampasha Ester habari hizi, akamwagiza aende kwa Sultani awaombee Wayahudi, ndio nduguze. Naye akasema, "Siwezi, killa aingiaye kwa Sultani huko ndani, Sultani asimpungie fimbo lake, huchinjwa." Akamwambia, "Hatta usipomwingilia utachinjwa. Siwe Myahudi?" Akasema, "Ntakwenda, fungeni tu siku hizi tatu, wewe na Wayahudi wote, nami pia." Siku ya tatu akamwingilia Sultani, Sultani akampungia fimbo lake la thahabu, akisema, "Wataka nini?" Akamwambia, "Nataka wewe na Hamani, mje kula kwangu." Akasema, "Vema." Wakaja. Sultani akamwambia, "Wataka nini tena?" Akamwambia, "Nataka mje kula kwangu kesho marra ya pili. Ndipo nitakapomjulisha Sultani nitakavyo." Hamani yule akajivuna sana kwa sababu ya kwitwa marra mbili, akaenda kwake, akaona Matakasi yuko mlangoni hamwondokei vilevile, akaingiwa na uchungu. Akafika kwake akawaita wenzake na mkewe, akawaonyesha mali zake nyingi na daraja lake na mambo yote bora na makuu yaliyompata, na kwitwa kula kule na Sultani na malkiya yake. Akawaambia, "Hatta haya yote hayanifai neno, nikimwona yule Matakasi yuko anakaa mlangoni mwa Sultani." Wakamwambia, "Kesho mtakie Sultani asulubiwe." Akafurahi, akafanyiza msalaba wa mti wa mikono hamsini, ndio urefu wake.

Usiku uleule Sultani halali, akaletewa vitabu vya mambo ya ufalme wake akasomewa habari. Likasomwa jambo lile la watowashi wawili, waliotaka kumchinja mwenyewe. Sultani akasema, "Zawadi gani aliyopewa Matakasi, sababu aliniokoa?" Wa-

Digitized by Google

kamwambia, "Hapana hatta kitu." Sultani akawauliza, "Yuko nani huko uani?" Wakamjibu, "Hamani yuko." Akasema, "Mwite." Wakamwita. Sultani akamwambia, "Ikiwa Sultani anataka kutukuza mtu sana, amfanyieje?" Hamani akaona katika nafsi yake, "Atakayetukuzwa ndimi." Akasema, "Ziletwe nguo zake Sultani za kifaume, na frasi wake Sultani na taji yake Sultani, tena mtu aliye na daraja bora azipokee, amvike yule mtu Sultani atakaye kumtukuza, ampandishe juu ya frasi, amwongoze katika njia kuu ya mji, atangaze mbele yake, Hivyo ndivyo atakavyofanyiwa mtu Sultani atakaye kumtukuza." Sultani akasema, "Haya, twae nguo na frasi pia, kama ulivyosema mwenyewe, ukamfanyie vivi hivi Matakasi, yuko mlangoni mwa Sultani. Usikose hatta neno moja." Hamani akazitwaa nguo na frasi pia, akamvika Matakasi, akamwongoza kwa frasi katika njia kuu ya mji, akatangaza mbele yake, "Hivyo ndivyo atakavyofanyiwa mtu, Sultani atakaye kumtukuza." Alipokwisha kurudi, akaenda kwake kwa haraka, mwenyi uso umefunikwa, akawapasha wenzake habari. Wakamwambia, "Yule Matakasi atakushinda." Marra Hamani akaitwa aende kula na Sultani, Sultani akamwambia Ester katika karamu, "Wataka nini?" Akajibu, "Nataka nipone mwenyewe na watu wangu. Kwani tumeuzwa tuchinjwe wote pia na adui yetu." Sultani akamwuliza, "Nani yule adui yenu?" Akasema, "Mbaya huyu Hamani ndiye." Sultani akaondoka kwa ghathabu, akatoka kutembea kidogo katika bustani. Hamani akashikwa na hofu akamwomba Ester, asichinjwe mwenyewe. Sultani akarudi akaona naye Hamani ameangukia kitandani mwa Ester. Sultani akasema, "Hatta atamfanyia malkiya jeuri?" Wakamfunika Hamani uso, wakasema, "Uko msalaba kwake huyu tayari." Sultani akasema, "Msulubi-

Digitized by Google

sheni bassi." Wakamsulubisha. Moyo wa Sultani ukatulia. Akapeleka wajumbe mahali pote pa mamlaka yake na barua kwa Wayahudi, akiwapa ruhusa ya kupigana na kujilinda, ikiwa mtu anataka kuwaua. Wayahudi wakapigana na adui zao wakaua wengi. Wakafanya siku kuu wakati uleule mwaka kwa mwaka hatta kwa leo, ndio siku kuu ya Purim.

(Mambo haya yameandikwa katika kitabu cha Ester, na Sultani Serkisi ndiye Ahasuero, na Matakasi ndiye Mordecai.)

## SULTANI SERKISI NA WAYONANI.

SULTANI SERKISI akaita maliwali wake wote na wakubwa wake barazani, wafanye shauri la vita kwa Wayonani. Walipokwisha kufanya shauri, akawaagiza killa mtu kukusanya watu wengi, akafanya jeshi kubwa kubwa ajabu mno, hatta kuwa kama elfu elfu marra tatu ao zayidi, mataifa mengi, na killa mtu amevaa nguo za taifa lake na selaha zake pia. Serkisi akaondoka akafika Dardanels, ndipo mlango mwembamba wa bahari karibu ya Stambuli. Akaamuru watu wafanyize daraja la mashua nyingi, apate kulivukisha jeshi lake kwa Europa. Wakafanyiza. Ikawa thóruba kuu, daraja likavunjika. Serkisi akaghathabika sana, hatta akatuma watu waende wayapige maji yale na mjeledi, mapigo mia tatu, tena kuyatupia pingu za chuma, wakisema, "Enyi maji makorofi, nawalipia kisasi cha jeuri yenu. Kama mwapenda, kama

Digitized by Google

hampendi, Sultani Serkisi atavuka." Akawachinja wasimamizi wale waliolifanyiza daraja. Marra wakashika kazi tena wakafanyiza madaraja mawili, wakafanyiza hivi. Wakapanga mashua nyingi kwa safu upande kwa upande, safu moja yenyi mashua mia tatu na settini, wakazifunga kwa kamba nzuri na nene, wakatia magogo, na juu ya magogo makoko, na juu ya makoko udongo, wakaupigilia, wakafanyiza ua wa fito huko na huko katika madaraja, frasi wasishtuke wakivuka baharini. Na urefu wa madaraja kama mwendo wa nuss u saa. Serkisi akavukisha jeshi lake lote, na muda wa kuvukia muda wa siku saba, wakivuka mchana na usiku. Akasafiri katika barra, akipita pwani kwenda Uyonani, merikebu nyingi sana zikafuatana naye baharini. Miji yote ikamwogopa ikitoa chakula cha jeshi lake, killa mji kwa siku yake, hatta mengi kuangamia mali zao zikitumuliwa mbali, na mito mengi imekauka isiweze kuwatoshea watu na frasi.

Serkisi akafika Uyonani, hana buddi kupita Mlango wa Thermopuli, ndio njia nyembamba sana, milima huko na bahari huko. Wakawa Wayonani wamekaa kule kule njiani wakiivizia, nao si wengi. Hatta Serkisi akastaajabu, akakaa mwenyewe siku 'nne, akingoja watu wajitoiee. Halafu yake akatuma watu wawafunge wakawalete kwake wazima. Watu wale wakapigana na Wayonani wakapigwa sana, wengi wakafa. Na siku ya pili vilevile. Hatta Myonani mmoja mbaya akawaonyesha Waajjemi njia ya kuzungukia katika mlima na kufika nyuma ya Wayonani. Wayonani wakisikia habari wangine wakakimbia. Wasiparta tu waliokaa, ndio watu mia tatu tu bassi na mkuu wao, jina lake Leonida, na wangine si wengi. Na Waajjemi, hesabu yao kupita elfu elfu. Bassi ndipo mapigano makuu. Kwanza Waajjemi wakakaribia wakikatwakatwa kwa panga

Digitized by Google

na Wayonani, wakifanya hofu, wakitaka kukimbia, wakapigwa nyuma na maakida yao na maamiri, wakaendelea mbele, wakashindana tena. Sultani Serkisi amekaa kitini mwake kutazama, akaruka marra tatu katika kiti kwa hofu na kushangaa. Na Wayonani wale washujaa sana kwelikweli, wakapigana kama simba. Kwanza wakachoma Waajjemi kwa mikuke, hatta mikuke imevunjika, tena wakawachinja kwa panga, hatta panga nyingi zimepotea, wakatenda kazi kwa mikono na meno pia. Mwisho Waajjemi wale wengi wengi wakawazunguka Wayonani, watu haba sana, wakawagharikisha kama mawimbi, wakafa. Maneno haya yakaandikwa katika kaburi lao palepale walipokufa, "Ee rafiki, nenda zako Siparta, kamwambie, tumezishika sheria zake, tumekufa, bassi."

Waajjemi wakautwaa Atene, ndio mji mkubwa wa Wayonani, akauteketeza moto. Nao Waatene wakauacha mji wao, wakapanda vyomboni wote, ndilo shauri la mtu mmoja mkubwa na mwenyi akili nyingi, naye akasema, "Boma la mti, ndipo salama." Waajjemi wakapeleka merikebu, wakapigana na Waatene baharini penyi pembamba, wakapigwa sana, merikebu zao zingine zikavunjika, zingine zikatekeza pwani, zingine zikazama. Hatta Sultani Serkisi akaingiwa na hofu, akiona Wayonani walivyo hodari na washujaa, nao watu haba tu, akakimbia hatta kwake kwa haraka. Mahali pale alipopigwa baharini, panakwitwa Salamisi. Baadaye Waajjemi wakashindana na Wayonani marra mbili tu bassi, wakapigwa vile vile. Sultani Serkisi akafa.

Digitized by Google

## HABARI ZA WAYONANI.

Wayonani watu si wengi, na inchi yao ndogo. Wallakini wamepita walimwengu wote kwa sifu zao nyingi za zamani. Warumi mbali, ndio wapitao wote kwa kutiisha ulimwengu na kuutuliza kwa sheria na kwa haki. Wayahudi mbali, sifa zao kumjua Muungu, na kungojea kwa saburi mambo mema yatakayokuja. Nao Wayonani, ndio watanguliao katika kufikiri kwa akili, na kuvipambanua na kuvifanyiza vyote vilivyo vizuri. Wayonani kama wangwana, wangineo kama washenzi bado. Wayonani waalimu, waliowafuata hatta leo waanafunzi wao. Hajawa atungaye mashairi mazuri kupita Homero na Sofókili, wala afanyizaye kazi nzuri za mawe kupita Fidia, wala atiaye rangi vizuri kupita Apelli, wala atawalaye kwa shauri zuri kupita Períkili, wala aongozaye watu kwa haki kupita Sokrati, wala afikiriye kwa akili kupita Plato na Aristoteli. Na lugha yao nzuri ikaenea sana katika ulimwengu, hatta maandiko ya Waanjilisti na ya Mitume yote yameandikwa kiyonani.

## HADITHI YA ULISSE.

Homero Myonani aliyokwimba kwa mashairi zamani sana, imepata kama miaka elfu tatu.

### 1. *Ulisse na mtoto wake.*

Palikuwa na mtu mmoja Myonani, jina lake Ulisse, mfalme wa Ithaka, ndicho kisiwa katika

Digitized by Google

bahari Mediterraneo karibu ya Uyonani, na mkewe jina lake Penelope. Wakazaa mtoto mmoja wa pekee. Yule mtu akawapenda sana na mkewe na mtoto wake. Wakakaa siku nyingi. Hatta mfalme mkuu wa Wayonani akafanya vita, akawaita wafalme wote walio chini yake, akatuma wajumbe kwenda kumwita Ulisse.

Hakukubali Ulisse kuwaacha mkewe na mtoto wake, akafanya hila akajifanya kuwa mwenyi wazimu, hatta akaenda pwani akilima mchanga na ng'ombe. Wajumbe wale wakamkuta analimalima mchanga huko pwani. Ndio kazi yake. Wakafanya shauri wapate kumfahamu, ana wazimu kwelikweli ao mzima. Wakatwaa mtoto yule wa pekee, wakamchukua pwani, wakamweka pale pale katika mchanga mbele ya ng'ombe. Naye babaye hakupenda kumwua mtoto wake, akageuka kidogo katika njia yake ya kulimia, akapita upande. Bassi wajumbe wakamwita, wakampeleka vitani.

## 2. *Vita katika Troja.*

Wayonani wote wakapanda vyomboni, wakasafiri mbali baharini, wakapigana na watu wa Troja, ndio mji karibu na Stambuli, miaka kumi, wasiwashinde. Wakachoka sana wakataka kwenda zao. Wafalme wakaona haya kurudi kwao, wasipouteketeza mji kwanza. Naye Ulisse akawa mwenyi akili sana, akafanya shauri, wasipoweza kushinda kwa nguvu washinde kwa hila. Akawaambia wafalme shauri lake, wakalikubali. Bassi wakafanyiza frasi mkubwa ajabu kwa mbau, nao mtupu ndani, hamna kitu, nafasi tu. Wakaweka ndani yake watu hodari arobaini wenyi selaha, wakamwacha frasi amesimamishwa kule pwani, wakapanda vyomboni, wakaenda zao si mbali. Watu wa mji walipoona Wayonani wana-

Digitized by Google

kwenda zao, wakatoka kwa furaha, wakashangaa wakitazama frasi yule mkubwa anasimama pwani. Hatta mtu mmoja mkohani akaingia shaka, akampiga frasi mkuke katika matumbo, yakalia wazi. Akalia, "Hiyo ndio hila." Marra majoka mawili makubwa wakapanda baharini wakamshika yule mkohani na watoto wake wawili pia, wakawasonga, wakafa. Watu wa mji wakaogopa, wakasemana, "Frasi huyu amewekwa wakfu. Haya tumpandishe mjini." Wakampandisha wote pamoja, na wazee na vijana na waanake na watoto, wakikokota kwa kamba wakishangilia na kufurahi. Hatta ukiwa usiku watu wale waliomo ndani wakatoka, wakawatolea wenzio alama ya moto, wakaufungua mlango wa mji. Wayonani wakarudi pwani upesi, wakautwaa mji, wakauteketeza moto.

### 3. *Ulisse na Wakikoni.*

Mji Troja ulipokwisha haribika, Wayonani wote wakapanda vyomboni wakafunga safari kwenda kwao. Naye Ulisse akachagua watu akawapandisha vyomboni, akaenda zake, akitamani sana kwa nafsi yake kumtazama mkewe na mtoto wake wa pekee, aliowaacha huko kwake. Pepo zikamsukuma kwa inchi ya Wakikoni, akashuka pwani, wenziwe wengi wakafuatana naye, wakapigana na Wakikoni wa mji akawashinda, wakauteka mji, wakatwaa mateka, wakayagawanya, killa mtu akipata sehemu yake. Hatta Ulisse akawaonya kuingia vyomboni kwenda zao, nao hawakukubali. Wakakaa kitako pwani wakafanya karamu wakala wakanywa mvinyo. Bassi Wakikoni waliobaki wakaenda kwita wenzio waliokaa barrani, wakaja watu wengi na wenyi frasi, wengi wengi kama mchanga, kama majani. Wakapigana sana, wakitupiana na

Digitized by Google

mikule ya shaba mchana kuchwa. Hatta jua lichwapo Wakikoni wakashinda, wakachinja watu wengi wa Ulisse, nao wangine wakakimbia wakaokoka vyomboni.

### 4. *Ulisse na Walotofagi.*

Wakashika njia baharini wakafika inchi ya Walotofagi, ndio watu chakula chao loto. Ile loto ni boga, na boga lile kazi yake hii. Killa alilaye boga lile, marra moja amekwisha kuisahau inchi yake, hatamani kurudi kwake hatta kidogo, illa kukaa tu na kula loto. Ulisse na wenziwe wakashuka pwani wakapika chakula. Akatuma watu watatu kwenda kuzumgumza na Walotofagi, wapate habari zao. Walotofagi wakawakaribisha, wakawalisha loto. Walipokwisha kuila loto, marra moyo wao umegeuka, wamesahau kwao. Wakakaa wakikataa kurejea pwani. Wallakini Ulisse akaamuru watu, nao wakawachukua kwa nguvu wakitoka machozi wakiombaomba wakishindana, wakawaweka vyomboni chini wakawafunga sana, wakatweka matanga wakienda zao upesi.

### 5. *Ulisse na Mkuklopi.*

Wakaenda katika bahari kule katika kuja zao hatta inchi ngine, inchi ya Wakuklopi, ndio inchi nzuri sana, huzaa yenyewe mtama na mchele na mizabibu wasilime watu wala kupanda mbegu hatta kidogo. Nao Wakuklopi watu warefu mno ajabu, wenyi mioyo mibaya, hawaabudu Muungu, hawashiki sheria, hawatendeani haki wao kwa wao, hukaa katika milima, killa mtu peke yake akimiliki mali zake, kazi yao kuchunga kondoo tu bassi, na kula nyama ya waana Adamu. Bassi Ulisse akashuka, akawaambia wenzi wake, "Haya, twende zetu baathi, tukawatazame watu gani wa-

Digitized by Google

kaao hapa, ao wema ao wabaya." Nao wakatia nanga wakashuka pwani wakatembea. Hatta wakaona paango kubwa karibu na pwani penyi miti mengi, liko zizi kubwa mbele yake limezungukwa na ua wa miti na mbau hodari sana, limejaa ndani kondoo wengi na mbuzi. Naye mwenyewe hayuko kwake. Ulisse akawaonya watu warudi chomboni illa thenashara tu, nao wakafuatana naye. Wakaingia katika paango wakitazama killa kitu, vimo vyombo jamii nzima, mitungi na ndoo na mabakuli yamejaa maziwa yote. Bassi watu wale wakafanya shauri kutwaa vitu kwenda zao marra moja, lakini Ulisse akawazuia akiwashawishi wakae kuko huko kumngojea mwenyewe. Wakawasha moto, wakatwaa chakula wakapika wakala wakangoja. Halafu yule Mkuklopi akarudi kwake, mtu mrefu mno mwenyi uso mbaya, ana jicho moja katikati ya paji la uso wake, naye jina lake Polufemo. Akawa analeta kondoo wengi katika shamba, na mzigo wa kuni begani mwake, akawapeleka kondoo ndani ya zizi akazivumisha kuni chini. Tena akafunga zizi kwa jiwe, nalo jiwe kubwa sana, hatta watu asharini na wawili hawawezi kulichukua. Kiisha kutia jiwe, akawakama mbuzi, akaweka maziwa katika vyombo, akawasha moto, marra akawaona watu wako wanaketi humo paangoni. Akawaambia vikali, "Nani ninyi? mmetokapi? shughuli gani mlio nao?" Wakashangaa wakaogopa sana sauti yake kama ya radi. Hatta Ulisse akamjibu akisema, "Wayonani sisi. Tumetoka katika Troja, tunarudi kwetu. Bassi sisi maskini wa Muungu, twakusihi tupewe ada twende zetu." Akawaambia, "Wajinga ninyi, mmetoka mbali sana kwelikweli nanyi, bado kutujua sisi Wakuklopi hatumheshimu Muungu wala kumwangalia. Kiko wapi chombo chako bassi?" Ulisse akajibu kwa uwongo, akisema, "Chombo limekwisha

Digitized by Google

vunjika, sisi tu tuliookoka, hakuna mtu tena." Yule Mkuklopi akanyamaza, akawarukia gháfala, akakamata watu wawili akawapiga vitwa chini, akawararua vipande vipande akawala. Alipokwisha kula akalala usingizi. Ulisse akafanya shauri kwa roho yake, "Nimchome upanga palepale akilala? Lakini hatuwezi kujongeza lile jiwe limewekwa huko mlangoni. Shauri hilo halifai."

Hatta assubui yule Mkuklopi akiamka akafanya vile vile, akikamata watu wawili akiwala. Alipokwisha kushiba chakula akaondoka akaenda zake akichunga kondoo mchana kuchwa. Kwanza akaweka jiwe lile mlangoni, watu wasipate kutoka kukimbia. Hatta jioni akarejea, akawarukia akakamata wawili akawararua vipande vipande akawala. Ndipo Ulisse akafanya shauri lililofaa. Marra Mkuklopi alipokwisha kushiba chakula, Ulisse akamtolea mvinyo, na mvinyo ule ndio mwenyi nguvu sana, ukatekwa katika mji wa Wakikoni. Mtu akinywa asichanganye maji tele kwanza marra hulewa. Ulisse akamwambia, "Haya, rafiki, twae kanywe, mvinyo huu ndio mzuri na mtamu sana. Nimeuleta sadaka kwako. Nawe una wazimo, hukaribishi wageni vema." Yule Mkuklopi akanywa akapendezewa mno, akasema, "Haya lete tena. Nitakupa zawadi yako." Akanywa hatta marra tatu. Ulisse akamwambia, "Jina langu mimi ndilo Hapana mtu. Nipe zawadi bass." Akajibu, "Hapana mtu ataliwa wa mwisho. Ndio zawadi yake." Akalewa Mkuklopi akajinyosha chini kwa tani, akikokomoka makombo ya nyama, akalala usingizi mzito. Ulisse akaondoka akatwaa mti, akauchongachonga akachoma moto, akawaagiza wenzi wake waliosalia killa mtu kazi yake na mahali pake, wapate kumsayidia taratibu, akapanda mwenyewe juu ya meza, akaupiga mti katika jicho la Mkuklopi, nao mti

Digitized by Google

mwenyi motò sana unang'aa, akaushindilia chini, wenziwe wakaushika huko na huko wakapekecha-pekecha kwa bidii. Jicho likatoka damu na moshi, likiharibika kabisa. Yule Mkuklopi akalia ajabu, akifingirika akijinyonganyonga akipiga kiyowe, asiweze kuuondoa mti katika jicho lake. hatta walo wakashikwa na hofu wakakimbia wakajificha kimya huko na huko paangoni. Bassi yule akaondoka akawatafuta pote akipapasa na mikono, hatta akachoka akakaa, asiwapate. Ilipofika assubui, Ulisse akafanya shauri. Akawakamatia wenzi wake killa mtu kondoo wawili, nao kondoo wale wakubwa sana, akawafunga kwa kamba, kondoo wawili na mtu mmoja katikati. Halafu yake Mkuklopi akaamka akasema. "Nitatoa kondoo wangu waende wale nje, tena nitawakamata wale wabaya nitawala." Akaliondoa jiwe akafungua mlango wa zizi, kondoo wakatoka na watu wakichukuliwa nao. Akabaki Ulisse tu bass. Akatwaa kondoo mume aliye mkubwa sana mwenyi nyele ndefu, akajitundika chini ya tumbo lake akishika sana ngozi ya kondoo. Naye Mkuklopi akastaajabu kwa sababu yule kondoo mume hakutangulia kutoka zizini, nao ndio desturi yake, akamwambia, "Ewe kwa nini kuchelewa leo? Siku zote umezoea kutoka wa kwanza, leo umekawia nawe." Akamgusa kondoo mume akapapasa pia, asitambue aliko Ulisse huko chini yake anachukuliwa.

Bassi walipokwisha toka wote salama, wakafika pwani wakapanda chomboni wakapiga makasia, ndipo Ulisse alipomwita Mkuklopi akimfanyia thihaki sana. Mkuklopi akamsikia akafika mbio pwani akatwaa mwamba mkubwa akakitupia chombo, asikipate. Mwamba ukianguka majini upande wa pili wa chombo na karibu yake ukakikaribisha pwani. Yule Mkuklopi akaruka akaingia baharini akipiga

Digitized by Google

makelele akitupa mawe, asiwapate. Tena akawaita jirani wake waliokaa karibu, wakatoka wengi na warefu mno na wakali, wakaja wakamwuliza, "Unani wee? Huwezi nini?" Akajibu, "Ee rafiki, Hapana mtu aliyeniumiza, Hapana mtu," sababu Hapana mtu ndio jina lake Ulisse alilomwambia. Watu wale wakamcheka sana, "Ah! Hapana mtu! Bassi wee, bassi. Mbona umetuita? Labuda huwezi tumbo. Haya, twende zetu." Wakarudi kwao. Naye Ulisse na jamaa yake wakaenda katika bahari katika kuja kwao.

### 6. *Ulisse na Aiolo.*

Bassi wakaenda hatta wakawasili katika kisiwa. Na kisiwa kimekwitwa kisiwa cha Aiolo, ndio jina lake mwenyi kisiwa. Chaenda juu sana katika bahari, kama mwamba mtupu pande zote, na juu yake boma la shaba na jumba kubwa. Ndipo anapokaa mwenyewe Aiolo na mkewe na watoto wake thenashara, waume sita na wake sita. Naye Sultani wa 'pepo zote, ndio kazi yake kuzitawala.

Wakashuka, wakapanda juu ya mwamba, yule akawakaribisha akawatendea mazuri akiwalisha mwezi mzima, wakakaa raha, wakila wakimpa habari zote za safari yao. Bassi walipokwisha kupumzika katika taabu ya bahari ile, wakaomba ruhusa kwenda zao, wakapewa. Sultani yule akatia pepo zote pia katika mfuko, zisivume njiani safari yao isizuiliwe, akafunga mfuko kwa kamba akampa Ulisse, naye akauweka ndani ya chombo chini. Wakaenda zao baharini, safari ile ikafanikiwa sana, hatta wakakaribia inchi yao wenyewe.

Bassi wenzi wake Ulisse wakasemana, "Tazama, sisi fukara hahehohe, na bwana huyu mwenyi mali sana. Mfuko ule unani? Umejaa fetha labuda. Haya, bwana akilala usingizi tutamfungulia mfuko

Digitized by Google

wake tutazame ndani tupate kujua, kama imo hazina kwelikweli." Wakangoja usiku, Ulisse akalala usingizi, nao wenziwe wakafungua mfuko. Marra 'pepo zote zimetokea kwa nguvu, zikavirukia vyombo vyote zikivuma zikipeperusha, hatta zikavipeperushia mbali baharini, inchi yao isionekane tena hatta kidogo. Wakasukumiwa na pepo kwa kisiwa kilekile cha Aiolo, wakamtakia safari njema ya pili, wasipate. Yule akawatukana akawafukuza vikali. Wakaenda zao, wakifanya huzuni nyingi ya ujinga wao na choyo chao.

### 7. *Ulisse na Walaistrugoni.*

Wakasafiri wakafika hatta inchi ya Laistrugoni, wakajongezea vyombo pwani penyi miamba miwili mirefu huko na huko, na kati ya miamba mlango mwembamba wa kuingilia bandarini, na bandari iliyomo nzuri sana. Wakavifunga vyombo ndani, Ulisse akapanda juu ya mwamba apeleleze inchi na watu walioko. Akaona mji mwenyi boma kubwa, akatelemka, akawapasha wenziwe habari, akatuma watatu kwenda mjini kuuvizia. Bassi wale watatu wakaenda wakakuta kijana mwanamke anateka maji kisimani, akawaonyesha njia ya kwenda nyumbani kwa babaye. Wakakaribu wakabisha hodi, akaitikia mwanamke mrefu mno, kama mnazi, hatta wakamchukia. Marra yule akamwita mumewe yuko sokoni, akafanya shauri la kuwachinja. Akakamata mmoja akamchinja kwa chakula, wawili wakakimbia. Yule akapiga kelele kwa wenziwe wakaja wakawafukuza hatta pwani. Wakatwaa mikuke na mawe makubwa, wakawatupia watu na vyombo. Watu wakalia sana wakichomwa kwa mikuke, vyombo vikafanya mshindo vikivunjikavunjika kwa mawe. Walaistrugoni wakavua wengi kama samaki, waka-

Digitized by Google

wachukua, wakachoma moto wakawala. Chombo cha Ulisse tu kimesalia, naye akaikata kamba, akaenda baharini hima.

## 8. *Ulisse na Kirki.*

Wakasafiri wakaja zao hatta kisiwa cha pili. Kisiwa kile kinakwitwa Aiaia. Wakashuka wakakaa siku tatu. Hatta Ulisse akapanda kilima, akaona moshi. Akachagua watu asharini na wawili waende kupeleleza. Wakaenda katika mwitu hatta wakafika mahali peupe, iko nyumba kubwa na nzuri, wakasikia sauti ya mtu anakwimba ndani. Wakapiga moyo konde, wakakaribia, wakaona mwanamke mzuri anafanya kazi ya kutarizi naye akiimbaimba katika kazi yake. Akawaita, "Karibuni wangwana, karibuni wangwana, kafungueni kinwa." Na mwanamke yule ndiye mchawi, pana katika nyumba chui tele na simba na mbwa wa mwitu wakitembea ndani, nao wamegeuka katika hali ya kuwa waana adamu kwa uchawi wake, wakawa nyama, wakakaa huko ndani. Bassi Kirki, ndilo jina lake mchawi, akawakaribisha mezani, meza imejaa vyakula vya mali na vitamu. Wakakaa kitako, wakala wote, illa mtu mmoja tu, jina lake Eurialo, naye hakula, amekaa uani nje, kwa maana hatumaini mambo haya kuwa mema. Kiisha kula, mchawi akawapiga fimbo ya uchawi wake, marra wamekuwa nguruwe, akawafunga katika mazizi. Wakawa kama nguruwe uso na mwili na sauti pia, lakini wenyi moyo wa kwanza na akili za kwanza. Yule Eurialo, yule aliyekaa nje huko, akakimbia akampasha Ulisse habari zao. Ulisse akawa mtu mshujaa sana, hana hofu hatta kidogo, akawapenda wenziwe kuliko uzima wake mwenyewe. Akaondoka akaenda peke yake mwituni, jini akamkuta njiani akamwonyesha

Digitized by Google

boga, jina lake molu, mtu akiwa na hilo hapatikani na uchawi. Akafurahi Ulisse akafika hatta nyumba ile nzuri akaingia. Kirki akamkaribisha akimtendea vizuri akimkalisha mezani, tena akamwandalia chakula akatia dawa baya akamletea ale. Naye akiisha kula, akampiga fimbo ya uchawi akisema, "Haya, nenda zizini kwa wenzio ndio nguruwe." Haendi Ulisse, hageuki hatta kidogo, molu ile ginsi ilivyomfaa, akavuta upanga wake akamrukia yule mchawi, kama anataka kumua. Kirki akapiga kiyowe, E-e-e-e-e! akaanguka chini, akamnasihi, "Ee Bwana, bassi bwana, usiniue. Mimi hapa nitafanya killa upendayo mwenyewe." Akamwapia uapo ulio mkuu. Ulisse akamwambia, "Jambo la kwanza, uwageuze wenzangu kwa hali ya kwanza. Jambo la pili, huna buddi kunipa habari za mwendo wangu, mambo gani yatakayonipata." Kirki akaenda mbio kwa mazizi, akawaleta wale wenziwe, akawapaka dawa killa mtu, wakageuka kwa uso wa kwanza na mwili wa kwanza. Kiisha akawafanyia karamu, wakala wakanywa, akampa Ulisse habari zote za njia atakayokwenda. Akawaambia, "Kua herini." Wakasema, "Kua heri." Wakaenda zao.

### 9. *Ulisse na wafu.*

Wakasafiri sika nyingi wakafika hatta mpakani mwa bahari kuu, ndipo inchi ya Kimmeri. Wakashuka pwani, wakatoa kondoo walioleta katika chombo, wakaenda zao kando la bahari hatta kwa mahali paliponenwa na Kirki. Na inchi ile yenyi giza tupu siku zote. Mchana na usiku. Haliangazi jua huko hatta kidogo wala lichapo wala lichwapo, ulimwengu umefunikwa dayima na mawingu manene na maghubari. Bassi walipokuja kule, Ulisse akavuta upanga mkali, akafukua shimo urefu wake



Digitized by Google

kama mkono mmoja huko na huko. Tena akatoa kafara ya kunywa pande zote za shimo, asali na mvinyo na maji, akatawanya unga juu, akasali kwa maneno mengi. Wenzake wawili wakashika kondoo, naye Ulisse akamchinja kondoo juu ya shimo, damu ikaingia shimoni. Marra wafu wakaonekana wengi wengi, wakitoka katika chini ya inchi, wakisongana-songana wakitaka kuionja damu ile, wapate nguvu za kujizumgumza naye Ulisse, Ulisse akawazuia kwa upanga, hakuwaacha kunywa damu, illa taratibu tu na mmoja mmoja, alivyopenda yeye.

Kwanza akakaribisha nabii mkuu wa Wayonani, jina lake Tiresia, akamjalia damu, ndio iliyomwezesha kunena vema, akampasha Ulisse habari nyingi za kusafiri katika kwenda kwake na za hatari zote na misiba pia yatakayompata njiani, na habari ya kufa kwake mwenyewe. Wa pili na mamaye akakaribu akanywa akasema naye, akamjulisha mambo ya nyumbani huko katika Ithaka, ndio inchi yake, ya kwamba mkewe anamtamani sana siku zote, hatta na kumkalia eda imepata miaka kumi na minane, na watu wengi, wakubwa na wenyi mali, wakimposa wakimjia siku kwa siku, naye hataki, huwafanyia hila asipatwe nao, hufuliza akitoka machozi na kufikiri yule mumewe yuko katika kupotea mbali ao labuda amekufa, hakuna kufarijika illa wageni wafikapo tu, naye bibi huwakaribisha vizuri huwauliza habari akitafutatafuta mambo ya mumewe, ndio faraja yake. Hatta na mtoto yule wa pekee, sasa amekua, mtu mzima, naye hukaa huzunini akimngojea baba akimtazamia sana akimtafuta huko na huko. Na baba mzee sana amekwenda mashamba anafifia kwa taabu na hamu peke yake, hapendi kula, hulalia magumu, wala hana amwangaliaye. Na habari ya mamaye mwenyewe, ndio amekufa kwa huzuni na kumtazamia mwana wake, ndiye Ulisse, naye haji siku zote.

Digitized by Google

Ulisse akalia sana akisikia habari hizo za nyumbani akataka kumkumbatia mamaye, asiweze kumshika mikononi mwake, kwa maana yu pepo mwenyi umbo la mwana Adamu, hana mwili kwelikweli, wala hapapasiki. Akajaribia marra ya pili, asimpate, akajaribia marra ya tatu, asimpate. Akalia sana.

Pepo wengi wa wenziwe waliokufa zamani wakamtokea wakazumgumza naye wakamwarifu mambo yao, wakimwuliza habari za watu. Kiisha akaondoka, akaenda zake kule chomboni. Wakapanda wakapiga makasia, halafu yake baridi nzuri ikawasukuma katika njia yao.

## 10. *Ulisse na Masairini.*

Wakasafiri siku nyingi, wakawasili katika kisiwa cha Masairini. Na Masairini ndio waanake wachawi, wabaya sana, wenyi kwimba nyimbo kwa sauti nzuri nzuri isiyofanana na kitu kwa kuwa nzuri. Kazi yao, hukaa pwani, killa apitaye baharini humwimbia nyimbo kwa sauti nzuri na tamu, naye akisikia hakosi marra kuchukia mambo yote mangineyo illa kwenda upesi kuzisikiliza zile nyimbo. Bassi huenda, hukamatwa na Masairini, huliwa. Nako mifupa mengi ya watu huko pwani, chungu chungu.

Siku hiyo chombo cha Ulisse kikakaribia kisiwani kule, upepo ukatulia ikawa shwari, wakapiga makasia, wakafika karibu, wakasikia Masairini wanaimba zile zile. Marra Ulisse akaondoka kwa haraka akatwaa nta, akakata kipande kikubwa, akaikandakanda kwa mikono, hatta na jua likaiyeyusha, akawapaka wenziwe wote masikio pia, wasipate kusikiliza nyimbo za Masairini wanazokwimba. Ndivyo alivyoamriwa kufanya na Kirki. Na tena hivi roho yake mwenyewe ikataka sana kusikia kidogo. Bassi

Digitized by Google

akaagiza wenziwe, wakamfunga kwa kamba penyi mlingote, asiweze kujimudu hatta kidole kimoja, nao wakavuta makasia kwa bidii, hawakusikia neno, Ulisse tu aliyesikia wanavyomwimbia, wakamwimbia hivi, " Ee Ulisse, munyi mkuu, karibu karibu, jongeze chombo pwani utusikilize maneno yetu. Hakuna mtu apitaye asitusikilize kwanza, hukaa siku zote wakifurahi wakipata habari tele. Naswi tumesikia sifa zako za vitani katika Troja, tena tunazo habari nyingi za mambo yatakayokuja duniani." Akafanya wazimo, akishindwa na uchawi ule, akataka sana kushuka pwani, hawezi, amefungwa, akawalilia sana wale wenzi wake wamfungue, haifai, wamepakwa dawa killa mtu masikioni hawamwangalii, akawakonyezea kwa macho, akikunjana uso, haifai. Hatta watu wawili walio rafiki zake sana wakaondoka wakazidi kumkazia kamba, hatta chombo kimekwisha kupitia mbali kidogo, nazo nyimbo hazisikiliki, akili zake Ulisse zikamtulilia akapata hajambo, akamshukuru Muungu.

## 11. *Ulisse penyi Sikula na Karubidisi.*

Wakashika safari, hatta hawana buddi kupita pembamba pa bahari, napo penyi hofu na mashaka sana. Pana mwamba huko na mwamba huko, nafasi haba katikati, maji mengi. Mwamba mmoja mdogo, hauendi juu sana, mwenyi hatari chini. Maji yale yakipita kassi, huzunguka-zunguka chini yake, hufanya mawimbi makubwa yakivuma yakitoka moshi yakichemkachemka kama maji yachemkavyo katika sufuria, na shimo kati. Na habari ya shimo, killa siku marra tatu hutoa maji yake kwa nguvu, huyarusha juu, pofu lafika mawinguni, marra tatu huyameza chini sana, maji yakiboromoka chini, hatta na inchi kuonekana chini ya bahari. Zimo

Digitized by Google

mbau na milingote na vipande vya vyombo, vilivyozama na kuvunjika, vyingi. Na mazunguko yale ya maji yamekwitwa Karubidisi, ndilo jina lao.

Mwamba wa pili mkubwa na mrefu unakwenda juu sawa na laini kama kioo, hapana kuupanda wala kuutelemka hatta akiwa mtu na mikono asharini na miguu asharini, nako chini paango, na katika paango nyama ya ajabu na kuogofya, ndiye joka naye mwenyi mikono kumi na miwili na mashingo saba marefu, killa shingo na kitwa chake, vitwa saba, na killa kitwa meno makali safu tatu. Kazi yake kukaa mle ndani, kuvizia vyombo vinapita karibu, marra hutoa mashingo yale marefu, hukamata watu huwameza. Jina lake Sikula.

Naye Ulisse ametangulia kupewa habari yake na Kirki. Bassi walipokaribia wakiona vumi na kishindo cha mawimbi na moshi pia wakasangaa wakataka kwenda nyuma, wasiweze. Shuti kupitia njia hiyohiyo. Bassi Ulisse akafanya shauri na nafsi yake hivi, "Nifanyeje? Nipoteze chombo na watu wote wenzangu na roho yangu mimi? Naona heri wangine waokoke. Kweli ndio afathali, tupite upande wa paango." Akawaagiza wenziwe na rubani wake wapige makasia sana waepuke mawimbi makubwa, wasogee upande wa mwamba mkubwa. Wakamtii, hawakujua ya paango na yule joka. Bassi Ulisse akavaa selaha, akasimama katika gubeti kungoja mbele, chombo kiko katika kupenya palepale, mawimbi huko mwamba huko, watu wanatazamia mawimbi yakiruka yakizungukazunguka kwa nguvu na mashindo, yule joka akawagundulia, akatoa mashingo yake marefu, akakamata killa shingo mtu mmoja, watu saba, akawatupa humo paangoni kama samaki, wakipiga kiyowe wakimlilia Ulisse. Hatta yeye akasikiliza kelele, asipate kuwaponya. Aona miguu yao tu, wakichukuliwa paangoni, asikia

Digitized by Google

sauti bass. Chombo kikapitia upesi, kikaenda zake. Akalia sana, yeye na wenziwe waliobaki.

### 12. *Ulisse na ng'ombe.*

Wakasafiri hatta wakawasili kisiwa chingine, panapo ng'ombe wengi wazuri waliowekwa wakfu. Naye Ulisse alijua habari zao, ya kwamba kumegombezwa kuwachinja ng'ombe hao, mtu akichinja hatta mmoja hakosi kuuliwa mbali. Bassi akanasihi sana wenziwe waendelee mbele wasiposhuka kisiwani kule, nao hawakukubali kupita, wamechoka, wataka kupumzika katika taabu ile ya bahari. Wakapatana naye, wakamtolea nathiri, "Tutakula pwani tutalala bassi, kesho assubui tutakwenda zetu." Wakashuka pwani, wakala wakalala. Ikawa thoruba kuu, ikishinda siku nyingi, hatta hali yao hawana chakula. Ulisse akafathaika, akaondoka akaenda tembea peke yake kidogo apate nafasi ya kumwombea Muungu katika shidda zake na taabu yake. Alipokwisha kwenda, wale wenziwe wakakamata ng'ombe wakamchinja wakamla. Halafu yake Ulisse akarudi, marra nyama ikamnukia vizuri, akajua ng'ombe amekwisha chinjwa. Akafanya hofu rohoni mwake, asitoe neno hatta moja. Wakapanda chomboni wakashika safari, wala hawajaenda mbali, ikawa tufanu tena, chombo kikakamatwa kikichukuliwa na mawimbi huko na huko, mwisho kikavunjikavunjika, watu wote wakazama wakafa, illa Ulisse tu. Naye kwanza kuogolea, akashika mlingote, akaupanda kama frasi, akichukuliwa huko na huko baharini vilevile siku nyingi asijue yu wapi.

### 13. *Ulisse na Kalupiso.*

Akachukuliwa kwa mlingote hatta kwa kisiwa kinachokwitwa Ogugia, panapokaa mwanamke mmoja

Digitized by Google

peke yake, mzuri sana, jina lake Kalupiso, naye zimwi. Akakaa katika paango, mahali pazuri sana pasipofanana na kitu kwa uzuri. Paango lile liko katika bustani yenyi miti mingi na mizuri, na maua rangi zote, na jamii ya matunda, na ndege wengi wakifanya matundu huko wakipiga sauti nzuri. Moto ukawaka ndani, namo manukato, uudi na ubani na mdalasini. Naye mwenyewe kazi yake kutarizi, hutarizi huimbaimba vizuri sikuzote. Ukawa mzabibu mkubwa mbele ya paango mwenyi matawi mengi, na chemchemi 'nne zikitoka maji ya baridi zikipita huko na huko na huko na huko. Pazuri sana pale kwelikweli. Ulisse akapanda pwani kwa shidda, amethoofika kwa kukaa sana baharini. Yule mwanamke akamtokea akamkaribisha akamlisha chakula akamtunza sana siku nyingi. Wallakini Ulisse, hakuna kwake kitu cha kutamanika illa kimoja tu, ndicho kwenda kwa inchi yake yeye, ndicho moyo wake ukitakacho sikuzote, kwa maana amependa sana mkewe na mtoto wake aliowaacha nyuma tokea zamani, nao wanamtazamia na kungojea, wasikome. Na kwenda kwake hakuyamkini, kisiwa kile kimezungukwa na maji, naye hana mashua, hana hatta mabawa, na yule mwanamke humvuta akae naye, hujaribu kumsahaulisha mkewe na mtoto, asiweze. Akakaa kwa nguvu, akitoka machozi akipotea peke yake killa siku pwani akipenyesha macho mbali katika bahari, wala hakuwasahau mkewe na mtoto hatta kidogo. Hatta mwisho yule mwanamke akaamriwa na Muungu amwache Ulisse aende zake asimzuie tena. Naye alipoamriwa hivi, akampeleka mahali penyi miti mizuri, akamtolea samani za serimala, akafanyiza mashua kwa akili. Akakata miti asharini, akapasua mbau, akapiga shoka, akazichonga vizuri akazikaza mbavuni, akatenda kazi hatta akaimaliza mashua. Aka-

Digitized by Google

fanyiza mlingote na foramali na shikio, akaushua kwa nyenzo, akasafiri furaha.

### 14. *Ulisse katika Faiekia.*

Akaenda baharini siku nyingi, siku kumi na nane, yee peke yake na mtumbwi wake katika bahari kuu asipoona inchi, illa nyota tu ndizo alizoangalia sana, hatta hakulala usingizi usiku kucha kwa kusudi asikose kunyosha njia vema akiziangalia sana nyota zile alizomfundisha Kalupiso. Siku ya kumi na nane inchi ikamtokea mbali, moyo wake ukafurahi, ukiona ndio mwisho wa taabu zake. Akakaribia pwani, marra thoruba ikamwangukia, mashua ile ikavunjika vipandevipande, hana kitu cha kushikia, akaogolea, mawimbi yakamtupa mwambani yakamkokota nyuma, hawezi kuushika mwamba vema, ngozi ya vidole vyake ikachubuka. Akaogolea tena, hatta akaona mahali palipotoka mto, akaingia akatoka pwani, naye hawezi kwenda kwa miguu, amethoofika sana amekonda kwa njaa amesumbuka sana na maji, akaanguka maguguni akipatikana na ulegevu na usingizi mzito. Inchi ile ni kisiwa, kinakwitwa Faiekia, na mkuu wa kisiwa, jina lake Alkinoo. Binti ya mfalme siku ile ile akaenda pwani na wajakazi wake, wafue nguo mtoni, kiisha kufua, wakacheza pira, hatta pira ikatupwa mbali, ikafika penyi anapolala Ulisse. Akaamka, naye hana hatta nguo, zote zimeoza kwa maji, akawatokea uchi mwenyi tawi la majani mkononi mwake, na nyele ndefu zisizong'olewa kitwani. Wakafanya hofu wakakimbia, illa binti yule wa mfalme tu, naye akakaa akamkaribisha vizuri akamwonyesha njia ya kwenda mjini. Kijana yule, jina lake Nausikaa. Mfalme akamtendea mazuri, akamwuliza habari ya mambo yote yaliyompata njiani akamtazamisha mali zake

Digitized by Google

mwenyewe na ngoma ya watu wake na michezo yao, halafu yake akampeleka kwake chomboni.

### 15. *Ulisse na mke wake.*

Akafika kwa inchi yake ndio Ithaka, akajifanya maskini akaenda nyumbani kwake, apate kutambua kama habari zile za nyumbani zi kweli ao uwongo, wala hakujulika na mtu kwanza, ginsi alivyogeuka kwa safari ya miaka asharini na kwa nguo za umasikini, illa na mbwa wake, naye mbwa mzee sana hatta alipokwisha kumtambua uso bwana wake akafa. Ulisse akakuta jumba lake limejaa watu wengi wenyi jeuri, nao walevi na washerati, wanamsumbua sana mke wake siku kwa siku wakimposa wakimwangamiza mali zake, wakimtharau mtoto wake. Naye kazi yake kukaa ndani na wajakazi wake, na kumlilia na kumtazamia mumewe. Bassi Ulisse akafanya shauri, akawaua watu wale wabaya, akajulikana na mkewe na mtoto, roho zao zikafurahi, roho zao zikaona kama wamekwenda ingia peponi, kwa roho zao zilivyofurahi. Wakakaa siku nyingi raha na mustarehe.

## KROISO NA SOLON.

Palikuwa na mfalme wa Waludi katika Anatolia (Asia Minor), na mji wake Sardis, akafanikiwa sana, akapata mali nyingi nyingi akasitawi hatta habari zake zikaenea katika ulimwengu, kama mfalme huyu ndiye mwenyi mali. Na mfalme huyu jina lake

Digitized by Google

Kroiso. Hatta siku moja akafika kwake mtu Myonani naye mwenyi akili nyingi na busara, jina lake Solon. Yule mfalme akamkaribisha furaha akamtendea mazuri, kwa hesabu alijua habari yake ya kwamba Wayonani wote wenyi akili, lakini huyo aliyewapita wote ndugu zake, akasema, "Huyu atayatambua mambo yangu, kama hapana mtu katika ulimwengu aliye heri kama mimi." Akawaagiza watumishi wake waende wamwonyeshe Solon mali zake zote na hasina yake na pambo la nyumba na fetha zake na vitu vyake vyote vizuri na vya thamani. Wakamwonyesha vyote. Vilipokwisha kutazamiwa vyote, yule mfalme akamwita Solon akamwuliza, "Ewe Solon, nimejua habari zako ya kwamba umepita watu wote kwa kuwa na akili nyingi na busara. Bassi nataka uniambie, nani aliye heri kuliko watu wote uliokutana nao." Solon hakujipendekeza kwa mfalme hatta kidogo, akamjibu, "Ee mfalme, Tello Mwatene, ndiye mtu aliye heri." Yule mfalme akastaajabu akamwambia, "Kwa nini?" Akamwambia, "Kwa sababu ya kwanza, mji wake ukasitawi siku zake zote, ya pili akazaa watoto wazuri na wema, na mambo ya watoto wale mema na habari zao njema siku zake zote, ya mwisho akafa mwenyewe kwa heshima na sifa nyingi, akipigana na adui akiwafukuza. Watu wake wakamzika pale pale alipokufa, kwa heshima na utukufu mwingi." Yule mfalme akasangaa, akasema, "Na wa pili je baada yake yeye?" akiwaza kwa roho yake, "Sikosi kuwa wa pili mimi." Naye akamjibu, "Kleobisi na Biton, Waargi. Vijana hao wenyi jamaa bora na mali nyingi na nguvu tele. Na habari zao ndizo hizi. Waargi wakifanya siku kuu, kwa desturi za siku kuu wakataka kupeleka mama wa vijana wale hekaluni katika gari la ng'ombe wawili, ng'ombe hawapatikani, wakatafuta wasiwapate. Wale vijana

Digitized by Google

wakasikitika, kwa maana heshima yake inakwenda kumpotea mamao, wakafanya shauri wakampandisha mamao garini, wakakokota gari kwa kamba mwendo si haba, hatta wakafika kule hekaluni. Watu wakawasifu wakishangilia, mamao akafurahiwa sana watoto wake walivyofanya kazi bora, hatta akamwomba Muungu, waanawe wale wajaliwe kupewa kitu kilicho heri kuliko vyote. Bassi kiisha kufanya siku kuu, vijana wale wakalala wasiamke tena. Ndio waliojaliwa na Muungu." Yule Kroiso akakasirika akamwambia Solon, "Bassi kwa nini kutharauliwa hali yangu mimi? Haifai hatta neno?" Akajibu Solon, "Ee mfalme, fikiri kwanza ginsi yabadilikavyo mambo ya waana Adamu siku kwa siku. Labuda mtu atajaliwa kukaa miaka sabwini, ndio kama siku elfu asharini na tano, na hamsi mia na siku hamsini. Na watu hubadilibadili siku kwa siku katika hali yao. Bassi gissi gani kusema heri huyo na huyo, kabla hajaisha maisha yake?" Yule mfalme asitulie, hatta akamwondoa Solon, akiona shauri lake, ndilo siku zote kungojea mwisho, maneno tu.

Akakaa siku nyingi akajifurahisha moyo kwa milki yake na mali zake pia, hatta mwisho akapatikana na taabu nyingi, akajua Solon ndiye mwenyi shauri jema kweli kweli. Kwani Kuro, Sultani wa Waajjemi, akaondoka akapigana na Waludi akawashinda sana, akateka mji wao mkubwa, ndio Sardis, akamtwaa Kroiso, akamfunga, wakaleta kuni wamchome moto kule kule. Naye Kroiso akafahamu sana maneno ya Solon alivyomwambia sikuzote kungojea mwisho, akamwita jina lake marra mbili kwa uchungu na huzuni, "Ee Solon, Ee Solon." Kuro akasangaa akaamuru afunguliwe kwanza kidogo, akamwuza, kwa nini anamwita Solon. Naye Kroiso akampasha habari za yote yaliompata, na

Digitized by Google

ginsi Solon alivyokataa kumnena yeye mtu aliye heri. Kuro akafikiri mambo ya waana Adamu, kama hubadilibadili siku kwa siku, akaona huruma sana, akamwacha Kroiso, halafu yake akamkaribisha mezani, akamtendea mazuri.

## LUKURGO NA WASIPARTA.

Zamani za kwanza ikawa miji miwili katika Uyonani iliyo mikubwa, ndiyo Siparta na Atene. Na watu wa miji hii mbalimbali kwa tabia na desturi zao; wote wenyi akili, lakini Waatene wakazidi kujifunza na kuyafanya mambo yote mazuri na ya kiungwana, wakipata daraja kwa mambo haya lisilopitika na wangineo, Wasiparta wakajizoezea vita tu bass. Na habari za Wasiparta ndizo hizi.

Wasiparta watu washujaa sana, wakaondoka, wakapiga watu wa inchi wote waliowazunguka. Na inchi ile ndiyo Lakonia katika Uyonani. Walipokwisha kuwapiga, wakawatuma kulima mashamba, wakakaa mjini wenyewe. Na Wasiparta haba, Waheloti, ndio watu wa asili, wengi.

Hatta mtu mmoja alikuwa, jina lake Lukurgo, mwenyi kuupenda sana mji wake na watu wake, akawatengenezea mambo yao yote na desturi zote kwa ginsi wapate kukaa salama wakizungukwa na adui, wenyi hali njema na daraja bora. Akatengeneza hivi. Alifanyiza mji mzima kuwa kama ngome, na watu waliomo kama asikari, jeshi moja na jamaa moja. Hawafanyi biashara, hawasomi illa kidogo tu, hawakai nyumbani, hawasafiri baharini. Huji-

Digitized by Google

weza roho, hushika kadiri na taratibu, hujizoeza miili kazi zote ngumu na za bidii na zifaazo kwa vita, huzaa watoto wazuri na hodari, kukaa pamoja, kula mamoja, hustahimili misiba yote, hupigana hatta kufa, bassi.

Tumehadithiwa kama Lukurgo akageuza mapesa yao yote kuwa vipande vya chuma, vikubwa na vizito, killa kipande rahisi sana. Hatta mtu akitaka kulipa hesabu ya reale miteen, hawezi, angeijaza vile vyuma nyumba pia, akinunua kitu cha thamani angetaka ng'ombe wawili, waichukue mali yake.

Meza za kulia, waanaume huandikiwa meza wazi, killa meza yenyi watu hamstashara ao asharini, chakula mchuzi mweusi na unga na mvinyo na tende na kitoweo bassi. Mtu amechelewa kuja mezani, hukaripiwa; mtu asipokuja, hutiwa athabu. Hatta mkuu wao mmoja alipopiga sana adui, akirudi mjini mwenyi heshima nyingi na kusifiwa sana, akataka siku ile ile tu kwenda kwake kula na mkewe. Wakuu wangine hawakubali, hawampi posho lake la chakula. Naye akafanya hasira, akakataa kazi, wakamlipisha fetha. Wakiingia mezani aliye mzee huuonyesha mlango akisema, "Neno litakalonenwa hapa ndani, lisitoke nje." Mazungumzo mengi walapo, na bishi na mizaha. Hatta ndio sifa ya Wasiparta, kusema maneno haba, lakini merevu.

Siku moja mtu akaja barazani, akiwaomba sana wamsayidie katika vita, akitoa maneno mengi mengi na mazuri. Wakamwambia, "Maneno mengi mno." Akaenda zake yule mtu akaleta mfuko mtupu, hamna kitu ndani, akauweka mbele yao akisema maneno matatu tu, "Mfuko unataka ngano." Wakamwambia, "Nao maneno mengi. Kwa nini kuunena mfuko? Hatuna macho?"

Wasiparta wakapigana na Waatene marra nyingi. Bassi siku moja Mwatene akawacheka Wasiparta

Digitized by Google

kwa sababu panga zao fupi, akisema, "Panga hizo! Ah! fupi mno! Naona zinalika." Akajibiwa, "Zafika hatta tumboni mwa adui zetu kweli kweli."

Alikuwa mtu akamjia Lukurgo akamtolea shauri, ya kuwa haifai Wasiparta watawaliwe na wafalme, heri watu wajitawale wenyewe. Lukurgo akamjibu, "Nenda zako nyumbani, usitawale huko wewe bwana, watoto watawale na kijoli pia. Naona utalia. Na nyumba za wafalme ndio miji yao."

Tena Lukurgo akauzwa siku moja, "Kwa nini Wasiparta humtolea Muungu sadaka ndogo na zizi hizi tu?" Akajibu, "Tusikose kuwa na kitu cha kumtolea siku zote."

Tena mtu akamtakia Lukurgo shauri, "Tufanye nini, adui zetu wasitujie?" Akaitika, "Mwe hali ya masikini, msitamani mali nyingi."

Tena watu wakamwambia, "Mji hauna boma. Tufanyize boma bassi?" Naye akasema, "Watu ndio boma, mawe si boma, wala miti."

Palikuwa na mtu, akatoa shauri jema sana, illa kwa maneno mengi mengi na wakati kusipompasa kuzumgumza sana. Hatta Mfalme wa Wasiparta akamwambia, "Ee rafiki, hakufai kunena yafaayo wakati yasipofaa."

Vile vile na mtu akakaribishwa mezani kwao Wasiparta, naye mgeni, akanyamaa kimya, hakusema hatta neno, watu wakamsangaa. Hatta mkuu mmoja akawaonya hivi, "Ajuaye maneno mazuri, naye ajuaye kwa muda wake."

Siku moja Msiparta akasumbuka na mtu mpumbafu, akiulizwa marra nyingi, "Nani aliye mwema sana katika Siparta?" akajibu, "Asiyefanana na wewe bassi."

Wasiparta wakaupenda sana mji wao, hatta na wakajithania kuwa wamezaliwa kwa hesabu yake tu. Wakienda kwa vita, wakishinda hurudi, wasiposhinda

Digitized by Google

hawarudi, hufa pale pale. Ndivyo walivyofanya simba wale waliopigana katika Thermopuli. Hatta na mwanamke aliyefiwa na watoto wake wawili katika vita, nao Wasiparta wameshindwa, jirani wakamwambia, "Huwalilii?" Akasema, "Siwalilii mimi. Wangalirudi wazima, ningaliwalilia."

## MASULTANI WA WAYONANI.

ZAMANI za kwanza walikuwa masultani katika miji mengi ya Wayonani. Masultani wale wakali sana na wenyi enzi kuu na asikari wengi. Wakawaonea rayia zao, wakawatwalia mali, hatta wakawachinja killa wapendapo. Palikuwa na Sultani mmoja, jina lake Periandro, akawa kwanza mwenyi nia njema. Halafu yake akataka kuweka imara enzi yake, akatuma mjumbe kwa Sultani mwingine, aliye rafiki yake, jina lake Tharasibulo, akamwuliza shauri. Naye hakujibu hatta neno, aondoka tu, atoka yeye na mjumbe yule, wakatembea katika mashamba. Kulikuwako mtama tele umeauka kule mashamba. Wakatembea wale wawili, yule Sultani akamwuliza habari za njiani, naye Sultani mwenyi fimbo akivunja killa suke lililo juu ya wenziwe, akafuliza vivi hivi, anatembea anamwuliza maneno mengi, anayavunjavunja masuke yaliyofika juu sana. Hatta mjumbe akastaajabu, akaenda zake akampasha Sultani wake habari, ya kwamba Sultani yule alitembea shamba, alivunja masuke bassi. Periandro akafahamu, shauri lake halikosi kuwa hili, "Uwachinje walio wakuu, utakuwa imara." Akafanya hivyo.

Digitized by Google

## WAATENE.

Waatene walipokwisha kupiga Waajjemi katika Salamisi wakafanikiwa sana wakapata daraja bora juu ya Wayonani miaka mingi. Wakalipata hivi.

Wayonani waliogopa Waajjemi watarudi halafu vile vile na jeshi kubwa kubwa, watawajia watawapasha taabu nyingi. Wakasema, "Haifai hali hii ya kukaa killa mji peke yake, hauna nguvu, tutaharibika mmoja mmoja. Bassi tupatane sisi kwa sisi." Wayonani wale wengi wamekaa katika visiwa na miji ya pwani. Wakapatana kutengeneza na kuweka tayari vyombo, killa mji kwa kadri ya ukubwa wake na mali zake. Na shauri la vyombo, wakija Waajjemi vyote vitakusanyika marra kwa vita. Waliotengeneza vyombo vyingi ndio Waatene, kwa hesabu ya mji wao kuwa mkubwa na watu wengi.

Wakakaa siku nyingi. Waajjemi hawaji tena. Wayonani wangine wakachoka kuweka tayari vyombo kwa vita, wakataka kukaa raha na kufanya biashara. Vyombo vile uthia tu. Bassi wakaja kwa Waatene, wakisema, "Vyombo vyenu vyatosha. Naswi tusitoe vyombo, tutoe fetha, ndiyo tutakayo, tupate kukaa raha. Nanyi twaeni fetha zile, mzitumie kwa vyombo." Waatene wakawaambia, "Toeni fetha bassi." Akawa mtu mmoja Mwatene, jina lake Aristide, naye mwenyi moyo sawa na wa haki. Akawaamua watu, akawafanyia hesabu ya fetha, killa mji kwa kadri ya ukubwa wake na mali zake. Na hesabu zile sawa sawa barabba, watu wote wakawa rathi. Aristide akapata heshima nyingi ya kazi hiyo, hatta kwitwa jina lake, "Mwenyi haki." Na fetha zile huwekwa mwaka kwa mwaka katika kisiwa

Digitized by Google

kimoja kidogo kilichofanywa wakfu na Wayonani wote, ndicho Delo.

Wakakaa siku nyingi. Waatene wale wakazidi kuwa na nguvu nyingi na vyombo vyingi. Mji usipotoa fetha yake taratibu, huupiga huulipisha ushuru. Hivyo walivyopata kumiliki Wayonani karibu wote waliokaa katika visiwa na miji ya pwani. Mji ukiasi, hupigwa, si yote mamoja, mmoja mmoja tu, ndio werevu wao. Waatene wakasitawi sana, miji mingi ya Wayonani wakiwatumikia, wakitoa ushuru.

Ndizo siku zao Waatene. Wakawa na mali mengi na watumwa wengi. Wakapamba sana mji wao, wakajenga mahekalu mazuri na makubwa kwa mawe ya marmár, wakaweka juu mfano wa muungu wao mmoja,(Waatene huabudu miungu mingi ya uwongo,) wakaufunika thahabu. Na desturi zao ajabu. Killa mtu huwaachia watumwa kazi zote za nyumbani, hujifunga kwa kazi za serkali. Hakuna kathi kwao, killa mtu kathi kwa zamu yake, hukaa barazani huamua wenziwe wakiteta. Ndio kazi walioipenda sana Waatene wote. Hakuna Sultani kwao, killa mtu mzima kama Sultani, hujishughulisha na mambo ya mji na ufalme. Siku kwa siku wote walio wazima hufanya baraza kuu, hukusanyika mahali, hufanya shauri hili na hili, hutoa maneno, tena watu wengi wakitaka hivi ao hivi, bassi jambo limekatika, watu huenda zao.

Na michezo yao mizuri. Hujizoeza sana miili yao killa kazi nzuri na ya kufaa, ndio kuruka, kupiga mbio, kupigana mbavu, kupigana mikono, na zinginezo. Na hii ndiyo iliowapendeza sana. Uko mjini uwanda mkubwa sana wa kuweka watu hatta thenashara elfu, umeviringana, wenyi madaraja mengi ya kukalia yakienda juu kwa juu pande zote. Bassi wakifanya siku kuu, huenda ndani watu wote, hukaa



Digitized by Google

madarajani, hudumu mchana hatta kuchwa wakisikiliza wakitazama watu wakiimbaimba vizuri katikati ya uwanda, wakicheza kwa miguu, wakisumulia hadithi kwa mashairi.

Bassi Waatene wote, wakubwa hatta wadogo, watajiri hatta maskini, wote hodari sana, wote wenyi akili.

Wakapigana na Wasiparta miaka mengi, wakashindwa, ufalme wao ukapunguka.

## SOKRATI.

PALIKUWA na mtu katika Atene, mji mkubwa wa Wayonani, jina lake Sokrati, naye mwalimu mkuu. Desturi yake kutembea huko na huko mjini, kuongea na watu, akiwasikiliza akiwauliza. Ndivyo alivyowafundisha siku zote. Hatta akaona mwenyewe ameaminiwa kazi hiyo na Muungu. Kwa sababu siku moja mwenzake kijana akaondoka akaenda kwa hekalu lililo kuu la Wayonani katika Delfo. Killa mtu atakaye shauri jema ao habari za mambo yatakayompata huenda hekaluni kule, hupewa majibu yake kwa mkohani. Bassi yule kijana akatoa swali, ndio, "Nani aliye na akili kupita walimwengu wote?" Akajibiwa, "Sokrati Mwatene." Akaenda yake akampasha Sokrati habari. Naye akafathaika sana. Hazisadiki habari hizo kuwa kweli, wala hakubali kijana yule ameambiwa uwongo. Kwani Wayonani wote wakaona maneno ya mkohani alioko katika Delfo ndio maneno aliyoyafunuliwa na Mu-

Digitized by Google

ungu. Naye Sokrati mcha Muungu sana. Bassi akaingiwa na mashaka, akasema kwa nafsi yake, "Sina buddi mimi kuyashuhudia maneno haya, Muungu aonekane amesema kweli."

Akaondoka akaenda kuamkia watu waliosifiwa kuwa wenyi akili nyingi, mafundi wa kazi na majemadari na waalimu na watabibu na watunga mashairi na wangineo, akawatafutia habari za kazi zao na elimu yao. Kwanza wakamjibu kwa adabu, halafu yake alipozidi kuwauliza sana wakafanya hasira, wakionekana hawana elimu kweli kweli wala kujua vema hatta kazi zao wenyewe. Sokrati akawaacha, akisema, "Watu hawa hujithania wameih'timu, wasijejua neno. Nami najua, kama sijui neno. Ndiyo nijuayo. Bassi ninazo akili kupita hawa. Maneno ya Muungu kweli." Akaondoka akajiweka pia kwa kazi hii ya kuwafathilia vema watu wa mji wake, ndio kuwafundisha yaliyowapasa na ya haki. Waalimu wangine wakapata fayida ya mafundisho yao, wakitosa waanafunzi fetha. Sokrati hufundisha killa mtu burre, hataki fetha. Naye maskini, hana mali nyingi, huvaa mabovu, huenda kwa miguu, na uso wake mbaya.

Hatta siku moja mtu mgeni akafika Atene, akajivuna kwa kuweza kupambanua watu kwa nyuso, kama wenyi mioyo mema ao mibaya. Waanafunzi wa Sokrati wakamwita wakamwonyesha Sokrati wakasema, "Tazama huyu. Ni mtu mwema ao mbaya?" Yule mtu akamkazia macho akawaambia, "Mzee huyo mbaya na mgomvi pia." Vijana wale wakamcheka sana, wakijua kama Sokrati ndiye mwema na mtulivu. Lakini Sokrati akawachekelea waanafunzi wake, akawaambia, "Amesema kweli mtu huyu. Roho yangu imelekeana na mabaya, nami nimejiweza roho, nikazishinda tamaa zilizo mbaya. Bassi amesema kweli."

Digitized by Google

Naye Sokrati amesema kweli, akisema anajiweza roho yake. Kwa hiyo tena akawa hodari sana na mshujaa. Hatta akaenda kwa vita kuvizia mji, napo penyi baridi nyingi. Ukawa usiku, na pepo za baridi zimetoka milimani, ikanya theluji, wenziwe hawakustahimili, wakaingia vibandani waepukane na baridi, Sokrati akastahimili, akikaa nje usiku kucha, hana viatu, hana illa nguo moja tu, lakini roho yake hodari, hakubali kuiacha kazi yake aliyoiagizwa.

Tena siku moja Waatene wakipigana na adui wameshinda wanakimbia mbio. Yule Sokrati hakimbii, aenda nyuma polepole na taratibu, akitazamia vikali adui zake, nao wakamwacha, hawamfukuzi, hufukuza wale waliopiga mbio. Akaokoka.

Hatta na siku moja Waatene wakafanya baraza kuu, wakataka kuhukumu majemadari waliokosa katika vita, kwa thulumu si kwa haki. Sokrati amekuwa mkuu wa baraza siku ile ile kwa zamu yake. Bassi akawazuia watu, yeye mtu mmoja nao watu wote wa mji wengi wengi, akawakataza wasifanye yasiyo haki. Wakamghathabikia wakubwa hatta wadogo, wakamtukana, wakamfanyia maogofya, wasimshinde. Mwisho wakamwondoa barazani. Ndivyo walivyopata nafasi ya kufanya mabaya. Bassi hodari sana Sokrati, akajiweza roho yake.

Akafuliza siku zote kazi yake ya kuongoa watu kwa haki. Hatta wengi wakasumbuka sana, wakafanya shauri wamue. Wakamshtaki maneno mawili, la kwanza, hawaamini miungu Waatene wote wanaowaamini, la pili, huwapoteza vijana tabia zao. Bassi kwa neno la kwanza, hana hatiya mwenyewe, hakosi killa siku kusali na kutoa thabihu kwa wazi, yu mcha Muungu sana, lakini kwa akili si kwa ujinga. Hatta watu hawangalimstaki hivi, illa kwa maana alisema marra nyingi ana sauti ndani yake, imwo-

Digitized by Google

ngoayo kwa mema imzuiayo kwa mabaya, akaiona sauti ile ndiyo sauti ya Muungu akaiangalia sana. Kwa neno la pili, hakupoteza vijana hatta kidogo, akiwafunza mema tu, lakini kwa akili. Bassi vijana wale walioongoka wakaacha desturi na nia zisizo kwa akili, baba zao wasioongoka wakazishika kwa ujinga wao. Ndiyo iliyowachukiza watu wengi, wakamchukia Sokrati.

Sokrati akahukumiwa kufa, mtu asiyetenda illa mema tu, akafungwa gerezani akanyweshwa sumu akafa. Naye hakuogopa kufa, akafa kikondoo akisema, "Sikatai mimi kufa. Kukiwa kutoa kuwa tu, siko hasara. Kukiwa kwenda peponi kwao waliotangulia kufa, ndiko fayida." Hajasikia habari ya kiyama ya wafu, Isa Masiya hajaja, bado miaka aroba mia. Kama angalisikia, angalifurahi.

## ISKANDER.

Siku zile ulipopunguka ufalme wa Waatene, palikuwa na mfalme wa Wamakedoni, jina lake Filipo, nao Wayonani pia wakikaa inchi upande wa kaskazini. Akaenda akawapiga Wayonani wangine akafanikiwa sana, akawa mfalme mkuu. Hatta akazaa mtoto mmoja mume, jina lake mtoto Iskander, na mtoto yule akawa na moyo mkubwa na mashauri makubwa ajabu tokea utoto wake. Hakubali kitu cho chote kilicho kinyonge, hutaka yaliyo bora na makuu tu. Hatta siku moja watoto wenziwe wakamwita ashindane na watu kwa kupiga mbio.

Digitized by Google

Akawaitika, "Watu gani bassi? Sitaki mimi kushindana illa na wafalme tu." Tena baba yake akiwa anateka miji mengi na kupiga adui zake sana, Iskander akaletewa habari zake akafanya huzuni akasema, "Baba yangu akishindashinda siku zote, hatatuachia sisi nafasi katika ulimwengu ya kutendea makuu na yenyi ajabu."

Akawa mtoto bado, mtu akampelekea babaye frasi mzuri, akataka kuuza kwa reale elfu kumi. Na frasi yule mzuri sana, mkali lakini, hajafugika, hatta mtu hawezi kumpanda wala kumtiisha hatta kidogo, alivyo mkaidi pia. Mfalme akaghathabika, akaamuru aondolewe. Iskander akawako akamwambia babaye, "Wamtiisheje watu woga na wajinga?" Mfalme akamwambia, "Ee mwanangu, gissi gani kutukana watu, usipoweza kumpanda mwenyewe?" Yule mtoto akajibu, "Naweza mimi." Akamwambia, "kapande bassi." Na yule mtoto ameangalia frasi anastushwa na kivuli chake yeye, akampindua uso kwa jua, akamtuliza kwa sauti na kumpapasa. Halafu yake akampanda akamkimbiza mbio sana, hatta amekwisha kumfuga pia, ndipo mfalme akatambua, mtoto gani aliyemzaa. Wakakaa siku, baba yake akafa, Iskander akawa mfalme, amepata miaka asharini tu kwa umri wake.

Akaondoka akawatuliza Wayonani kwanza. Alipokwisha, akafanya jeshi kubwa, nalo limezoea kazi zote za vita zamani ya babaye, Filipo. Akavuka kwa Asia penyi Dardanels (napo palepale alipovuka Serkisi kwa Europa), akawapiga Waajjemi katika mto Graniko, unakwitwa sasa Kodsha-su, akaipata Anatolia (Asia Minor) yote. Sultani wa Waajjemi, jina lake naye Dario, akakusanya watu wengi, wakapigana marra ya pili penyi Isso katika Kilikia, Dario akashindwa, mkewe akakamatwa na binti zake wawili, kwa shidda akapona mwenyewe. Iskander

Digitized by Google

akapata inchi yote ya Sham, akafanya vita ya miezi saba kwa mji mkubwa Turo akautwaa. Kiisha akatiisha Wamisri, akaandika misingi ya mji katika pwani, ndio Iskanderia hatta kwa leo. Kiisha akaenda mtafuta Dario aliko. Akamwona penyi Arbil, mji wa Sham, na jeshi kubwa sana naye. Majemadari ya Iskander wakafanya shauri la kumgundua Dario usiku. Iskander hakukubali akasema, "Simpigi mimi illa kwa wazi." Dario akaogopa, akataka kupatana naye, akimtolea fetha nyingi na sehemu kubwa ya milki yake na binti yake pia. Hatta jemadari mmoja Myonani akamwambia Iskander, "Nikiwa Iskander mimi, Ningekubali," Iskander akamjibu, "Hatta nami ningekubali, nikiwa wewe." Bassi hakupatana naye, akawaangukia Waajjemi kwa ghâfala, akawashinda sana ndio marra ya tatu, akatwaa miji yote ya Sultani Dario; na mji ule mkubwa Babel, na hasina zake na mali zake zote. Dario akakimbia, halafu yake akafa.

Na Iskander yule bado kuwa rathi. Akaendea tena, akapiga watu wa Asia mpaka Hindi, akamiliki inchi yote toka Uyonani mpaka Hindi, ndio milki yake. Akajenga miji akafanyiza bandari, akatengeneza njia, akawajulisha watu wote lugha ya Wayonani na elimu na mathehebu zao za kiungwana, akakalisha Wayonani wangine katika miji ya Asia kwa mashariki, na habari za Asia zikazidi kutambulika na kuenea katika Europa. Na kazi hizo zote akazifanya kwa muda wa miaka thenashara tu bassi, akarudi kwa Babel, akakaa huko siku, akapatikana na homa, akafa kuko huko katika Babel, akiwa amepata miaka thelathini na miwili. Milki yake ikagawanyika sehemu 'nne, wakamiliki majemadari yake wa'nne, killa jemadari sehemu moja. Wakakaa siku nyingi. Baadaye Warumi wakawapiga Wayonani, wakaweza sana katika ulimwengu.

Digitized by Google

Na Iskander huyo ndiye aliyefananishwa na chui na mbuzi mume katika kitabu cha nabii Daniele, kwa maana ya kuwarukia adui zake kwa gháfala na kuwapiga thoruba moja na kuwaharibu wote.

## VISA VYA ISKANDER.

PALIKUWA na mtu Myonani, naye mwalimu mkubwa, jina lake Diogenesi, akakaa katika pipa, ndilo nyumba yake, huvaa nguo mbovumbovu, hula mtama tu, hujipasha uthia siku zote. Ndizo desturi zake. Wayonani wakamheshimu sana. Hatta Iskander akaja kumwamkia, akataka mwenyewe kusifiwa naye kama na watu wangineo. Akamwambia, "Salaam. Mimi ndimi Iskander." Akamwambia, "Salaam. Mimi ndimi Diogenesi." Akamwambia, "Baada ya salaam, nataka sana kukufanyia fathili." Mwalimu akamjibu, "Similla jua bassi. Unanitia giza." Mfalme yule akasangaa, akawaambia wenziwe, "Nisipokuwa Iskander, ningependa kuwa, Diogenesi," kwa ginsi ulivyompendeza upweke wake.

---

Ulikuwa mji wa Asia, uliokwitwa Gordio. Na katika mji ule likawa gari lenyi mti wake umefungwa na kamba fundo la ajabu sana, ginsi lilivyopigwa fundo lile la kamba. Haliwezikani kufunduliwa kabisa, likahadithiwa ya kuwa, "Alifunduaye fundo hili, ndiye atakayemiliki dunia pia." Watu wengi wakajaribu kulifundua, wasiweze. Hatta

Digitized by Google

Iskander akafika kwa mji ule katika kwenda kupiga Waajjemi, akalikata fundo kwa upanga wake. Ndivyo alivyolifundua.

---

Akawa Iskander anafukuza adui zake katika jangwa pasipo maji, wakaona kiu sana na yeye na asikari wake, hatta wangine wakazimia, wote wakafathaika. Wakatafutatafuta maji, wasiyapate illa kidogo tu nayo kwa mbali. Likawa jua kitwani wakamwona Iskander anateswa na kiu, wakamletea maji katika ngao. Akawauliza, "Nani ninyi mnaoniletea maji?" Wakasema, "Watoto wako sisi tunaokufa. Haithuru, uyanywe bassi. Wangine watazaliwa, nawe wa pekee." Akaishika ngao, akawaona asikari wake wanamkazia macho wakitaka sana maji, akawarudishia maji, akisema, "Nikinywa mimi, hawa watazimia roho." Wale asikari wakasemana, "Twende zetu, hatuoni njaa wala kiu, tukiwa na bwana huyo." Wakampenda sana, wakaendelea mbio.

---

Iskander akawa jemadari mkuu kweli kweli, illa hakujiweza roho yake akafanya mabaya mengi, kama haya. Akakamata mtu mmoja, aliyepigana naye kwa ushujaa sana, naye jemadari, akamfunga mzima kwa gari lake nyuma, akakimbiza frasi, yule akakokotwa chini akafa. Akatwaa kwa hila majemadari wake mwenyewe, watu wawili, baba na mtoto wake, kwa sababu aliwathania tu wamefanya shauri juu yake, hakujua vema. Akawasumbua sana akawachinja. Siku moja akalewa katika karamu, akachinja pale mtu mmoja, aliye rafiki yake sana.

Bassi aliweza sana katika ufalme wake, hakujiweza vema mwenyewe.

Digitized by Google

## WARUMI.

SIKU za Bwana wetu Isa Masiya alizokuwapo hapa duniani, Warumi walimiliki inchi zote zilizoizunguka bahari Mediterraneo, toka Uingereza mpaka Misri, toka mlango wa Gibraltar mpaka bahari Kaspiani. Na mataifa yote yaliokaa katika inchi hizo yalikuwa siku zile yakikaa raha na amani.

Habari za Warumi, ginsi walivyotiisha mataifa hayo mengi, wakayatuliza kwa raha na mustarehe, ndizo hizi. Zamani za kale, imepata kama miaka mia saba na miaka hamsini mbele ya kuzaliwa kwake Isa Masiya, ukawa mji katika Italia, ndio Rumi, mji si mkubwa siku za kwanza, umejengwa juu ya vilima saba kando la mto Tiberi.

Warumi wenyewe wameihadithia asili ya mji wao hivi.

---

### HADITHI YA ROMULO NA REMO.

Palikuwa na mtu, jina lake Amulio, naye mbaya sana. Akaondoka akamtwalia ndugu yake mkubwa milki yake akamiliki mwenyewe. Na watoto wa nduguye akawachinja. Akabaki binti ya nduguye tu, naye amezaa watoto wawili waume nao pacha. Bassi Amulio akaamuru watoto wale watupwe mtoni. Wakawatupa mtoni, ndio Tiberi. Maji yakawachukua, wakawasili hatta mahali, wakakwama topeni. Mbwa wa mwitu akawakuta kule ukingoni mwa mto, akawapeleka tunduni kwake akawanyonyesha. Hatta siku moja mchunga kondoo akipita akisikia watoto wanalia akaona ajabu, wamo watoto wachanga wazima katika tundu la nyama ya mwitu. Akawaleta kwake akawalisha siku nyingi. Wakakua

Digitized by Google

wakawa vijana hodari sana, wakajulikana na yule babuo, wakamua Amulio, wakamrudisha babuo katika ufalme wake. Na vijana wale, majina yao Romulo na Remo. Wakafanya shauri la kujenga mji kando la Tiberi pale pale walipotolewa topeni na maji. Wakapiga misingi wakajenga. Fitina ikawapata kwa ajili ya nani amilikiye mji huo. Hatta Remo akamfanyia ndugu yake thihaki, akiruka juu ya kuta anazozijenga: nazo fupi, bado kujengwa juu. Romulo akaingiwa uchungu, akamwua pale pale kwa jembe lake, akawa mkuu wa kwanza wa Rumi. Hiyo ndiyo waliyohadithi Warumi.

---

Warumi wakalima mashamba, wakafanya biashara, wakafanikiwa. Na desturi zao za kwanza ndizo hizi. Mambo ya nyumbani, killa mwenyi nyumba hutawala nyumba yake. Na mambo ya mji wote, killa mwenyi nyumba huitwa barazani, hufanya shauri na mfalme, ndiye mkuu wa baraza. Wakakaa siku nyingi. Watu wengi wakaangalia mji ule unakua vema unafanikiwa, wakaja wakakaa humo, wakasayidia katika vita, wasiitwe barazani. Watu hao wageni wakaitwa Waplebi, na watu wa asili Wapatri. Rumi ukawa mkuu wa miji ya Walatini, ndio kabila lao Warumi wa kwanza. Halafu yake Warumi wakawaondosha wafalme wao, na mahali pa wafalme wakachagua killa mwaka watu wawili kuwa majemadari katika vita na maliwali wa mji, wakawaita makonsuli.

Warumi wakashindana sana na watu waliowazunguka, kwanza Waekwi na Wavoleshi na Waturuski, tena Wasaminiti, tena Wayonani waliokaa katika Italia upande wa kusini. Wakashindana nao hatta wakaisha kuwashinda. Na kazi ya kuwashinda watu hao wote, kazi ya miaka kama hamsi mia.

Digitized by Google

Bassi ndio ajabu kuu ya Warumi, walivyojifunga kwa kazi hiyo ya kushinda wote, mwaka kwa mwaka, kizazi kwa kizazi, wasilegee. Ajabu na hii pia. Warumi hodari sana, na wenyi akili nyingi katika vita. Kwa nini hawakushinda adui upesi, si polepole tu? Tazama maana yake.

Kulikuwa na fitina siku zote katika watu wa Rumi. Wale wa kwanza, wale wenyi kwitwa barazani na kutengeneza mambo ya serkali, ndio Wapatri, hawakukubali wageni, ndio Waplebi, washariki nao katika mamlaka yao. Na Wapatri si wengi lakini wakubwa na wenyi mali, na Waplebi wengi na wafaao sana kwa vita, hawana mali nyingi. Wakatetana miaka mengi, wasipigane lakini wao kwa wao. Mwisho Waplebi wakashinda wakajipatia daraja bora na mamlaka kwa kadiri yao katika mji.

Na fitina hiyo ndiyo iliyowapinga Warumi wasishinde adui upesi, ndiyo iliyowazoeza kujiweza roho zao na kutendana haki, ikawawezesha kudumu hatta wakashinda adui mwisho.

Bassi tazama halithi ya fitina ya ndani na za vita za nje, zilizowapata Warumi katika muda wa miaka hamsi mia.

## MJI NA MWILI.

HAPO kale watu wa Rumi walionewa sana na wakubwa wao. Hatta siku moja wakaondoka wakatoka mjini wakaenda zao kwa kilima wakakaa huko. Hawakupenda kupigana na wakubwa, wala kuwaua, wala kuwafanyia jeuri. Waliwaacha tu. Wakubwa wakauona mji hapana watu, na adui wengi waliozunguka Rumi, wakaogopa wakinena, "Mambo haya

Digitized by Google

hayafai. Pasipo watu, hatuponi naswi." Wakatuma wajumbe kwenda kutuliza watu na kuwapatanisha, nao hawakubali. Wakatuma wangine vile vile, hawakubali.

Bassi mwisho mkubwa mmoja, jina lake Menenio Ageripa, akaenda pale walipo watu akawaita barazani akatoa maneno haya, " Enyi watu, sikilizeni." Siku za zamani kulikuwa na fitina katika mwili, vipande vyake vyote wakimteta tumbo, wakimwambia, " Ewe mvivu, gissi gani mambo haya? Sisi kutumwa hivi na hivi, hivi na hivi, siku zote, wee kukaa, kupata fayida, kushiba, bassi?" Naye tumbo hakusema hatta neno. Bassi wale wakanyung'unika, wakafanya hasira wakasema killa mtu, " Sitaki bwana huyo, sitaki kazi. Haya, twende zetu." Wakakoma, wasifanye kazi kabisa. Miguu hawaendi mezani, mikono hawasogezi chakula, masikio hawasikii kengele, macho hawatazami sahani, kanwa hajifumbui, meno hawatafuni. Hatta tumbo mwenyewe akaona njaa. Halafu yake nao wote hawawezi. Hawana nguvu wala miguu kwa kutembea, wala mikono kwa kushika, wala masikio kwa kusikia, wala macho kwa kuona, wala kanwa kwa kujifumbua, wala meno kwa kutafuna. Tumbo akawaambia, " Enyi wavivu, sitendi kazi mimi? Kukaa, kuwaagizia kazi zenu, kushiba mwenyewe, ndio kazi yanyu kweli. Na fayida kwenu je? Tazama, mimi ninayewawezesha kwa vitu vyote. Kwa maana yanyu ninyi hupata kulishwa, kujipendeza, kakaa raha, kuwa na uzima na hali njema pia. Bassi, kazi yenu ndio fayida yenu. Nami, si mvivu mimi." Watu wa Rumi wakasikia kama kweli haifai fitina katika mji, wakafanya shauri na wakubwa, wakajaliwa njia ya kujilindia wenyewe wasionewe sana na wakubwa. Ndivyo walivyopatana, wakarudi mjini, wakakaa.

Digitized by Google

## KORIOLANO.

Palikuwa na mtu Mrumi, naye mshujaa sana. Warumi wakapigana na adui zao, watu wa Korioli, ndio mji wao, wakawafukuza hatta wakaingia katika mlango wa mji. Mtu yule akaingia pamoja nao peke yake, mlango ukafungwa nyuma yake. Akawa mshujaa sana, akapigapiga Wakorioli, akawafungulia wenziwe mlango wa mji, wakautwaa mji. Yule mshujaa akaitwa Koriolano kwa sababu ya tendo lile kuu.

Ikawa njaa katika Rumi. Wapatri wana chakula, Waplebi hawanacho. Naye Koriolano Mpatri, akasema, "Waplebi wasipotii Wapatri, hawali." Waplebi wakamkasirikia sana. Hatta akaogopa akakimbia kwa adui wale wale aliowapiga kwanza. Wakamkaribisha furaha, akawa jemadari wao. Akaondoka kwenda pigana na Warumi. Warumi wakafanya hofu, wakatuma wajumbe walio wakubwa na rafiki yake Koriolano waende kupatana naye. Hakukubali. Wakatuma wakohani wenyi sanamu za miungu yao. Hakukubali. Mwisho wakatuma mama yake na mkewe na watoto wake. Wakamlaki wenyi nyuso za huzuni na nguo mbovu mbovu, wakampigia magote. Koriolano akawakaribisha vizuri akataka kumbusu mamaye. Yeye akakataa, akamwuliza, "Wewe adui ao mtoto wangu mimi?" Akamwambia, "Ee mama, ndiwe umenishinda." Akaenda zake, asipigane na Warumi.

Bassi tazama Warumi ginsi gani walivyothoofika kwa maana ya fitina zao, na watoto walivyoheshimu mamao sana.

Digitized by Google

## KINKINATO.

Ilikuwa vita ya Warumi na Waekwi. Jeshi moja la Warumi likatoka likienda kupigana na Waekwi. Wakafika hatta kwa mahali palipozungukwa na milima na mlango wake mwembamba sana. Waekwi wakawavizia wakiingia humo wakaja mbio wakaulinda mlango ule, wasiweze kutoka tena. Jeshi lote zima limefungwa ndani. Watu wa mji wakaletewa habari, wakafathaika sana, wakafanya shauri, wakasema, "Tumwite Kinkinato. Ndiye jemadari mkuu." Wakaenda kumtafuta. Naye akawako koondeni, amepiga uwinda, analima katika koonde lake. Akiona wajumbe wanakuja mjini, akavaa nguo kwa heshima yao. Wakamwambia, "Umekwitwa kuwa jemadari mkuu." Akawaambia, "Haya." Akaenda mjini, akakusanya jeshi, akaamuru killa mtu atwae chakula na miti kumi na miwili. Wakatoka wakafika kule kwenyi milima usiku. Nao Waekwi wako wanaulinda mlango wa boonde vile vile. Bassi Warumi wakawazunguka Waekwi kwa hila katika giza, wakafanyiza ua wa miti pande zao zote. Ilipofika assubui, wakaonekana Warumi kwa ndani, Warumi kwa nje, na Waekwi nao kati kati. Marra Waekwi wakajitolea. Kinkinato akarudi kwa Rumi kwa shangwi na majeshi mawili ya Warumi mazima. Badaye akaenda zake koondeni akalima vile vile.

Bassi tazama Warumi walivyo hodari. Hatta mtu leo mwenyi shamba tu, kesho mkuu wa Rumi na apigaye adui kwa akili akipata sifa nyingi, marra hugeuka kulima tena, kama maskini.

Digitized by Google

## WAGALLO NA MABATA.

PALIKUWA na watu, wakikaa upande wa kaskazini wa Italia, waliokwitwa Wagallo. Wakafanya jeshi kubwa, wakaenda kupigana na Warumi, wakafika karibu na Rumi penyi mto Alia, wakawapiga Warumi sana. Warumi wengi wakakimbilia mbali, wangine si wengi wakaingia katika ngome ya mji, wakailinda. Walikuwako tena mjini wazee wenyi mvi, nao wakiona haya kuuacha mji, wakavaa mavazi mazuri, wakakaa kitako barazani killa mtu katika kiti chake, wakangoja. Hatta Wagallo wakaja kwa tadi, wakakuta wazee wale wanakaa kimya wasifathaike hatta kidogo, wakasangaa. Mmoja wao akapapasa mzee ndevu zake, mzee akampiga fimbo kitwani. Wagallo wakawarukia, wakawachinja wote thóruba moja. Kiisha wakauteketeza mji, wakajaribu kuitwaa ngome, wasiweze.

Na ngome ile imejengwa juu ya kilima kisichopandika na mtu, ginsi kilivyosimama sana, pande zote zaenda juu sawasawa. Ikaitwa Kapitoli ile ngome. Bassi Wagallo wakakaa siku nyingi wasiweze kuitwaa. Hatta mtu mmoja akatafuta njia, akaita wenziwe, wakapanda kwa shidda sana usiku, na Warumi wamelala usingizi wote. Wakawa katika ngome mabata. Bassi marra Wagallo walipokuwa wakifika juu, mabata wale wakalia sana, Mrumi mmoja akaam'ka, akatwaa ngao yake akamsukuma Mgallo aliyetangulia, akamtupia chini. Warumi wangine wakaja mbio, wakawafukuza kabisa.

Walipokwisha kuuteka mji, Wagallo wakaondoka wakaenda zao kwa inchi zao. Warumi wakarudi, wakajenga tena pale pale.

Digitized by Google

## PURRO MYONANI.

WALIPOKWISHA Warumi kuwapiga Wasaminiti, Wayonani waliokaa katika miji mingi ya Italia upande wa kusini wakaogopa, wakamwomba Purro, aliye mfalme wa Epiro katika Uyonani, aje awasayidie. Akaja, na watu wengi naye na frasi na tembo pia. Akapigana na Warumi, akawashinda, lakini kwa shidda nyingi sana, watu wake wengi wengi waliouawa siku ile. Hatta Purro akasema, "Nikishinda hivi marra mbili tatu, nimeshindwa," kwa sababu ya watu kuwa wengi waliompotea. Akatuma mtu mwenyi akili kwenda kupatana na Warumi. Nao kwanza wakapenda, halafu yake wakakataa, isipokuwa Purro atatoka kwanza katika Italia. Yule mtu akarudi kwa Purro akampasha habari ya baraza ya wazee katika Rumi, akasema, "Haifai kushindana na Warumi. Wazee wale wote sawasawa, wote wafalme." Purro hakumwangalia akapigana na Warumi akawapiga marra ya pili, asiwatiishe hatta kidogo. Akaenda zake kushinda miaka miwili, akapigana marra ya tatu, akapigwa sana. Akarudi kwake.

Warumi wakamiliki Italia yote kwa kusini.

## TABIA YA WARUMI.

WARUMI waliupenda mji wao kuliko nafsi zao wenyewe. Hatta akawa mtu, jina lake Dekio, naye konsuli mwaka mmoja. Warumi wakakipigana na adui zao, wasiwaweze kwanza. Na yule Dekio ame-

sikia habari, kama watu, jemadari wao atajitoa afe, ndio watakaoshinda. Marra akajifunika kitwa, akaruka kati ya adui akauawa. Warumi wakashinda adui zao siku ile.

Na Warumi wagumu sana. Wakapigana siku moja na adui, konsuli jina lake Manlio akatoa amri, mtu ye yote asipigane na adui peke yake. Wakakaa. Halafu adui akatokea akamwita mtoto wake yule konsuli, akamwambia, "Tupigane sisi." Akaitika, "Haya tu." Wakapigana. Mrumi akampiga adui akatwaa mateka yake akarudi. Babaye akasikia habari ya kuwa amepigana peke yake, nayo marufuku, akaamuru aletwe kwake akamhukumu kukatiwa kitwa, sababu aliasi. Akakatiwa kitwa akafa kuko huko mbele ya baba yake. Watu wote wakaingiwa na machukio, wakaona amefanya vema lakini yule konsuli.

Warumi wa kwanza hawana choyo. Hatta siku moja Wasaminiti wakitaka kujipendekeza kwa jemadari mkuu wa Warumi, wakampelekea zawadi, thahabu nyingi. Wajumbe wakamkuta anashinda shambani, anapika boga mwenyewe ndio chakula chake, na nyumba haina pambo. Wakamtolea zawadi ile, asiipokee. Akawaambia, "Heri kuwa huna mali, na kuwaweza walio nazo." Wakaondoka.

## NJIA NA MAKOLONIA.

Kwa desturi za vita, Warumi mbali na watu wangineo mbali. Watu wangine wafanyapo vita, hupiga adui, huteka miji, huteketeza nyumba, huchukua

Digitized by Google

ng'ombe na vyombo na vyakula, labuda hukaa kidogo, hurudi kwao, bassi. Warumi hawaachi inchi yo yote waliyoipata, huimiliki dayima; huwapiga sana adui kwanza, tena huwatuliza, huwazoeza desturi na tabia zao Warumi. Wakawatuliza hivi. Huweka asikari Warumi katika miji huko na huko ya killa inchi waliyoipata. Warumi hao, hutiisha watu waliopo, hulima mashamba, huongoa watu kutambua nia za Warumi na nguvu zao, kama kuasi hakufai, kutii kwafaa. Na miji hiyo ya asikari, ndiyo iliyoitwa makolonia.

Tena Warumi hufanyiza njia kuu na nzuri killa wamilikipo. Hatta na njia hizo ajabu sana. Zatokea Rumi, zafika hatta mipakani kwa milki yao, zimenyoka kabisa, zaenda sawasawa milimani boondeni mashambani mitoni, hazipotoki, zimetengenezwa na mawe na chokaa tele, upana wao wa kupisha gari la frasi. Hatta zingine zakaa mpaka leo, zimepata miaka elfeen, zinatumika vile vile siku hizi katika Uingereza na kwenyi inchi zilizo mbali sana na Rumi. Na maana yao, majeshi ya Warumi wapate kupita pote upesi, tena Warumi kuletewa upesi habari za milki yao yote.

Hatta na fumbo hili limejulika, kama "Warumi walitiisha ulimwengu kwa majembe,"—kwa sababu ya njia hizo na tena, killa Mrumi akienda kwa vita huchukua miti na jembe, na killa watuapo usiku majeshi ya Warumi katika vita zao, hufanyiza boma la udongo na miti lisilotwalika na adui, hulala raha na salamu. Ndizo kazi za majembe yao.

Digitized by Google

## WAKARTAGINI.

MARRA walipokwisha kuwatiisha watu wote wa Italia, Warumi wakafanya vita na watu wa mji mkuu, ulioko pwani ya kaskazini ya Afrika, ndio Kartago. Wakartagini wakaweza sana baharini. Bassi wakafanyiza vyombo vyingi, wakapigana nao miaka mia. Mwisho wakawashinda, wakamiliki inchi ya Kartago, na Sikilia na Hispanya pia, wakawa wakuu wa bahari yote Mediterraneo.

## REGULO.

WARUMI wakawa wanapigana na Wakartagini. Na Wakartagini wakatumia tembo wengi katika vita, Warumi wakaogopa, wakashindwa sana kwanza. Hatta na jemadari mkuu wa Warumi, jina lake Regulo, akatwaliwa akafungwa akachukuliwa kwao. Akashinda huko gerezani amefungwa miaka miwili. Bassi siku moja Wakartagini wakapigwa, wengi wakatwaliwa wazima na Warumi. Wakafanya shauri, wakataka kupatana nao Warumi na kuwabadili wafungwa. Wakatuma wajumbe kwa Rumi na Regulo pia, kwa maana mtu huyo mwenyi sifa nyingi na daraja bora kwao, wakamwapisha kwanza, atarudi kwa Kartago gerezani, wasipopata wajumbe kupatana na Warumi.

Bassi Regulo akafika kwake Rumi, akasimama mlangoni nje ya boma, akisema, "Mimi nimetoka

Digitized by Google

kuwa Mrumi, mimi mtumwa wa washenzi, wakuu wa Rumi kukaribisha wageni ndani ya boma ndio haramu. Bassi nimekaa hapa." Hatta mkewe na watoto wake wakamtokea, wala hakufurahiwa moyo nao, akawaambia, "Mimi mtumwa, si mtu mimi, kitu tu." Halafu yake na wazee wakaja, wakafanya baraza huko nje, wakamwambia, "Karibu, kakae mahali pako, mkuu wa Rumi na wewe." Asikubali, akasema, "Enyi wazee, mimi mtumwa wa Wakartagini, nimetumika nao kwenda kupatana nanyi." Kiisha kusema haya, akataka kwenda zake. Nao wakamzuia, hatta na wajumbe wa Wakartagini wakamsimamisha hapo tena. Hana buddi kukaa. Akatoa maneno haya, "Enyi Warumi, msipatane na Wakartagini hatta kidogo, msiache kupigana nao, msibadili wafungwa. Na mimi pia, nikitolewa kurudi kwao, haithuru." Mtu mmoja aliye mkohani akaondoka akamwambia shauri, "kwani kurudi huko? Hawakuapisha kwa nguvu? thulumu hiyo, siyo haki. Uapo ule haufai neno." Naye Regulo akajibu, "Nimeapa, bassi. Si mwongo mimi, mtumwa mimi lakini Mrumi bado. Najua nitateswa sana hatta kufa. Haithuru." Wazee wa Rumi wakasikitika, hawana buddi kulifuata shauri lake. Wakamsindikiza njiani, na mkewe na watoto wakitoka machozi wakimwomba akae, wasimweze. Akarejea Kartagoni na wajumbe. Wakartagini wakafanya uchungu mwingi, wakamkaza ndani ya pipa lenyi misomari mingi, mikali na mirefu, pande zote kwa ndani, wakalifingirisha, akapata maumivu machungu, akafa.

Digitized by Google

## HANIBALI.

Siku zile Warumi walipopigana na Wakartagini, palikuwa na mtu, jina lake Hanibali, Mkartagini. Akiwa mtoto bado, amepata miaka tissia, babaye akamwambia, "Wataka kwenda kwa vita nami?" Na baba yule jemadari mkuu wa Wakartagini. Akamwambia, "Nataka." Akamwambia, "Uniapie bassi, hukosi siku zote kuwa adui yao Warumi." Akamwapia, akaenda kwa vita, babaye akatiisha inchi ya Hispanya, babaye akafa.

Hanibali hakusahau alivyoapa, akafanya jeshi, akapiga mji mmoja katika Hispanya, uliokwitwa Sagunto. Na mji ule umetegemea Warumi. Bassi Warumi wakapeleka wajumbe kwa Kartago, wamtete Hanibali. Wajumbe wakafika Kartago, wakaleta mastaka, wasithubutishe. Mmoja wao akakunja joho lake, akasema, "Zimo humo vita na raha. Mwataka ipi?" Wakamwambia, "Upendavyo mwenyewe." Akalikunjua joho, akisema, "Natoa vita." Wakamwambia, "Haya."

Yule Hanibali marra akafunga safari ya kuendea Italia. Akatwaa asikari wengi akaondoka katika Hispanya, akapita milima mikubwa, ndio Purenisi, akaingia Ufransa, akavuka mto mkubwa, ndio Rone, akapanda milima mirefu na mikubwa sana, ndio Alpi, kwa taabu nyingi na hatari nyingi na misiba mingi. Hatta nussu ya jeshi lake lote likapotea milimani, kwa baridi na kwa njaa na kwa adui, na kwa kwenda penyi theluji na maji yalioganda kwa baridi nyingi na maboromoka makubwa pasipo njia ya kutelemka salamu.

Naye hazimi nafsi yake, halegei, akawa hodari sana. Akawapiga Warumi marra tatu moja kwa

Digitized by Google

moja, akafika hatta karibu na Rumi, asiwatiishe hatta kidogo kidogo. Hujitumainia sana Warumi, wakiona kama, "Sisi hufa, mji haufi." Tena watu wa Hanibali wakipunguka sana kwa mapigano, Warumi wakiwa na miji mingi ya Italia ilivowasayidia. Hatta mahali palepale alipotua Hanibali na jeshi lake karibu na Rumi, mwenyi shamba lile akaliuza sokoni kwa mnada akapata fetha nyingi.

Hanibali akawa mshujaa kwelikweli, asiweze kuwatiisha Warumi. Wakartagini wakaona uwivu na ugomvi, hawakumsayidia vema. Mwisho hana buddi kuiacha Italia, kurudi kwake. Warumi wakapiga Wakartagini wakauharibu kabisa mji wao.

## KAISARI.

WARUMI wakashindana na adui miaka mia tena, baada ya kwisha kuwapiga Wakartagini, wakatiisha Wayonani na Washami na Wamisri na watu waliokaa zamani katika Ufransa, ndio Wagallo, na katika Uingereza, ndio Wabritoni,—watu walioizunguka bahari Mediterraneo ndio milki ya Warumi. Wakapata mali nyingi nyingi, wakajifunza elimu ya Wayonani na desturi za kiungwana, wakafanikiwa sana. Mioyo yao ikageuka, na desturi zao za kale zikageuka. Maskini wengi mjini, nao hawaangalii mambo ya mji, mambo yao wenyewe tu, kushiba na kukaa raha bassi. Baraza ya wazee, ndio yenyi nguvu na mamlaka, nao wenyi choyo sana, wakawaonea watu wa zile inchi walizozitiisha, wakawalipisha fetha nyingi kwa thulumu tu. Hatta wakubwa wao

Digitized by Google

wakashindana sana, wakafanviana vita marra nyingi wao kwa wao. Rumi ikafathaika sana kwa fitina.

Halafu mtu mmoja akaondoka, naye hodari kupitilia mbali wenziwe wote, jina lake Julio Kaisari. Akawa mfalme mkubwa sana. Hatta wenziwe na rafiki wakaingiwa uwivu wakamchinja, akafa.

Baada yake yeye mfalme mwingine akapata milki yake, ndiye Augusto Kaisari. Alipokwisha kuwatuliza Warumi, akawasuluhisha watu wote wa ufalme wake, akatengeneza vizuri mambo yote ya ufalme, huwatendea vema na kwa haki, huweka maliwali katika inchi zote, hufanya hukumu sawa kwa watu na kwa maliwali pia, watu wote watoto wake, si Warumi tu. Ulimwengu wote ukifurahi, ukikaa raha na amani, inchi zote toka Uingereza mpaka Misri na toka mlango wa Gibraltar mpaka bahari Kaspiani. Ulimwengu ukaitii Rumi, ukaiheshimu.

Ndipo alipozaliwa Bwana wetu Isa Masiya, ndipo ilipoanza milki yake isiyo na mwisho, ufalme wa mbinguni.

## PETRO MTUME.

WAKATI wa zamani Wamasihiya walifukuzwa sana na wafalme wa Rumi, walioitwa makaisari, kwa ajili ya imani ya kimasihiya. Hatta na tumehadithiwa kama Petro yule mtume mtakatifu akakamatwa nao akafungwa akatiwa gerezani mwa mji wao, ndio Rumi katika Italia. Akiwamo humo gerezani akaongoa asikari wawili waliomlinda, akawabatiza, wakawa Wamasihiya. Hatta siku moja rafiki zake

Digitized by Google

wakamjia, wakamwambia, "Ee baba, ondoka bassi, katoka gerezani, wende zako. Asikari hawa ndugu zetu, wanazo funguo, watafungua milango. Kwa nini kukaa humo? Utachinjwa tu. Ukikimbia, utapona, utapata nafasi ya kuhubiria watu wangine, nao wataongoka kuwa Wamasihiya vile vile na sisi. Ukikaa humo, utakufa tu bassi." Wakamsihi sana. Naye Petro akafanya mashaka mengi kwa nafsi yake, "Nikae humo, ao niende zangu?" Halafu yake akakubali. Wakangojea usiku, nao walinzi wakafungua milango, mtu asiwaone, wakatoka wote watatu wakapita katika njia za mji, watu wakawakuta njiani, ikawa giza, wala hawakumtambua kama ndiye Petro, mkuu wa Wamasihiya, amefunguliwa anakimbia. Bassi na mji ule umezungukwa na kuta ndefu na nene, hakuna kutoka mjini illa kwa milango. Wakakaribia mlango, mngoje mlango akawauliza habari, wakampa fetha yake ya kupisha watu mlangoni, akawaacha wakatoka nje. Petro akaagana nao walinzi wale wa gereza, wakarudi, yeye akashika njia peke yake.

Hatta akipita njiani, na bado kuendelea mbali. Bwana wetu (ndivyo tulivyohadithiwa) akamtokea, anakwenda mjini naye mwenyi msalaba wake begani mwake. Petro akasangaa mno, akamwambia, "Ee Bwana, wendapi?" Bwana akamwambia, "Mimi nakwenda Rumi, nisulubiwe humo marra ya pili." Akaenda zake mjini, asionekane tena. Petro akafikiri sana maneno haya katika roho yake. "Bwana yule amekwisha kusulubiwa zamani, amepata miaka zayidi ya thelathini. Bassi atakani? Hawezi kufa tena. Bassi nini? Ah! nasikia kidogo. Sisi tuliobatizwa, si sisi mwili wake Masiya, na viungo vyake mmoja mmoja? Labuda maana yake, Uwe tayari na kufa kwa ajili yangu. Mimi nimekufa kwa ajili yako. Kweli, imenielea." Petro akaondoka, akaenda

Digitized by Google

zake naye mjini, akajitoa mwenyewe akafungwa gerezani vile vile. Akaandika barua kwa wenziwe Wamasihiya, kama, "Najua kama upesi nitaivua masikani yangu, (ndio mwili wake), kama Bwana wetu alivyonionyesha."

Baadaye siku si nyingi Warumi wakamtwaa yule Petro, wamsulubishe. Akawasihi asulubiwe kitwa chini, sababu akaona hastahili kufa vile vile alivyokufa Bwana wake. Wakakubali, wakamsulubisha kitwa chini, akafa.

## BLANDINA,

### MJAKAZI ALIYEKUWA MSHUJAA.

WAKATI wa zamani Wamasihiya walionewa sana kwa ajili ya imani yao ya kimasihiya. Palikuwa na kijana mjakazi katika mji mmoja wa Ufransa, Warumi walioumiliki mji ule, na bibi yake bibi ya kiungwana, jina lake Teodora, na mjakazi jina lake Blandina. Yule mjakazi akawa Mmasihiya, na bibi yake huabudu sanamu na miungu ya uwongo. Bibi yule akamstaajabu mjakazi wake, alivyo mwema siku zote na mnenyekevu na mtendaji kazi. Hatta na siku moja kijana akapigwa sana burre, asikose neno mwenyewe, naye akastahimili kikondoo. Bibi yake akazidi kumstaajabu. Ikawa bibi akaondoka anakwenda hekaluni kutoa sadaka kwa sanamu zilizomo. Akamwita mjakazi yule akasema, "Twende zetu hekaluni, tutoe sadaka." Naye hakukubali, akamwambia, "Siendi mimi." Bibi akasangaa, sababu kijana yule humtii sana siku zote, sasa amekataa. Akamwambia, "Gissi gani huendi?" Akamwa-

Digitized by Google

mbia, "Siabudu sanamu, mimi Mmasihiya." Yule bibi akafikiri kwa nafsi yake, " Huyo mwema lakini, —labuda heri kuwa Mmasihiya." Wakakaa siku. Bibi yule akampenda sana mjakazi, akamtunza kama mtoto wake.

Hatta siku moja liwali wa mji akafanya shauri ya kuwaharibu Wamasihiya wote waliomo, akatuma asikari kuwatafuta wahukumiwe. Wakakamata wengi, na askafu jina lake Pothino na shemasi mmoja na Blandina pia na wangine. Wakafungwa gerezani, halafu wakapelekwa kwa kathi, wahukumiwe naye. Wangine wakaikana imani ya kimasihiya, wakaachwa, wangine wakaiungama wakahukumiwa kuteswa sana hatta kufa. Yule mjakazi akawa shahidi mwema, akaiungama imani yake kwa ushujaa, akahukumiwa kuuawa.

Palikuwa katika mji ule uwanda mkubwa na mweupe, umeviringana pia, mwenyi ua wa mawe pande zote, na nje ya ua viti vyingi vya kukalia kama madaraja vikienda juu kwa juu pande zote za uwanda, na maana ya kutengenezwa hivi watu wakae madarajani wapate nafasi ya kutazama yote yaliofanyika ndani ya uwanda. Na uwanda huo kazi yake hii. Waliohukumiwa kufa na serkali, huwekwa katika uwanda, huchinjwa na asikari huuawa na nyama kali za mwituni na vinginevyo. Ndio siku kuu ya watu wa mji na uchezo wao walioupenda sana, kutazama watu wakipigana wakiuana katika uwanda. Na uwanda namna hiyo umekwitwa amfiteatro.

Bassi tena watu wa mji ule wakafanya siku kuu, wakakusanyika wengi wengi wakakaa katika viti pande zote za uwanda. Mji ukaachwa mtupu pasipo watu. Wamasihiya wengi wakawekwa katika uwanda wakauawa. Hatta na yule mjakazi kijana akaletwa, wakamwambia, "Piga kiyowe tu, utaa-

Digitized by Google

chwa. Ndio ishara ya kutubu na kuikana imani yako." Akasema, "Vema." Kwanza wakamwumiza sana kwa mijeledi, ngozi ikachubuka pia, hakutoa kelele. Watu wote wakafanya uchungu, wakasema, "Hatta mjakazi atatushinda. Haya bassi." Wakaleta kiti, na kiti kile cha chuma pia, wakatia moto, kiti kikapata moto sana, wakamweka kijana katika kiti, akaungua akashikwa na maumivu makali sana yasiyofanana na neno. Hakutoa kelele. Hatta pakawa na mtoto mmoja Mmasihiya anateswa pale pale anapasuliwa kwa nguvu mwili wake na viungo vyake, naye karibu na kupiga kelele, ndio kukufuru. Mjakazi yule amefungwa kitini, anaunguliwa moto sana, asijiangalie mambo yake mwenyewe, akamwangalia yule mtoto, akamfariji moyo akimwambia, "Ewe ndugu, usisahau, Yeye ndipo pale mbinguni mwenyi kutuombea kwa Baba, ndipo papa hapa anatutia nguvu." Watu waliohuthuria wakampigia makelele sana, wakataka auliwe mbali. Wakamtoa mjakazi kitini, wakamkunja katika wavu, wakaleta fahali mkali mwenyi pembe, akamwangukia akamchoma sana akamrusha juu akamkanyaga chini. Yule kijana akanyamaa kimya, wala hajafa.

Hatta mwisho na liwali mwenyewe akachoka, wote wakamsangaa ginsi alivyoishika imani yake, ndio alijaliwa na Muungu kuwa shahidi mwema wa Bwana wetu. Liwali akaamuru kuleta upanga kumkata kitwa. Akafa.

Bibi yake akaingiwa huzuni sana akafikiri mambo haya yaliyompata mjakazi mtaowa, akatubu akaongoka kuwa Mmasihiya.

Digitized by Google

## SAPRITIO,

### MTU ASIYEMSAMEHE RAFIKI YAKE.

Siku za kwanza Wamasihiya walionewa marra nyingi kwa ajili ya imani yao ya kimasihiya. Palikuwa na mtu katika mji wa Sham uliokwitwa Antiokia. Jina lake mtu yule Sapritio, naye kasisi. Akakamatwa na asikari wa liwali akachukuliwa kwa kathi ahukumiwe. Kathi akamwambia, "Toe sadaka tu, utaachwa." Akajibu, "Sitoi sadaka mimi, siabudu sanamu wala miungu ya uwongo. Naamini kwa Muungu mmoja aliyeviumba vitu vyote, na Mwana wake wa pekee." Akaathibiwa sana, akashinda asiikane imani yake. Wakamchukua achinjwe.

Bassi na huyo alikuwa na rafiki mmoja, jina lake Nikeforo, wakapendana sana. Hatta ugomvi ukawapata, wakachukiana, hawaonani kabisa. Bassi yule Nikeforo (na huyo pia Mmasihiya) akatubu akaenda zake kwa rafiki yake akamtaka sana kumsamehe. Yule kasisi hakukubali. Nikeforo akatuma rafiki zake wawili wampatie masamehe. Akakataa. Tena akaenda mwenyewe, akamwomba tena kwa ajili ya Isa Masiya, amwachie kosa lake, asipate illa kutharauliwa tu vile vile. Bassi na saa ile Sapritio alipo akichukuliwa na asikari anawe, rafiki yake akamlaki njiani akamsihi kwa unenyekevu, "Ewe shahidi bora wa Masiya, nalikosa siku ile, nimetubu, bassi unisamehe tu." Yule hakusema neno, hakugeuza uso. Nikeforo akazidi kumwomba kwa juhudi, "Ee bwana, unisamehe tu, nawe marra unaingia peponi. Kwa ajili ya urafiki wetu wa kwanza na ya Bwana aliyesema katika msalaba,

Digitized by Google

"Baba, uwasamehe, hawajui wafanyavyo." Yule akanyamaa kimya.

Wakafika mahali palipo na mti mfupi umekazwa chini sana, nao wenyi damu. Na kazi yake mti huo, killa achinjwapo mtu, kitwa chake huwekwa juu ya mti. Sapritio akanyamaa akautazama mti na asikari wanamfunga kamba, akaanza kutetemeka. Asikari akamwambia, "Njoo karibu." Akakaribia. Na yule rafiki anafuliza kumwombaomba amsamehe, asipate. Asikari akamwambia Sapritio, "Piga magote." Yule kasisi akasema kwa sauti ndogo na yenyi hofu, "Kwa nini bassi?" Akasema, "Sababu umekataa kutoa sadaka, kuabudu miungu yetu." Akamwambia, "Nimegeuka. Sikatai mimi. Lete sadaka." Watu wakamcheka sana kwa kuwa mwoga. Hatta Nikeforo akafathaika sana, akamwambia, "Ewe, wasemani? Umesahau yaliyoandikwa, Uwe amini mpaka kufa, utapewa taji ya fakhari." Naye akamjibu, "Sivyo. Nimegeuka. Lete sadaka." Wakamchukua tena kwa kathi, kathi akamwacha. Na yule rafiki yake akakaa akawaambia watu na asikari, "Mimi Mmasihiya. Mimi sigeuki." Wakamfunga, akahukumiwa kuchinjwa, akafa pale pale.

## MASHAHIDI AROBAINI.

PALIKUWA na mji katika Armenia, uliokwitwa Sebaste, Warumi wakaumiliki, na kwa sababu ya kuwa kama mpakani mwa milki yao kwa mashariki na adui zao karibu, wakaweka asikari wengi mjini mle, waulinde. Bassi katika asikari hao wakawa arobaini walio Wamasihiya, wenzio wote makafiri

Digitized by Google

bado, wanaabudu sanamu. Na siku zile mfalme wa Rumi, alikionea sana Wamasihiya kwa maana ya imani na ya dini yao. Bassi na watu hao arobaini wakateswa sana na akida yao, kwa sababu hawa'aki kuabudu sanamu. Wakapigwa bakora, wakapigwa mijeledi yenyi risasi, ngozi ikapasuka, wakapata maumivu machungu, wasitiishwe roho zao, wakijua yaliyoandikwa, "Msiwaogope wauao mwili wasiweze kuua roho, afathali mmwogope awezaye kupoteza na mwili na roho motoni." Akida akafanya uchungu, akanyamaa siku.

Ukawa wakati wa baridi nyingi, napo penyi baridi nyingi mahali pale, pepo za baridi zikavuma, theluji ikanya, maji yote yakaganda kwa baridi, na inchi pia imekauka ngumu kama chuma. Bassi baridi ile kali kweli kweli. Watu wote huvaa nguo nzito na nene, huwasha mioto mikubwa. Hatta asikari wangine, kazi yao kukaa nje usiku kuulinda mji, wakaonekana assubui wamekufa kwa baridi. Akida yule akafanya karamu katika nyumba yake, akanywa mvinyo, akasema moyoni mwake, "Nitawashinda wakaidi wale usiku leo." Pakawa katika mji uwanda mweupe, na katika uwanda ziwa la maji, maji yameganda pia kwa baridi kwa ginsi yatachukua watu na magari yakivuka juu yao. Na karibu ya ziwa hekalu la muungu wa uwongo, na nyumba ya muadini aliyelingojea hekalu. Bassi akida akaita asikari wote akawaambia, "Tazameni ziwa hili. Amri yangu ndio hii. Waasi hao wasiokubali kuabudu miungu yetu sisi watavuliwa nguo, watasimamishwa ziwani kule mpaka assubui. Mtu akikubali kuingia hekaluni kutoa sadaka, atapewa nguo na chakula, atapona. Wasiokubali, watakaa tu. Bassi." Tena akaagiza kenturioni, ndiye mkuu wa kikozi kimoja, jina lake Sempronio, kufanyiza vyote alivyoamuru, akaenda zake kwa nyumba yake. Sempronio

Digitized by Google

akawatwaa watu wale arobaini akawavulia nguo, akawaweka ziwani. Ulipofika usiku, baridi ikazidi sana, killa mtu wa mjini huingia nyumbani, hufunga mlango na madirisha, na asikari vile vile. Nao arobaini wakikaa nje, wanasimamia maji za ziwa yaliyoganda kwa baridi. Halafu wangine wakaanguka wakalala usingizi wasiamke tena, wangine wakatembea huko na huko kwa haraka, wajipashe moto kidogo, wangine wakasimama kimya wakimwomba Muungu rohoni mwao, wangine wakafarijiana, wakisema, "Heri na baridi hii kuliko moto wa jehannum usiozimika." "Sisi asikari wa Jemadari aliye juu. Tukifika kwake, haiko baridi, Yeye ndiye jua." "Tunashindana na Shetani, tukijaliwa tutamshinda, sote arobaini." Wakafikiri sana habari za hesabu hiyo arobaini, kama Waisraeli wamepotea jangwani miaka arobaini, Musa amekaa mlimani Sinai siku arobaini marra mbili, Eliya amewezeshwa kusafiri siku arobaini asipokula, Ninawi ikajaliwa nafasi ya kutubia siku arobaini, Bwana wetu amefunga siku arobaini, amelala kaburini kama saa arobaini, akakaa duniani siku arobaini baada ya kufufuka kwake. Wakaombaomba, "Tuokoke, Ee Bwana, sisi sote arobaini, sote arobaini."

Sempronio yule akaingia chumbani akajikunja katika mkeka akalala. Akaota ndoto, na katika ndoto yake anasimama naye mwenyewe kule ziwani, akiwatazama wenziwe wale washujaa. Hatta malaika akashuka mbinguni, anachukua taji ya thahabu yenyi kung'aa isivyofanana na kitu. Tena akachukua ngine na ngine na ngine, aka'ambulikana analeta taji kwa killa mmoja astahimiliye mpaka kufa, akaleta taji thelathini na kenda bass. Sempronio akaamka akasema, "Nini hii bassi? Naona watu hao watapewa zawadi bora na Muungu wao, lakini mmoja hapewi." Marra akaitwa akaamka akatoka

Digitized by Google

chumbani akasikia habari mmoja wao arobaini ameondoka ziwani anakubali kwenda hekaluni kuabudu. Akamwona yupo penyi moto, anajipasha moto anakula, na uso wake kama uso wa mtu anayechomeka maumivu makali kwa ndani. Hatta na Sempronio akasema, "Amepata fayida, asione fayida." Akatoka tena kutazama waliobaki huko ziwani thelathini na kenda, wengi wamekwisha kufa, walio hayi wanafuliza kuomba vile vile, "Tuokoke, Ee Bwana, sisi sote arobaini." Akawaambia, "Wajinga nanyi, haiwezikani. Hamjui mwenzenu mmoja amekwisha ondoka?" Akajibiwa, "Muungu mwenyezi awezaye yote," nao wakiomba vile vile. Marra yule kenturioni akania kwa nafsi yake, "Yule amekosa taji. Nipate mimi tena?" Akaenda upesi kwa akida akamwamsha, akamwambia, "Nami hapa Mmasihiya." Akawekwa pale pale ziwani. Ilipofika assubui wamekufa wote, nao watu arobaini kama walivyoomba.

## KUFUNGA NA KUFUNGUA.

Zamani palikuwa na hekalu katika inchi ya Sham. Na hekalu lile kama nyumba kubwa na nzuri ya mawe ya thamani, yenyi nguzo nyingi za marmár, na ukumbi mrefu ulionakishiwa wa mawe meupe, ukingaa sana kama jua; hekalu limejaa ndani hazina na sadaka zilizowekwa humo. Kwa maana watu wengi huliendea siku kwa siku kutoa sadaka na kuabudu muungu wa uwongo, na kumwuliza habari za mambo yo yote waliyoyataka. Pakawa ndani ya hekalu sanamu nzuri ya fetha pia, na muadini mmoja ndiye mngoja hekalu,—na mwanamke mchawi



Digitized by Google

tena huketi katika paango ndani kwa ndani, anawezeshwa na Shetani kutoa majibu kwa watu wamtakiao habari.

Hatta siku moja alikuwa askafu Mmasihiya, mzee na mwenyi mvi, anasafiri akipita njiani karibu na hekalu. Ikawa jioni, yule mzee amechoka, anatafuta pa kutua, alale usiku. Akaona mlango wa hekalu umeachwa wazi, yule muadini amekwisha kwenda zake, hamna mtu ndani. Akasema kwa moyo wake, "Ntalala mumo humo. Napajua kuwa pabaya kweli kweli. Lakini mimi Mmasihiya. Wala mashetani wala wangoje wao hawawezi kuniumiza, akiwapo Bwana wetu pamoja nami." Bassi akajiandikia alama ya msalaba, akaingia hekaluni, akateka maji kisimani kilichomo ndani, akanywa akala mkate. Kiisha kula, akapiga magote akamwomba Muungu, amlinde amtie nuru katika giza, amfukuzie hatari zote za usiku kwa ajili yake Isa Masiya. Kiisha kusali, akalala akapata usingizi mzuri. Ilipopambazuka assubui, yule askafu akaondoka akaomba vile vile akaenda zake.

Bassi na muadini akarudi kwa kazi yake ya kungojea hekaluni, akatoa sadaka za assubui, akachinja ng'ombe, akavukiza ubani, akatia maua, ngoma ikapigwa mbele ya sanamu ya fetha.

Halafu yake maskini akaja akaingia ukumbini, akamwambia muadini, "Nataka habari za ng'ombe zangu, wamenipotea usiku wote wa'nne. Nataka kujua, wamekwendapi." Muadini akamwambia, "Na mapesa je? Asipewe ada yake kwanza, muungu hakujibu." Akamwambia, "Reale hii yatosha?" Akamwambia, "Hatta kwa reale tatu hujibiwi." Yule maskini akasema, "Ah! nifanyeje mimi? Nipate wapi habari za ng'ombe zangu? Hapana illa hapa tu." Muadini akamwambia, "Lete reale tatu bassi." Akamwambia, "Hatta mimi sinazo." Akasema, "Ko-

Digitized by Google

ndoo mmoja je?" Maskini akasema, "Halafu yake ntaleta. Sharti kukamata ng'ombe zangu."

Wakaingia hekaluni, hatta wakafika paangoni mle, pakawa giza tu, na mwanamke yule mchawi anaketi ndani. Muadini akamwuza habari akisema, "Ewe mnenaji, ng'ombe za huyu wamekuwaje?" Mchawi akanyamaa, hatoi neno. Muadini akamwombea muungu wake tena, asipate majibu. Akamlilia sana kwa sauti kuu. Hatta mchawi akatetemeka akisema, "Mgeni ameingia humu. Nimefungwa. Sina maneno." Muadini akafanya uchungu na ghathabu sana, akamwuliza maskini, "Nani aliyeingia humo?" Akasema, "Mtu alikuwapo usiku, askafu Mmasihiya, nalimchungulia alipotoka assubui. Naye mganga pia, amefanya miujiza mingi." Akamuza, "Amekwendapi?" Akamwambia, "Amekwenda mjini." Muadini akatwaa selaha, akapanda frasi, akaenda mbio, akampata yule askafu anakula penyi mti. Akamtukana vibaya, akisema, "Ee mshenzi wee, Ee kafiri wee, Ee mchawi wee, Mnazareni, mwabudu aliyesulubiwa, utuponye marra nawe." Askafu akamjibu kwa upole, "Unani, mwanangu?" Akasema, "Walilala hekaluni, umenyamazisha mnenaji wake muungu. Umponye, usipomponya, utachinjwa." Akamwambia, "Hatta na mimi mtu mmoja mzee maskini namweza muungu wako? Muungu gani yeye? Mimi sina nguvu ya kumponya. Wallakini angalie tu nguvu zake Yeye ninayemtumikia." Akatwaa karatasi, akaiandikia maneno, akaikunja, akampa, akasema, "Tweke juu ya mathbahu, yule mchawi atanena." Muadini akamwambia, "Wamasihiya wote ng'ombe na mbuzi na mbwa, hawasemi uwongo lakini." Akaenda zake. Karatasi ile imeandikiwa maneno haya, "Gregorio (ndilo jina lake askafu) kwa shetani, karibu." Muadini akaiweka khati juu ya mathbahu, akamwendea

Digitized by Google

mchawi. Akiwa akienda, yule maskini akamtokea, akilia furaha, "Amenena, amenena. Ng'ombe zangu wako huko mjini." Muadini akafikiri sana mambo haya kwa nia yake, mchana usiku mwezi mzima, ginsi yule askafu alivyoweza funga na fungua. Akatubu akaongoka kuwa Mmasihiya, akabatizwa, baadaye akawa askafu mwenyewe.

## MJINGA NA MWALIMU.

WAKATI wa zamani wamasihiya wakanenana sana mambo ya imani yao ya kimasihiya. Wakataka kupatana tena, wapate kuishika imani moja kwa moyo mmoja, ginsi alivyotuagiza Roho Mtakatifu. Bassi askafu wengi wa Kanisa lo takatifu wakakusanyika, wafanye shauri pamoja watangaze yaliyo kweli, kama Mitume walivyofanya katika Yerusalemi mbele, wakakusanyika katika Stambuli, ndipo akaapo Sultani Rum siku hizi, lakini kwanza ulikuwa mji wa Wamasihiya mwenyi makanisa mengi mazuri.

Palikuwa na mtu kafiri, naye mwalimu mkubwa na mwenyi akili sana, hatta akajisifu kwa wazi ya kuwa anaweza kwa maneno yake merevu kuvuta mtu ye yote kuikana imani ya kimasihiya. Na askafu wenyi elimu nyingi na akili nyingi siku moja wakawa wanasimama katika peupe palipo kati ya mji, watu wengi wakawapo pale pale wakitaka kusikia shauri lao. Yule mwalimu akawatokea, akawaambia, "Sikilizeni, Enyi Wamasihiya. Tushindane kwa maneno. Nipe mtu ashindane nami, maana yake yeye aliyesulibiwa, ni Muungu ao siye

Digitized by Google

Muungu? Bassi mimi nikishindwa na mtu wenu, kwa maneno nisiyoweza kukatalia, nibatizwe. Naye akishindwa na mimi, aabudu sanamu." Wamasihiya wakanyamaa, watu wengi wakaja mbio wakakutanika wasikie maneno haya. Askafu wakaulizana, "Nani awezaye kushindana naye vema? Haifai imani yetu takatifu inenewe vibaya, itiwe aibu mbele ya watu." Hatta akaondoka mtu maskini, mkulima mizabibu, ndio kazi yake, akasema wazi, "Ewe rafiki, hatta mimi hapa nataka kushindana na wewe." Watu wakampigia kelele, wakisema, "Sivyo, sivyo, huyo mjinga pia, hafai kwa kushindana na mwalimu." Askafu mmoja mkubwa akaondoka akawaambia watu, "Hatta kwa kanwa la watoto wachanga Muungu aweza kutimiliza sifa zake." Watu wakasema, "Haya bassi, washindane, mjinga na mwalimu." Na yule mwalimu akakataa, akisema, "Sishindani mimi na mjinga." Askafu akamwambia, "Bassi mjinga amekushinda." Mwalimu akasema, "Ndio uwongo. Haya, tushindane tu." Askafu wakasemana, "Jambo hili namna moja na lile, Daudi na Golia Mfilisti."

Bassi maskini akasema, "Ewe mwalimu, nitangulie mimi kukuuliza, nawe tena unijibu. Usipoweza kunijibu, umekwisha shindwa. Siyo?" Mwalimu akasema, "Ndio." Masikini akasema, "Haya bassi. Naanza sasa. Ewe mwalimu, kuna Muungu mmoja, aliyeviumba vitu vyote vilivyomo mbinguni na katika inchi, na Bwana mmoja Isa Masiya, mwana wake wa pekee, Bwana wetu, na Roho mmoja mtakatifu, ndiye mfariji. Nawe umekana imani hiyo. Bassi kwa sababu gani umeikana? Unijibu. Lakini kwanza kwa jina lake Bwana wetu Isa Masiya, nakuamuru uwe bubu. Bassi ujibu." Mwalimu akaondoka, akafumbua kinwa, halitoki neno. Ulimi wake hautendi kazi. Akajaribia kunena marra nyingi,

Digitized by Google

asiweze kutoa hatta neno moja. Watu wakapiga kelele kuu, "Mwujiza huo, mwujiza huo." Hatta na makafiri wakasema, "Mmasihiya aliyeshinda." Yule mwalimu akaenda zake. Askafu aliye mkubwa akawaambia wenziwe kwa maneno ya Paolo, "Muungu ameyachagua mapumbafu ya duniani illi waaibike wenyi hekima, hatta yasiyo nayo, yaliyo nayo yapotee, mwenyi mwili asipate kujisifu mbele ya Muungu."

## MICHEZO MIBAYA.

KATIKA hadithi ya Blandina, mjakazi aliye mshujaa, zimeandikwa habari za Warumi walivyopenda sana kwa siku kuu zao kwenda kwa uwanda mkubwa uliofanyika kwa kazi hiyo hiyo, kutazama watu wakipigana wao na wao, wakiuawa na nyama za mwitu na vinginevyo. Ndio mchezo wao. Nako katika Rumi uwanda mzuri na mkubwa kupita zote, uliokwitwa Koloseo, viti vyake vyaweza kuweka watu elfu themanini na elfu saba, viti vimetegemea matao na nguzo, vimejengwa juu kwa juu pande zote za uwanda. Na wafalme wa Rumi walipoongoka kuwa Wamasihiya hawakuthubutu kwanza kuwagombeza watu wasifanye mchezo huu. Watu wakaupenda sana.

Hatta siku moja Warumi walikuwa wanafanya siku kuu. Killa mtu akaenda uwandani, wakasonganasongana katika viti vilivyouzunguka, wakatazama watu wanashindana katika uwanda wanauana kwa panga na mikuke na visu wanapigana na nyama kali za mwitu. Palikuwa na mtu, mtaowa na

Digitized by Google

mcha Muungu, amesikia habari za michezo hii mibaya, naye akikaa mbali mbali katika inchi ya Sham, na jina lake Telemako. Akaondoka akasema moyoni mwake, "Hatta mimi nakwenda Rumi kukomesha michezo hii, haiwapasi Wamasihiya kufurahiwa nayo. Najua mimi mtu mmoja tu, nao watu wengi watanikasirikia. Haithuru. Nikifa, nife bassi. Nijaribie tu." Akaenda kwa Rumi, mwendo wa siku nyingi, akakuta siku kuu ile, akaingia mwenyewe mahali pa michezo, akaona watu wanapigana katika uwanda, na wengi wengi wanaowatazama furaha. Marra yule akaruka katika uwanda, akawaangukia wanaopigana, akawapinga wasipigane tena. Watu wote wenyi kutazama wakafanya ghathabu kuu, wakaruka nao katika uwanda, wakamkamata yule mshujaa wakampigapiga mawe na fimbo, akafa. Alipokwisha kufa, marra wakageuka wakaingiwa haya na majuto machungu. Mfalme akawaambia, "Kweli mtu huyo shahidi mzuri wa Isa Masiya. Michezo hii haifai." Watu wakakubali, wasifanye michezo ile tena. Ndivyo ilivyokwisha.

## WATU WALIOSINZIA MIAKA MITEEN.

Zamani za kale Wamasihiya walifukuzwa sana kwa ajili ya imani yao ya kimasihiya. Palikuwa na watu saba vijana katika mji wa Anatolia (Asia Minor), uliokwitwa Efeso, nao Wamasihiya. Wakakutana pamoja wakafanya shauri, wafanyeje. Sababu Dekio, mfalme wa Rumi, alikuwa anasumbua sana Wamasihiya, wakatafutwa pote wakachukuliwa wauawe.

Yule wa kwanza akasema, "Angalieni, ndugu, ginsi tunavyofukuzwa sisi Wamasihiya. Haya bassi, tujitoe kwa liwali, sababu tukifa kwa ajili yake Bwana wetu Isa Masiya marra tutafika kwake mbinguni." Wa pili akasema, "Hakufai kujitoa, kwani kujitoa kwa liwali ndiko kujifisha wenyewe. Muungu hataki watu wajifishe. Amesema, 'Mkifukuzwa katika mji mmoja, kimbieni hatta mwingine.'" Wa tatu akasema, "Hatta na Kanisa lo takatifu ndivyo lilivyothihirisha. 'Hakufai kujitoa wenyewe.'" Wa 'nne akasema, "Shauri langu hili. Twende tujifichie si mbali na mji. Halafu yake mafukuzo haya labuda yatakoma." Wa tano akasema, "Nami najua pazuri pa kufichia, ndipo paango penyi mlima Latmo. Hatta nimelala humo marra nyingi mwenyewe." Wa sita akasema, "Nina shauri tena, ndilo kuuza kwanza mali zetu zote tuwape maskini. Hivyo twaziweka mbinguni." Wa saba akasema, "Shauri hilo jema sana." Wote saba wakaenda zao wakauza mali zao, wakampa askafu, awape maskini, wakatoka mjini, wakafika hatta kwa mlima Latmo. Wakaliona paango, limefunikiwa pia na majani na magugu, upo tena mti mmoja mdogo unapanda karibu na mlango. Ikawa jioni wakakaa kidogo wakitazama jua linakuchwa kwa fakhari, wakala chakula, wakanywa maji, wakaweka makombo ya chakula kwa assubui wakasali wakalala usingizi.

Assubui wakaamka, wakamshukuru Muungu, wakataka makombo yale yaliyobaki jioni. Wakatafutatafuta sana wasiyaone. Wakastaajabu, wakasema, "Labuda nyama walioyachukua makombo, ao waivi." Wakatoka nje kuyatafuta. Mmoja akasema, "Enyi tazameni mti huo. Jana ulikuwa mdogo, sasa mkubwa sana na mkukuu, umeoza ndani. Ah! Ajabu hiyo!" Wenziwe wakasema, "Ajabu kweli kweli." Wakasema, "Tupateje chakula bassi? Ha-

tuna buddi kwenda mjini." Mmoja, jina lake Iambeliko, akasema, "Mimi hapa niende. Nikikamatwa nikifa, haithuru." Wakakubali wenziwe, wakamsindikiza njiani mpaka chini ya mlima, wakarudi paangoni, naye akaenda zake peke yake.

Ikawa assubui na mapema, akapita njia kuu, asikute watu illa mmoja mmoja tu nao akawathani kuwa wageni pia, namna ya nguo zao ilivyo ngeni, nao wakamsangaa yeye vile vile, wasimwambie neno. Akashika njia akakaribia mjini akaenda taratibu, asipate kukamatwa. Akautazama mlango wa mji, napo ajabu mno, msalaba mzuri wa mawe umewekwa juu yake. Akafikiri moyoni mwake, "Ah! jana hapana msalaba, leo upo. Naona hila hiyo ya kuwadanganyia Wamasihiya." Akaingia mjini. Akasema, "Mji umejaa wageni leo. Sitambui hatta mtu. Tena wote wamevaa sawa sawa. Wako wapi watu wa mjini? Kwani hunitazama uso?" Wakamtazama sana kweli kweli. wakasemana, "Mtu gani huyo? Tazama nguo za kishenzi. Mgeni na mjinga huyo." Akaendea punde, akaona jumba refu na zuri la mawe ya marmár, lenyi mnara, na juu ya mnara msalaba mkubwa wa shaba. Akasema kwa nafsi yake, "Ee Muungu, unirehemu. Uchawi hapo. Sifahamu hatta njia, hatta nyumba. Bassi nini? Akili zimenipotea?" Akakuta na kijana akamwambia, "Ee rafiki, njia hii imekwitwa nini? njia ya Artemi, siyo?" Yule kijana akamchekelea, akasema, "Ee bwana, wewe mgeni. Njia ya Kiyama hii." Akasema, "Ya Kiyama? Jana njia ya Artemi, leo ya Kiyama. Ah! uchawi huu." (Na Artemi ndio jina la muungu wa uwongo, Waefeso waliomwabudu sana.) Akaona duka la mwokaji, akamjia, akataka mikate sita. Mwokaji akampa. Akatoa fetha, akataka kuivunja fetha. Mwenyi duka akatazama fetha ile akasema, "Fetha hii ya zamani sana. Umeipa-

Digitized by Google

tapi?" Akamwambia, "Sijui. Nimepewa tu." Yule mtu akamwita mwenziwe anaketi hapo karibu, akamwonyesha fetha. Wote wawili wakaiangalia sana, wakamjia kijana, wakamwambia, "Hatuna buddi kutafuta habari za fetha ile. Unazo zingine nawe?" Kijana akafathaika sana, akawaambia, "Twaeni zote bassi. Uniache tu." Akatoa kifuko chake cha fetha. Yule mwokaji akasema, "Bado kwanza wee." Akafunga mlango, akazitazama fetha, akamwambia, "Ee rafiki, umeokota fetha hizo, fetha za watu." Kijana akatoka haraka, akakimbia. Watu wakamfukuza wakamkamata, wakamfunga wakamchukua kwa kathi. Naye akichukuliwa akauangalia mji umegeuka pia. Hapana mahekalu ya miungu ya uwongo, hapana njia za kwanza, na misalaba ipo pote. Wakafika hatta kathi, mwokaji akamstaki ya kuwa ana fetha zisizotumika wala kutambulikana siku hizi. Labuda ameokota, labuda ameiba. Kathi akasema, "Huyo asema kiyonani ao kirumi?" Mwokaji akamwambia, "Asema kiyonani, bwana, lakini si vema."

"Jina lako nini?"

"Jina langu Iambeliko."

"Wakaa wapi?"

"Katika njia ya Ares."

"Katika mji upi?"

"Mumo humo, katika Efeso."

"Njia ya Ares! Ah! Siijui mimi."

"Ee bwana, waijua njia ile iendayo toka hekalu la Ares mpaka amfiteatro?"

"Una wazimo wee. Hakuna njia ile." Hatta mzee mmoja aliyekuwako akamwambia kathi, "Ee bwana, nimesikia babu yangu akisema, ilikuwako njia ya Ares, zamani sana, sasa imegeuka." Kathi akasema, "Mambo haya hayanielei. Bassi wewe Mmasihiya?" Kijana akaona sasa atakufa marra,

Digitized by Google

akaungama, "Ndio, mimi Mmasihiya." Kathi akamwambia, "Vema. Nalikuthania u kafiri." Kijana akazidi kusangaa, akamwuliza kathi, "Na Dekio je? Dekio, mfalme wa Rumi?" Akajibu, "Una wazimo kweli kweli wewe. Dekio amekwisha kufa zamani, imepata miaka miteen." Akasema, "Muungu ajuaye, jana alikuwa mzima." Wakaita mtabibu wakamwambia, "Angalia huyu, hawezi kitwa, ana wazimo, ao nini?" Mtabibu akasema, "Naona mzima huyo, lakini amefathaika sana roho yake." Saa ile ile askafu wa mji akaingia chumbani mwa hukumu. Wote wakamwondokea wakamsalimia. Kathi akamwelezea habari za kijana. Bassi askafu akamwuza kijana, "Ee mwanangu, nipe kisa chako." Yule kijana akamwambia, "Baba wangu, kisa changu si chingi. Jana nalitoka mjini, sababu Dekio anafukuza sana Wamasihiya, nikalala usiku katika mlima Latmo, mimi na wenzangu watu sita. Leo nikaja mjini kutafuta chakula, kumbe mji wote umegeuka pia, hatta nimeambiwa ya kwamba Dekio amekwisha kufa yapata miaka miteen." Askafu akasangaa akafikiri, halafu yake akamwuliza kwa werevu, "Sikilize, Mwanangu. Wajua maneno haya?" Askafu akanena maneno ya imani ya Nikaya, ndiyo ianzayo kwa, "Naamini kwa Muungu mmoja." Na maneno ya imani hiyo hayajaandikwa bado katika wakati wa Dekio, alipolala paangoni kijana yule. Baadaye yamejulika sana na Wamasihiya wote. Bassi askafu alipokwisha kunena maneno yale, kijana akasema, "Maneno mazuri hayo, lakini mimi sijayasikia." Akamwambia, "Nani aliye askafu wa mji siku zako?" Akamwambia, "Aithala, ndilo jina lake." Wakafuliza kumwuza maswali mengi. Hatta polepole jambo lote likatokea wazi, kama kijana yule amelala usingizi wa muda wa miaka miteen. Wote wakafurahi, wakimwuliza

Digitized by Google

habari za siku zake, wakimwonyesha mji ulivyogeuka kuwa wa kimasihiya. Wakaenda kwita wenziwe wale sita, nao wakasangaa sana. Halafu yake Muungu akawatwaa, wakalala wasiamke tena.

## JUMA YA PILI YA MITENDE.

### NDIO JUMA YA PILI MBELE YA PASAKA.

UKO mji katika Ufransa, unakwitwa Metz, mwenyi ngome kubwa na gereza ndani yake, na katika gereza akawa mtu amefungwa, naye askafu na mcha Muungu sana. Na sababu yake ya kufungwa ndio hii, amemnenea mfalme wake, kama Yohanna mbatizaji alivyomnenea Herode mfalme wa Wayahudi, kwa maana ya thambi zake na mabaya aliyoyafanya.

Hatta ikawa juma ya pili mbele ya Pasaka, na kwa desturi ya Wamasihiya tangu zamani, watu wote hupita taratibu kati ya mji siku ile, huenda kanisani wenyi majani ya mitende mikononi mwao, ndio ukumbusho wa Bwana wetu alivyoingia Yerusalemi kwa shangwi kama siku ile ile na watu wengi waliofuatana naye wenyi majani ya mitende mikononi. Bassi na katika Metz mfalme yule mbaya anakwenda kanisani na wakubwa wengi naye, wote wamepanda frasi, wanapita taratibu njiani hatta wakafika kwenyi gereza. Mfalme alipoiona gereza, akawaambia wakubwa wale, "Hatta nataka mimi yule askafu angewapo hapo naswi. Labuda nalimkasirikia mno, naye nia zake njema. Lakini kumwacha, asitubu kwanza na kuniombea masamehe, ndio aibu kwangu mimi. Sikuwezi." Mkubwa mmoja akamwambia, "Aibu kuu kweli kweli. Ata-

Digitized by Google

tubu kwanza. Hatta na akikusihi kwa unenyekevu sana, hakufai kumwacha upesi." Mfalme akamwuliza mkubwa mwingine, akinena, "Waonaje wewe? Si mazuri maneno yangu?" Yule mkubwa akasema, "Si mazuri hatta kidogo, Ee mfalme. Ukingoja mpaka yeye atakapokutakia masamehe, utaonekana ukitaka masamehe mwenyewe." Mfalme akaona uchungu, akamwambia, "Maana yako nini?" Akamwambia, "Siku ile mtakaposimama wote wawili pamoja, wewe na askafu, mbele ya kiti chake aliye Muamuzi wenu, yupi atakayetaka masamehe?" Mfalme akazidi kukasirika, akanena, "Usipokuwa umenitumikia vema mbele, ungelia wewe, lakini sasa, —Ah! nini hii?" Wakasimama wote wakasikia uimbo mzuri unaimbiwa juu kwa sauti yenyi huzuni na kushangilia pia, wakanyamaa kimya, wakasikia maneno yake haya,

Upewe utukufu,
  Mfalme Mkomboa,
Watoto wa zamani
  Waliyekuimbia.
Mfalme mbarikiwa,
  Mzao wa Daudi,
Ujaye kumiliki
  Kwa jina la Yahuwa
    Upewe utukufu,
      Mfalme, Mkomboa,
    Watoto wa zamani
      Waliyekuimbia.

Jamii ya malaika
  Wakusifuo juu,
Na watu na viumbe
  Vyajibu chini vyote.
    Upewe utukufu,
      Mfalme, Mkomboa,
    Watoto wa zamani
      Waliyekuimbia.

Digitized by Google

Watu Waebrania
Waliotangulia,
Kusifu na kuomba
Kutangulia leo.
Upewe utukufu,
Mfalme, Mkomboa,
Watoto wa zamani
Waliyekuimbia.

Kusifu wakaimba
Ulipokwenda kufa,
Ukiwa juu ya yote
Twaimba kwa furaha.
Upewe utukufu,
Mfalme, Mkomboa,
Watoto wa zamani
Waliyekuimbia.

Umekubali wale,
Utukubali sisi,
Mfalme wa neema,
Mpenda mema wee.
Upewe utukufu,
Mfalme, Mkomboa,
Watoto wa zamani
Waliyekuimbia.

Uimbo ulipokoma, mkubwa mmoja akasema, "Sauti ya Malaika hii." Mwenziwe akasema, "Kuimba kule kuzuri kweli kweli." Mfalme akawaambia, "Nathani umetoka gerezani." Wakatazama juu kwa ngome, napo penyi dirisha jembamba na lenyi vyuma askafu yule akaonekana, anawatazama watu chini wakienda kanisani kwa furaha, anaimba vizuri. Mfalme akaingia majuto, akanena, "Nimekosa kwa namna ya Herode, ntatubu kwa namna ya Petro." Akatuma mjumbe kwenda kumwita askafu. Askafu akafunguliwa akaja, asijue atakuwaje. Akiwa katika kutoka mlangoni kwa gereza, mfalme akashuka katika frasi akampigia magote, akamwambia, "Ee baba mwema, unisamehe, uniombee kwa

Digitized by Google

Muungu. Nimekosa, nataka nafasi ya kutubia." Askafu akamwinua, akanena, "Utapewa, mwanangu. Muungu hakosi kukujalia ugeuke katika mabaya." Mfalme akamwambia, "Bassi twende kanisani, uniombee kwa Muungu." Wakaenda.

## WENSESLAO, MFALME WA BOHEMIA.

PALIKUWA na mfalme wa Bohemia, penyi inchi ya Germania, jina lake Wenseslao, na huko wakati wa baridi nyingi, theluji pote, maji yameganda, inchi imekauka ngumu, hapana kulima, hapana kutembea, hukaa nyumbani tu, hushinda kwa njaa na baridi kali.

Akawa mfalme yule anaketi katika jumba lake, akapenyesha jicho kwa dirisha akaona mtu maskini mwenyi nguo mbovumbovu anatafuta majani na fito katika magugu. Mfalme akamwita mtumishi wake, akamwambia, "Tazama maskini yule kule kwenyi magugu. Nenda kapata habari yake, yu nani, akaapi, afanyaje, nipate kujua." Mtumishi akatoka akaenda zake. Baridi ikazidi kuwa kali kupita zote. Halafu akarudi akampasha mfalme habari, "Mtu yule, jina lake Rudolfo, mchunga nguruwe, hukaa kando la mto kule. Hana moto, hana chakula, anatafuta fito za kukoka moto, yeye na jamaa yake wasife kwa baridi. Na baridi leo kali sana kweli kweli." Mfalme akamwambia, "Tumekosa sisi, tusipomtunza vema yule maskini. Bassi nenda kalete chakula, uje pale pakuwekea kuni. Nitakuwapo mimi." Mtumishi akasangaa, akamwambia, "Hatta wewe watoka usiku huu, bwana?" Akamwambia,

Digitized by Google

"Natoka, nakwenda mtoni, na wewe ufuatane nami." Akamwambia, "Ee bwana, usitoke, utume watu, baridi nyingi leo, na mbali kufika mtoni." Akajibu, "Nakwenda lakini, nawe uende usiende, upendavyo." Akamwambia, "Ee bwana, hasha! Haifai uende peke yako. Usiende tu." Akanena, "Nakwenda bassi, usiambie mtu hatta neno." Na wakubwa wake wako jumbani wanafanya karamu, wanajipasha moto na kucheza ndani. Naye mfalme akatoka akashika njia, akichukua mzigo wa kuni begani mwake. Mtumishi akamfuata mwenyi vyakula katika mfuko, akamfuata bwana lakini kwa shidda na huzuni, baridi ilivyokuwa kuu inamwumiza sana. Hatta halafu yake moyo karibu ukazimia, hawezi kustahimili tena, akamwambia bwana, "Ee bwana, nimeshindwa, sina nguvu za kuendelea, baridi imenipata." Mfalme akamwambia, "Hatta umesahau alivyosafiri vigumu Bwana wetu akitoka mbinguni kuja hapa duniani?" Mtumishi akanyamaza. Mfalme akanena, "Haya shika njia hivi. Weke miguu yako killa niwekapo yangu, utakwenda rahisi." Yule mtumishi akaangalia sana awekapo miguu yake bwana, akaweka yake yeye pale pale penyi nyayo za bwana wake. Na tazama, marra akaona miguu inapata moto, akapona asiangalie tena baridi wala pepo. Wakaenda zao.

## MELKIOR KASISI.

Liwali wa Goa, ndio mji mkubwa wa Wagoa katika Hindi, alikuwa katika safari anarudi mjini na asikari kama mia, na wakubwa wake, na kasisi mmoja aliyesafiri nao, jina lake Melkior. Yule liwali aka-

Digitized by Google

chukuliwa na watu wa'nne kwa machela, wakubwa wamepanda frasi, asikari waenda kwa miguu, na kasisi yule anashika njia kwa miguu, akithani, "Si mimi asikari wa Masiya? Bassi niende vile vile na asikari hao." Wakafika hatta palipo pembemba, bahari huko na msitu huko, killa mtu akajifanya tayari kwa kupigana, kwa maana watu wa inchi ile hawakupenda Wagoa, huwaotea, hupigana nao, huwachinja. Walipokuwa karibu na kwisha pita pabaya pale, mtu Mhindi akawatokea, akamsalimia liwali, akamwuza kama yupo kasisi nao. Yule kasisi akamwambia, "Mimi hapa kasisi, mwanangu. Wataka nini?" Akamwambia, "Ee Baba, mtoto mmoja wangu ameugua sana na karibu kufa, naye bado kubatizwa. Bassi, baba, nakuomba sana uje umbatize." Kasisi akamwambia, "Ntakwenda, mwanangu." Akamwambia liwali, "Nitarudi, bwana, usiku kwa matuo." Liwali akamwambia, "Ee baba, naona hila hii. Nami siwezi kutuma asikari wafuatane nawe, sababu watu wachache." Akamwambia, "Ee bwana, sina hofu kwenda peke yangu. Hatta nikiwa na hofu, sina buddi kutenda kazi hii." Liwali akawauliza watu wake kama wamjua Mhindi yule. Mmoja akasema, "Namjua, jina lake Andrea." Liwali akawa rathi, akamwambia kasisi, "Bassi, baba, tutakungojea matuoni usiku." Kasisi na Mhindi wakaenda zao. Ikawa kuchwa, giza ikazidi, wakapita katika mwitu mkubwa na mnene, wakijizumgumza njiani. Hatta yule kasisi akajaliwa kuona katika nafsi yake ya kwamba, kama mchana unakwisha, vile vile na maisha yake inakaribu kwisha. Asijue mwenyewe apataje kuiona habari, aliona tu. Akanyamaza, akafikiri ulimwengu. Hatta halafu yake wakatokea katika shamba, Mhindi akamwambia, "Nyumba yangu ilee." Na nyumba ile nzuri, yenyi ua, na bustanini migomba na jamii ya ma-

boga. Kasisi akamsifu Muungu kwa maana ya kumwonya mbele habari ya kufa kwake, akaingia nyumbani. Mkewe Mhindi yumo analeta mtoto, na mtoto hawezi sana lakini hayi bado. Akambatiza. Akaagana na Mhindi na mkewe, akisema, "Naenda zangu upesi, nisipatwe na mabaya njiani." Mhindi akamwambia, "Ntakuonyesha njia ya kukata kwa matuo, nawe, baba, hukosi kupewa thawabu kuu kwa kazi hii njema." Wakaenda, wakashika njia mwituni wakafika hatta peupe, msitu ulipofiekwa. Marra kelele kubwa, watu wathenashara wakawarukia vichakani, wakawakamata wote wawili. Wakamwambia Mhindi, "Nenda wee." Hakubali. Kasisi akamwambia, "Nenda, mwanangu. Ukikaa, wafaa nini? Usijipoteze roho yako burre." Yule Mhindi akapiga magote akawaomba watu wale wamwache kasisi, akawapa habari ya kazi ile njema aliyoifanya. Asijibiwe neno illa kuondoka tu, kwenda zake. Hatta wangine wakampindia pindi, kasisi akamwambia, "Nenda, mwanangu, nenda bassi." Akaenda kwa shidda na majuto mengi.

Mtu aliye mkubwa wao akamwambia kasisi, "Wewe Mmasihiya?" "Ndio." "Na kasisi?" "Na'am." Yule mkubwa akamwambia mwenziwe, "Lete msalaba." Akaleta msalaba, umefanyika na fito mbili zilizofungwa na kamba katikati. Mkubwa akautupa msalaba chini, akamwambia kasisi, "Mambo mawili, ao kukanyaga msalaba ao kupigwa mishale. Chague bassi." Kasisi akanena, "Nimekwisha chagua." Mkubwa akawaamuru watu wake, wakajipanga kwa safu, killa mtu na upindi wake na mishale. Akamwambia kasisi, "Tutakupa nafasi ya kutubia. Haya, piga mmoja." Mtu mmoja akavuta upindi, akapiga, mshale akampenya kasisi mkono. Yule kasisi akasema, "Kwa mikono yako, Ee Bwana, naweka roho yangu. Ndiwe uliyeni-

Digitized by Google

komboa, Ee Bwana, Muungu wa kweli." Mkubwa akasema, "Piga tena mmoja." Mtu wa pili akapiga, na wa tatu akapiga, na wa 'nne akapiga vile vile, wote wakiangalia sana wasimchome mahali pa kumfisha roho. Ndilo shauri lao, kumtesa sana kwanza. Naye akatulia kimya, hasemi neno illa moyoni mwake ndani, "Ee Baba, uwasamehe, hawajui wafanyaje." Ndipo akainama chini, akashika msalaba, akaubusu. Mtu anayepiga mshale kwa zamu yake dakika ile ile akakosa shababa, mshale ukamchoma moyo. Akafa.

## WAVUVI:

KIKO kisiwa karibu na Uingereza, chenyi mji unakwitwa Pili, na mji ule mji wa wavuvi wengi. Bassi siku moja wavuvi wakawa wakitengeneza mashua na majarifa kwa kwenda kutega samaki. Penyi bandari pamejaa watu, waume na wake na watoto, wote wanatenda kazi, hupakia mashuani chakula na vinywa na tumbako na vyombo, huleta mapipa pwani tayari kwa kuwekea samaki na chumvi tele wasioze, sababu wakati wa kuvua umewadia; wasipotega samaki chungu chungu, watu wa mji hawakosi kushinda kwa njaa siku nyingi.

Halafu yake kengele kubwa ya kanisa lililoko ikapigwa marra moja, marra mbili. Wote wakaharaka kutia mashua baharini, kupanda wenyewe, wakangoja. Kengele ikalia marra ya tatu, akatoka kasisi katika kanisa amevaa nguo za dini, akashuka kule pwani. Waanaume wakasimama katika mashua, wamevua kofia vitwani, waanake wakapiga magote pwani, yule kasisi akawabariki watu na

Digitized by Google

mashua na vyombo vyote, wapate safari njema, na samaki wengi, na kurejea salamu na furaha, kwa jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu. Alipokwisha kusomesha, wote wakapiga kelele, "Kuaherini," wakavuta makasia, wakatweka matanga, wakaenda zao, bandari ikatulia pasipo watu.

Bassi na katika mashua moja wamo watu watatu, Mikael na nduguye Patriki, na rafiki yake Yohanna, wakaenda mbali, wakatupa jarifa, wakangoja usiku. Ilipopambazuka assubui, wakala wakaona, wamechukuliwa mbali na mkondo wa maji, na 'pepo zinageukageuka kama kwa tanga mbili, wakasema, "Haya tuvute jarifa twende zetu. Samaki wengi safari hii." Marra likiwa shindo kuu, wakaangushwa chini mashuani, wakasema, "Nini hii?" Mmoja akalia, "Mwamba, mwamba huo. Inavuja sana. Haya, vuteni maji, upesi nanyi." Wakavutavuta kwa juhudi. Wakawa mbali kidogo baharini, pepo zinavuma zinawazuia wasifike pwani upesi. Mikael akawaambia wenziwe, "Tutupie mbali jarifa, tuliache kabisa, tuzidi kwenda mbio." Yohanna akamwambia, "Hatta haithuru. Dakiki kumi bassi, tutazama. Tukate mlingote afathali, tuwe na dude la kutuogeleza." Patriki akanena, "Lakini tutachukuliwa huko na huko baharini." Wakamjibu, "Kweli kweli." Mikael akawaambia, "Muungu awezaye kutuokoa. Tumwombee." Wakavua kofia (watu wote wa inchi zenyi baridi huvaa kofia siku zote), wakaomba sana. wasiache kazi ya kuvuta maji" Walipokwisha, Mikael akawaambia, "Haya, tukate mlingote." Ndipo Patriki akalia, "Tumepona, enyi. Haivuji tena, haivuji tena." Wakatoa maji kidogo, maji hayaingii sasa. Yohanna akasema, "Mwujiza huo." Wakapiga magote, wakambariki Muungu. Wakavuta jarifa, wakateka jamii ya samaki wengi, mashua ikajaa. Wakasema, "Twende zetu banda-

Digitized by Google

rini. Wakaenda na 'pepo nzuri. Walipofika, wakapandisha mashua pwani, wakaona ajabu kuu. Mwamba ule umevunja sana mashua chini, akatoboa tundu kubwa. Bassi na samaki mkubwa akifukuza wadogo katika jarifa kwa nguvu amekwama tunduni mle, akajikaza sana, hawezi kuendelea wala mbele wala nyuma. Ndio iliyoziba tundu, maji yasivuje. Juma ya pili wavuvi wale wakaenda kanisani, wakamtolea Muungu mashukuru katika dini mbele ya watu wote.

## BUIBUI.

Uko mwitu katika Germania, mwitu mkubwa na mnene. Palikuwa na mtu mmoja, naye mcha Muungu sana, akakaa kule mwituni, akafanyiza kibanda, ndicho kanisa lake. Killa siku kuu apiga kengele, watu walioko mwituni waja kusali na kumwabudu Muungu. Na mtu yule kasisi, na nyumba yake ndio paango lenyi mlango mwembamba sana. Watu wengi huja kwake kumtaka shauri, kwa mambo yao, na dawa ya marathi.

Walikuwako tena mwituni mle watu wabaya, wanyang'anya na haramia, huchinja hatta watu, huteka nyumba. Na mkubwa wao jina lake Emeriko. Bassi siku moja Emeriko akaingia katika kanisa la kasisi, yule kasisi akamkataza kwa jina la Muungu, akisema, "Utoke, usizidishe thambi zako, utubu kwanza, urudishe marra 'nne uliyoyaiba, ukaungame, upate kusamehewa. Ndipo nitakukaribisha hapo." Yule mtu akamwambia, "Bassi nakwenda zangu, na wewe utalia nawe." Akaenda. Watu wengi wakamwomba yule kasisi akimbie aji-

Digitized by Google

fiche kwao, mmoja akasema, "Yule Emeriko mbaya sana, nalimwona alibusu upanga wake akitoka, ndio kiapo chake. Hakosi kufanya alivyoapa." "Ee baba, njoo kwangu, viko tena vichaka karibu, pazuri pa kujifichia mtu." Na mwingine, "Hatta kwangu pia kule ziwani utakaa salamu kabisa." Yule kasisi hakukubali, akawaambia, "Ahsante sana, waanangu, nami sikimbii, nipo hapa nilipowekwa na Muungu. Yeye awezaye kuniponya. Daudi amesema, "Kwamba jeshi lingekaa juu yangu, moyo wangu haungeogopa. Kwamba vita ingeniondokea, hatta hivi ningetumaini." Wakamtaka sana, asikubali, "Mimi kasisi, siwezi kuacha kazi yangu. Nanyi nendeni killa mtu." Wakaenda zao.

Siku ile ile jioni yule kasisi amekaa kitako karibu na paango, na mtoto mmoja mwanafunzi wake, aliyekaa pamoja naye siku zote. Wakatazama jua linakuchwa kwa uzuri mwingi. Yule mtoto akaona hofu akisema, "Ee baba, mbona hukimbii. Labuda sisi hapa tutakukosa kabisa. Naswi tutakuwaje tena?" Akajibu, "Ee mwanangu, tazama jua. Hatta na jua halifanani na fakhari Muungu aliyowatengenezea wao wampendao kwa kweli. Wafao kwa ajili yake Bwana wetu, kufa gani kule? Siko kushinda, kuingia peponi, kuokoka bassi?" Marra mtu akawatokea akija mbio katika mwitu, analia, "Ee baba, kuna rathi. Njoo upesi. Yule mbaya anakuja sasa hivi, na watu watano pamoja naye. Twende, hatta sasa waweza kupona." Mzee akamwambia mwanafunzi, "Nenda, mwanangu, ukajifiche. Imani kwako haba." Akajibu, "Sivyo, baba, nife nawe tu." Akamwambia yule mtu aliyemjia, "Siiachi kazi yangu. Kuaheri." Yule mtu akaenda zake.

Kasisi na mwanafunzi wake wakaingia paangoni, wakangoja. Marra wakiisha kuingia, buibui aka-

Digitized by Google

tokea juu ya mlango wa paango, akakimbia huko na huko kwa haraka sana, akitenda kazi kwa miguu, akafunga uzi wake pande zote za mlango, hatta marra moja amekwisha kufanyiza wavu katika mlango ule. Bassi ndipo wabaya wale wakafika pale pale, wakisema, "Tumefika. Yule kasisi atalia naye kweli kweli. Haya, tumkamate." Wakakaribia paangoni. Wakalia kwa msangao, "Tazama, hatta hamo mwenyewe. Wavu wa buibui!" Mwingine akasema, "Hayuko kweli kweli, wala leo wala jana wala juzi, naona. Lakini mwenzetu alileta habari amemwona leo yupo." Emeriko akasema, "Mwongo yule. Hayuko leo. Twende tumtafute kanisani." Wakamtafuta wasimpate. Wakaenda zao. Wale wakatoka paangoni, mzee akamwonyesha mtoto wavu, akamwambia. "Tazama, mwanangu, mwenyi malaika elfu elfu ametuponya kwa dudu hili moja dogo dogo."

## ABDALLAH NA SABAT.

Abdallah na Sabat walikuwa vijana wa jamaa bora katika Arabuni. Wakasharikiana sana, hatta wakapatana kusafiri pamoja kutazama inchi ngeni. Wote walikuwa wataowa wa Islamu. Wakafika hatta kwa Kabul, ndio mji mkuu wa Afganistán, Abdallah akafanywa karani katika Kabul. Sabat akamwacha hapo, akaenda zake hatta Tartari. Abdallah alipokuwa akikaa katika Kabul, akasoma kwa nasibu ya Muungu Maandiko Matakatifu, nao mali ya Mmasihiya Mwarmeni, hivyo akaongoka kwa imani yake Masiya. Bassi na katika inchi za Islamu ni mauti ye yote wa jamaa bora kuwa Mma-

Digitized by Google

sihiya. Abdallah akaona haiwezikani kustiri ongozo lake, akayakinia kukimbia kwa makanisa ya Wamasihiya yaliyoko karibu ya bahari Kaspiano. Akaondoka akaacha Kabul kwa kujigeuza, akafika mji ule mkubwa. Bokara katika Tartari. Akamkuta katika mitaa ya mji ule rafiki yake Sabat, na Sabat amesikia habari ya kuongoka kwake, akamtambua. Abdallah akajua shidda yake akajitupa miguuni pa Sabat, akaungama amekuwa Mmasihiya, akamsihi kwa urafiki wao wa kwanza, amsamehe. "Wallakini, Bwana," alisema Sabat, akiwa akieleza mambo haya baadaye, "sikumhurumia. Nikawatuma watumwa wangu kumkamata hamtoa kwa Marad, mfalme wa Bokara. Akahukumiwa kufa, muethini akatoka akaenda kati ya mji akitangaza saa ya kufa. Nami saa ikiisha nikaenda karibu ya Abdallah. Akaambiwa ataponya roho yake akimkana Isa Masiya, na asikari anasimama papo hapo na upanga katika mkono wake. Akanena, 'Hakuna, siwezi kumkana Masiya.' Marra akakatwa mkono mmoja katika kitango. Akasimama imara, na mkono wake chini. Mtabibu, aliyetumika na mfalme, akamwambia atamponya jeraha yake akiitharau imani ya Masiya. Hakujibu neno, akatazama juu, na macho yake yakitoka machozi. Tena akanitazama mimi, lakini si kwa hasira, mwenyi umbo la kusamehe. Na mkono wake wa pili ukakatika tena. Lakini, Bwana," alisema yule Sabat, si kwa kiingereza safi, hajaijua bado, "habadiliki, habadiliki. Alipoinama kitwa chake kutoa roho. Wabokara wote wakasema, 'Ajabu hiyo kweli kweli.'" Sabat akawa ametumaini kama Abdallah angebadilika alipopata nafasi ya kujiokoa. Lakini alipoona kama rafiki yake amekwisha kufa akashikwa na huzuni na msiba. Akasafirisafiri kutafuta raha asiipate. Hatta mwisho alinia kama atakwenda kutazama Hindi. Akaja kwa Madrás.

Digitized by Google

Elimu yake na daraja ya ujamaa wake katika inchi yake ukamstahilia kuwa mwalimu. Alipokuwa katika Vizingapatam, akitenda kazi yake ya mwalimu, akajaliwa kukuta msahafu wa Agano Jipya umeandikwa kwa lugha ya kiarabu. Akausoma akaufikiria sana, na Kuran kando yake. Akasoma zote pamoja kwa saburi na taratibu. Hatima kweli ya Anjili ikaanguka katika nia yake, kama gharika ya nuru, ndivyo alivyonena mwenyewe. Baadaye akaenda Madrás kutafuta ubatizo. Alipoungama kwa wazi imani yake, akabatizwa katika kanisa la Waingereza, jina lake alilopewa Nathaniel, naye mwenyi umri miaka saba asharini. Waliposikia jamaa katika Arabuni kama amekuwa Mmasihiya, walituma nduguze kwa Hindi, safari ya miezi miwili, kumvizia wamwue. Sabat akawa akiketi nyumbani mwake katika Vizingapatam, nduguye akamtokea kwa werevu kama fukara, mwenyi shembea imefichwa nguoni mwake. Akamrukia Sabat akamjeruhi, na Sabat akamshika mkono na mtumwa akaja kumsayidia. Marra akamtambua nduguye, na yule mwuaji angaliuawa kwa sheria ya Hindi, na Sabat akamtetea asiuawe, akampeleka kwake kwa amani na nyaraka na zawadi pia kwa nyumba ya mamaye katika Arabuni.

## MSAFIRI.

Nikiwa nikitembea katika jangwa, ndio dunia hii, nikakuta palipo mahali pa ndani, nikajilaza huku nipate usingizi. Hatta nikilala, nikaota ndoto, na habari za ndoto ile ndizo hizi.

Digitized by Google

1.

Palikuwa na mtu, amevaa nguo mbovumbovu, anasimama mahali, ameacha nyuma nyumba yake, mwenyi msahafu mkononi, na maongoni mzigo mzito. Akaufungua msahafu akasoma, naye akisoma, akalia akatetemeka, wala hakuweza kujizuia, akapiga kelele la huzuni nyingi, akinena, "Nifanyeje?"

Bassi akiwa hali hiyo, akarejea kwake akajinyamazisha kama awezavyo, mkewe na watoto wake wasipate kuiona huzuni yake, lakini hakuweza kunyamaza sana kwa sababu ya kuzidi taabu yake. Hatima akafunua moyo wake kwa mkewe na watoto wake akaanza kusema nao hivi, "Ee mke wangu mpenzi, nanyi watoto wa moyo wangu, mimi rafiki yenu mnipendao nimepotea kwa ndani kwa maana ya mzigo mzito unaonilemea. Tena nimepewa habari yakini ya kwamba mji huu utateketea kwa moto wa mbinguni, nao ukipatwa na msiba mkubwa huo, na mimi na wewe mke wangu, na ninyi watoto wangu niwapendao tutapotea vibaya, isipoonekana njia ya kuokoka, nami siioni tupate kupona." Jamaa zake wakastaajabu sana maneno yake, si kwa sababu wamesadiki aliyowaambia ndiyo kweli, illa kwa sababu wamethani ameshikwa kitwani na ugonjwa wa wazimo. Bassi usiku ukiwa karibu nao wakitaraja ya kuwa usingizi utamtuliza kitwa, wakamlaza kitandani kwa haraka yote. Illakini usiku wake umejaa taabu kama mchana, kwa hiyo hakupata usingizi akashinda katika kuugua na machozi. Hatta ukiwa ussubui wakataka kumjua hali yake, akawaambia, "Imezidi kuwa mbaya," akaanza kusema nao tena, lakini wao wakaanza kuwa wagumu, wakathani kufukuza ugonjwa wake kwa kumtendea magumu na makali,

Digitized by Google

marra humcheka, marra humkemea, marra humwacha kabisa, naye akajitenga kidogo chumbani kwake, kwa kusudi awaombee akawahurumie, na kwa kukumbuka shidda yake yeye, hutembea tena peke yake mashambani marra kusoma marra kuomba. Hivi siku zikapita.

Bassi nikaona katika ndoto marra moja alipokuwa akitembea mashambani, akawa kwa desturi yake akisoma katika msahafu wake akaona shidda nyingi nafsini mwake, naye akisoma akapiga kelele kama kwanza, akilia, "Nifanyeje nipate kuokoka?" Akawa anatazama huko na huko, kama angetaka kukimbia, illakini akasimama kwa sababu (kama nilivyoona) hajui njia ya kuendea. Halafu yake mtu akamjia, jina lake Mwanjilisti, akamwuliza, "Walilia nini?" Akasema, "Ee Bwana, naona kwa msahafu huu hapa mkononi mwangu ya kuwa nimehukumiwa kufa, na baadaye kuja katika hukumu, nami nimeona sitaki ya kwanza, na ya pili siwezi." Mwanjilisti akasema, "Mbona hutaki kufa, maisha hii ikifuatana na mabaya mengi kama haya?" Akasema, "Kwa sababu naogopa mzigo huu ulio maongoni mwangu, utanizamisha chini ya kaburi, nami nitatumbukia jehannum. Tena, Bwana, nisipo tayari kwenda gerezani, simi tayari kwenda kwa hukumu, baadaye kuuawa. Bassi mawazo hayo ndiyo yanilizayo." Mwanjilisti akasema, "Ukiwa hali hiyo, mbona umesimama?" Akajibu, "Kwa maana sijui niende wapi." Yule akampa khati ya ngozi iliyoandikiwa ndani, "Uikimbilie ghathabu ijayo." Akasoma akamtazama sana Mwanjilisti akanena, "Nikimbie wapi?" Mwanjilisti akamwonyesha koonde pana sana, akanyosha mkono akamwambia, "Waona mlango ule mdogo?" Akanena mwenzake. "Siuoni." Akamwambia, "Bassi waona mwanga ule ungaao?" Akamwambia, "Na-

Digitized by Google

thani nauona kidogo." Akamwambia, "Shika mwanga ule jichoni, ukaenda huko kwa kunyoka, hivi utauona mlango. Ukibisha kule, utaambiwa yanayokupasa." Naye marra akaanza kwenda mbio, wala hajafika mbali sana katika nyumba yake, mkewe na watoto wake wakamwona, wakampigia kelele, " Rudi, rudi." Naye akajitia vidole masikioni, akaendelea mbio, akilia, " Uzima wa milele!" asitazame nyuma. Tena jirani wake wakatoka wamwone anakimbia. Naye akikimbia, wangine wakamthihaki, wangine wakamwogofya, wangine wakampigia kelele, arudi. Na kati yao waliotenda hivi, wawili wakashika kumleta tena kwa nguvu, jina lake wa kwanza Mkaidi, jina lake wa pili Mgeushi. Naye sasa amekwisha kwendea mbali punde, wale wameshika kumfuata, wakaenda, hatta halafu yake wakamfikia. Akanena, " Enyi jirani, kwa nini mmekuja ?" Wakamwambia, "Tukushawishi urudi pamoja naswi." Akanena, " Haiyamkini. Mnakaa katika mji Uharibifu, mahali nilipozaliwa mimi, naona ndio kweli. Mkifa humo, hamkosi mwanzo hatta mwisho kuzama chini kuliko kaburi, mahali pawakapo moto na kiberiti. Kuna rathi, jirani wema, mfuatane nami."

Mkaidi akamwambia, "Je? Tuache nyuma rafiki na raha zetu?" "Ndivyo" akasema Mmasihiya, ndilo jina lake mtu yule aliyekimbia, " Sababu yote hayo mtakayoyaacha hayalinganikani na kidogo chao ninayotaka kupata. Mkifuatana nami, msilegee, mtakuwa hali ileile na mimi. Huko niendako, yako ya kutosha na kusaza tena. Haya, twende zetu, kashuhudieni maneno yangu."

Mkaidi. "Mambo gani uyatafutayo, kwa maana yao unauacha ulimwengu pia?"

Mmasihiya. "Natafuta urithi usioharibika, usiotiwa uchafu, usiokauka, umewekwa mbinguni salama. Wautafutao sana, watapewa kwa muhulla

Digitized by Google

wake. Soma tu, ukipenda mwenyewe, katika msahafu wangu."

Mkaidi. "Tupie mbali msahafu huo. Utarudi nami ama sivyo?"

Mmasihiya. "Sirudi mimi, nimetia mkono katika kulima."

Mkaidi. "Njoo bassi, Mgeushi wee, turudi sisi, tumwache, twende zetu. Kuna jamii yao wajisifuo wasio na akili, wakishika neno kwa mkia wake, wana hekima machoni pao wenyewe kuliko watu saba wajuao kujibu sababu."

Mgeushi. "Usitukane. Yakiwa kweli ayanenayo Mmasihiya huyo mwema, ataka mambo mema kupita yetu sisi. Moyo wangu unapenda kwenda naye."

Mkaidi. "Ewe, wapumbafu wengi siku hizi! Nisikie mimi karudi. Hujui kuwapi atakapokuleta mtu huyu mwenyi wazimo. Rudi bassi, rudi. Huna akili?"

Mmasihiya. "Sivyo. Uje nawe pamoja na mimi, Ee Mgeushi, ndiyo kupatikana niliyoyanena, na mangine mengi matukufu tena. Usiponisadiki mimi, soma katika msahafu huu. Kwa kuwa kweli habari yake, tazama, yote imefanyika imara kwa damu yake yeye aliyeuandika."

Mgeushi. "Bassi, Mkaidi, naanza kuona mwisho. Napenda kufuatana na mtu mwema huyu, na kusharikiana naye. Wallakini, rafiki wee, wajua njia ya kufika mahali pale pa kutamanika?"

Mmasihiya. "Naliagizwa na mtu jina lake Mwanjilisti, niende hima hatta mlango mdogo ulioko mbele yetu, huko tutapewa shauri kwa njia."

Mgeushi. "Haya, rafiki mwema, twende zetu."

Mkaidi. "Nami pia nakwenda zangu. Sitaki kuwa mwenzio waliopotea hivi pasipo akili."

Alipokwisha kwenda zake, na wakaenda wakijizumgumza njiani wakaanza maneno hivi,

Digitized by Google

Mmashihiya. "Haya, jirani Mgeushi, u hali gani? nimefurahiwa umekubali kufuatana nami. Hatta Mkaidi mwenyewe kama angaliona kama nilivyoona mimi nguvu na hofu zao yasiyoonekana, hangalikuwa mwepesi kugeuka nyuma."

Mgeushi. "Bassi, rafiki wangu, sisi hapa sote wawili tu, niambie tena mambo gani hayo, tutapataje fayida mahali pale tunapokwenda."

Mmasihiya. "Nayaona kwa nia yangu, lakini kuyanena kwa ulimi ah! siwezi kabisa. Ukitaka kuyajua, nitasoma katika msahafu wangu."

Mgeushi. "Waona maneno ya msahafu ndiyo kweli?"

Mmasihiya. "Najua sana. Umeandikwa na Yeye, asiyeweza kusema uwongo."

Mgeushi. "Njema. Mambo gani bassi?"

Mmasihiya. "Kunako ufalme wa kukalia usiokoma, tena twapewa uzima wa milele, tupate kukaa huko siku zote."

Mgeushi. "Njema. Na tena?"

Mmasihiya. "Ziko taji za utukufu tayari, na mavazi yenyi kutung'aalisha kama jua katika anga ya mbinguni."

Mgeushi. "Mazuri hayo. Na tena?"

Mmasihiya. "Hapana kulia wala huzuni. Mwenyewe atatufutia machozi yote machoni mwetu."

Mgeushi. "Na wenzetu wa huko je?"

Mmasihiya. "Wenzetu wa huko ndio Maserafi na Makerubi, viumbe vyenyi kutufanyia kiwi machoni tukiwatazamia. Nako utakutana na watu elfu elfu kumi, waliotangulia kufika mahali pale; hakuna aumaye, wote wanaopendana na watakatifu, wakitembea killa mtu mbele ya uso wake Muungu, wakisimama alipo Yeye kwa ukubali hatta milele. Kwa neno moja, tutawaona huko wazee wenyi taji za thahabu, tutawaona bikira watakatifu wenyi vinubi

Digitized by Google

vya thahabu, tutaona watu waliokatwa vipande vipande kwa dunia hii, wakateketea motoni, wakaliwa na nyama za mwitu, wakazamishwa baharini, kwa ajili ya kumpenda sana Mwenyiezi yule,—wazima wote, wamevaa yasiyoharibika."

Mgeushi. "Maneno haya ya kushinda roho. Lakini yanapatikana mambo haya? Tupateje kuyashariki?"

Mmasihiya. "Bwana yule Mwenyiezi ameandika shauri katika msahafu huu. Kusema kwa maneno haba, ndilo hili,—tukiyataka kwa sana, tutapewa burre."

Mgeushi. "Ee rafiki, habari hizi zimenifurahisha moyo. Haya twende upesi."

Mmasihiya. "Ah! Siwezi mimi kwenda upesi upesi kwa maana ya mzigo maongoni."

Wakaendea mbele.

2.

Wakafika hatta kwa ziwa moja lenyi matopetope mengi na kifusi na takataka zilizotangamana na maji. Likawako kati ya uwanda wanaokwenda, likaenea mbali huko na huko, wala hakuna kupita njia ile illa kwa kulivuka ziwa tu. Hatta zamani mfalme wa inchi akatuma watu marra nyingi wakajaribu kupaponya pabaya pale, wakatenda kazi kwa bidii wakatia mawe yasiyo na kiasi na udongo tele, pasizibiwe, hapapati hajambo. Wakafanyiza madaraja ya kuvukia, wallakini wakati wa musika ziwa likazidi kuchafukachafuka na kutapika taka zake, hatta madaraja yale yakazamia mbali. Bassi mahali pale pabovu sana. Pakaitwa Papotelea, ndilo jina lake.

Watu wale wawili wakakaribu nao, wala hawakutunza akili vema, marra wakatumbukia. Wakashinda wakifingirika matopeni, nguo zao zikapata

Digitized by Google

taka nyingi, hatta na yule Mmasihiya amelemewa na mzigo wake akawa anazama pia. Mgeushi akamwambia, "Ee Mmashiya, umefikapi safari hii?" Akamwambia, "Hatta sijui mwenyewe." Mgeushi akachukizwa akafanya hasira, akamwambia mwenziwe, "Raha gani hii nawe? ndiyo hiyo uliyoniambia? Safari yetu kubwa, bassi tukianza hivi vibaya, tutapatani njiani? Nitoke tu salamu, inchi ile nzuri ah! nakuachilia mbali." Akafanya juhudi sana, akatoka matopeni upande wa kwanza akaenda zake, Mmasihiya asimwone tena.

Naye alikuwa anafingirika vile vile peke yake akajitahidi dayima kufika upande wa pili, ndio wa kuendea kwa mlango mdogo. Halafu yake akafika, wala hakuweza kupanda kwa maana ya mzigo. Bassi mtu akamjia, jina lake Msaada, akamwuza, "Wafanyani huko ziwani? Akamwambia, "Ee Bwana, naliambiwa kushika njia hii na mtu jina lake Mwanjilisti, akanionyesha mlango ule, nipate kuokoka katika ghathabu ijayo; nami hashika njia, hatumbukia humo." Akamwambia, "Kwa nini hukutafuta madaraja?" Akanena, "Nalifukuzwa na hofu, hakimbia njia ya kukata, hatumbukia." Akamwambia, "Shika mkono." Akashika akampandisha katika ziwa, akamweka mahali pakavu, akamwongoza njiani.

3.

Akawa anasafiri peke yake, akaona mtu anakuja kumlaki, wakakutana penyi njia panda. Mtu huyu jina lake Mjuvi, hukaa mjini uliokwitwa Ujanja, mji mkubwa sana, nao karibu yake alipotoka Mmasihiya. Na yeye amesikia habari yake Mmasihiya, kwani imeenea sana, akamtambua kama ndiye ginsi alivyolemewa akashika njia kwa kuugua na huzuni. Akamwambia, "Ee rafiki, wendapi nawe mwenyi

Digitized by Google

kulemewa hivi?" Akamwambia, "Kulemewa nimelemewa mimi maskini, na kwendapi, bwana, nakwenda mlangoni kule, nipate kutua mzigo huu mzito."

Mjuvi. "Una mke na watoto?"

Mmasihiya. "Ninao; lakini ginsi nilivyolemewa na mzigo, hakuna kupendezewa nao, hatta najiona kama sinao pia."

Mjuvi. "Nikitoa shauri, wataka nisikia?"

Mmasihiya. "Kama zuri, nataka. Ndilo nitafutalo sana."

Mjuvi. "Bassi shauri langu hili. Ondolee upesi mzigo wako, upate kutulia moyo na kuzitumia vema riziki ulizopewa na Muungu."

Mmasihiya. "Hatta ndiyo ninayotaka mimi, kuondolewa mzigo. Wallakini siwezi mwenyewe, wala hakuna mtu kwetu mwenyi kuuchukua. Bassi ndio ninaokwenda, nipate kuondolewa huu."

Mjuvi. "Nani aliyekuonyesha njia hii?"

Mmasihiya. "Bwana mkubwa na tajiri kama nionavyo, jina lake Mwanjilisti."

Mjuvi. "Shauri lake yeye baya. Ukishika njia hiyo, utalia. Naona nguo zako zimepata taka za ziwa lile Papotelea. Bassi hizi mwanzo tu. Sikilize. Mimi mzee kuliko wee. Katika njia hii unaokwenda, utapatikana na kuchoka, maumivu, njaa, hatari, utupu, upanga, simba, majoka, giza, na kufa pia. Mambo haya ndiyo kweli, watu wengi walioyashuhudia. Bassi kwa nini kujipotezea mbali, kwa kuangalia mtu mgeni?"

Mmasihiya. "Ee Bwana, mambo hayo yote madogo, mzigo mkubwa. Hatta hayathuru ya njiani, nikipata kuufunguliwa mzigo."

Mjuvi. "Ukapatataje mzigo kwanza?"

Mmasihiya. "Kwa kusoma msahafu huu."

Mjuvi. "Ndivyo nilivyothani. Na wangine



Digitized by Google

wengi wajinga wakijishughulisha na mambo makuu, wamepoteza akili hatta na kushindisha nafsi zao kwa hatari nyingi, wapate hawajua nini."

Mmasihiya. "Najua nitakayo mimi, ndio kufunguliwa mzigo wangu."

Mjuvi. "Kufunguliwa gani njia hii nawe? Ukiwa na saburi ya kusikilia, nitakupa shauri la kupata utakayo kwa raha na mustarehe tena."

Mmasihiya. "Ee Bwana, uniambie tu."

Mjuvi. "Tazama, kunakaa katika mji ulee, unakwitwa Adala, mtu mmoja jina lake Mwanasheria, mwenyi sifa njema na kujua sana kuwafungulia watu mizigo kama huu, hatta natambua mwenyewe amefaa sana kwa jambo hili, ameponya wengi waliofathaika akili kwa maana ya mizigo. Nyumba yake si mbali, mwendo wa nussu saa, akiwa hayuko mwenyewe, ana mtoto mzuri, jina lake Adabu, ajuaye kazi hii sawa sawa na yule mzee. Halafu yake utaleta mkeo na watoto wakae humo, nyumba nyingi huko na rahisi kwa kupanga, chakula tele na kipatikanacho upesi, na watu wenyi desturi njema. Bassi utakaa kwa heshima na uzuri."

Maneno haya yakamtatanisha Mmasihiya, halafu yake akanena moyoni mwake, ikiwa huyu amesema kweli, afathali kushika shauri lake. Akamwambia, "Bwana, njia ipi ya kufika nyumbani kwake yule mwema?" Akamwambia, "Waona mlima ule mrefu?" Akamwambia, "Nauona sana." Akamwambia, "Pita njia karibu na mlima ule, marra utafika kwake."

Bassi Mmasihiya akageuka katika njia yake, aende nyumbani kwa Mwanasheria apate msaada. Wallakini akiwa amefika karibu na mlima, aliuona unakwenda juu sana, unatokeza mno upande wa njia anaopita, unafanya mdomo, kama unabomoka, unaanguka. Hatta akaogopa kuendea mbele kwa

Digitized by Google

maana asiangukiwe, akasimama hana shauri. Na mzigo wake ukazidi kumlemea, kuliko alipofunga safari kwanza. Mlima ukatoka moto na umeme, akathani ataunguliwa, akafanya jasho, akitetemeka kwa hofu, akaanza kulilia shauri la Mjuvi. Marra akaona Mwanjilisti anakuja, akafanya haya kwa kumtazama. Naye akamjia moja kwa moja, mwenyi uso wa ukali na uliokunjika. Akamwambia, "Unani hapa nawe, Ee Mmasihiya?" Akanyamaa kimya, hana neno hatta moja. Akanena, "Siwe yeye niliyemwona analia nje ya boma la mji Uharibifu?" Akamwambia, "Ee bwana wangu, ndimi yeye." Akamwambia, "Sikukuongoza njiani kwa kwenda mlangoni kule?" Akanena, "Umeniongoza." Akamwambia, "Bassi ya nini kugeuka hivi upesi? Umetoka njiani." Mmasihiya akampa habari za Mjuvi na shauri lake baya. Mwanjilisti akamwambia, "Simama, nikuonyeshe maneno ya Muungu." Akasimama akitetemeka. Akanena, "Angalieni msimkatae anenaye; kwani hawa wasipookoka waliomkataa aliyetoa wosia katika inchi, zayidi sana sisi tukimgeukia mbali aliye mbinguni. Tena, mwenyi haki ataishi kwa imani, illa atakayerudi, moyo wangu haupendezewi naye. Bassi na wewe uliyegeuka njiani, hatta umetharau shauri lake Aliye juu, ukakaribu kufa kwa milele." Marra Mmasihiya akaanguka chini kama amekufa, akilia, "Ole wangu, mimepotea pia." Mwanjilisti akamshika mkono akamwambia, "Wataachiliwa waana Adamu mathambi yote na manajisi. Usiwe asiyeamini, illa aaminiye." Mmasihiya akapata moyo kidogo akasimama akitetemeka kama kwanza. Mwanjilisti akamwambia hivi, "Angalia, Mjuvi yule anajua mambo mengi, lakini mambo ya dunia hii tu. Bassi utamchukia kabisa kwa sababu (1) ya kwanza, alikugeuza katika njia, na Bwana amenena, 'Fanyeni

Digitized by Google

bidii kuingia mlango mwembamba,' ndio mlango ule mdogo, 'kwani mwembamba ni mlango, na nyembamba njia iletayo kwa uzima, na ndio wachache waionao,' (2) ya pili, alikuchukiza kwa hatari na taabu za njia, na Mfalme amenena, 'Aipendaye nafusi yake ataipoteza. Mtu akija kwangu, asipomchukia babaye na mamaye na mkewe na watoto wake na nduguze na nafusi yake mwenyewe, hawezi kuwa mwanafunzi wangu,'—(3) ya tatu, alikuongoza kwa njia mbaya. Mwanasheria ni mtoto wa suria, naye anatumika na watoto wake. Hafai neno. Tena, kwa matendo ya sheria hapana kufanyiziwa haki mtu wo wote. Tena, walio wa katika matendo ya sheria, wako chini ya laana; kwani imeandikwa, 'Amelaaniwa killa asiyetenda yote yaliyoandikwa katika kitabu cha sheria, ayafanye.'"

Mmasihiya akatubu sana, akamsihi Mwanjilisti, "Nirudi tena, nisamehewe thambi zangu." Akamwambia, "Umekosa sana, lakini yule mngoja mlango mwema na apendaye wote. Atakukaribisha. Kuaheri." Akaenda upesi, akafika hatta kwa mlango.

## KRISTOFER MTAKATIFU.

HADITHI ya Kristofer ndio hii. Palikuwa na mtu katika inchi ya Sham, naye mtu hodari na mrefu sana kwa umbo lake. Akaondoka akaenda zake kwa mfalme mmoja akamtumikia. Hatta siku moja akaja mtu mwenyi kazi yake kuimba nyimbo, akaimba mbele ya mfalme na wakuu wake. Na katika uimbo alimtaja Shetani, naye mfalme aliposikia jina lile baya, akajiandikia alama ya msalaba. Yule

Digitized by Google

mkubwa akamwambia, "Kwa nini kufanya hivi?" Mfalme akajibu, "Nilindwe katika nguvu zake Shetani, kwani namwogopa asinishinde." Akamwambia, "Kama wamwogopa Shetani, yeye mkubwa kuliko wewe. Bassi naenda kumtafuta nimtumikie." Akaenda zake, akasafiri mbali huko na huko, hatta katika nyika kuu akakuta njiani jeshi la watu wenyi selaha za vita, na mkuu wao uso wake mbaya na mkali kama haramia, akamwambia, "Ee mwana Adamu, wendapi?" Akaitikia, "Nakwenda tafuta mfalme Shetani, nataka kumtumikia." Yule mkuu akamwambia, "Kae bassi, ndiye mimi." Akamsujudia, akawa mtumishi wake, akafuatana naye.

Wakafika penyi njia panda, napo msalaba wa mti umewekwa. Na Shetani akikaribia akashikwa na hofu, akatetemeka. Yule mrefu akamwuliza sababu yake, akasema, "Sababu Isa Masiya akafa msalabani, mbele yake natetemeka kwa hofu." Akamwambia, "Huyo Isa Masiya mwenyi enzi kuliko wewe. Bassi ndiye nitakayemtumikia."

Akaenda zake kumtafuta Isa, akawasili katika paango, ndipo alipokaa peke yake mtu mmoja mzee naye mcha Muungu sana, akamtakia mzee amwonyeshe Masiya. Akamwambia, "Masiya ndiye mfalme wa mbingu na inchi. Ukitaka kumtumikia Yeye, huna buddi kufunga na kuomba." Akajibu, "Kufunga siwezi, kuomba sijui." Akamwambia, "Bassi, nenda mtoni mle, kawasayidie wavukao. Maji yanapita kassi." Jambo lile likampendeza mtu sana, akang'oa mnazi mzima, ndio fimbo yake, akakaa kule mchana na usiku, tayari siku zote kuwachukua wasafiri begani kuwavukisha mto.

Akakaa siku nyingi. Hatta usiku mmoja akamtokea mtoto mchanga anasimama ukingoni mwa mto, akilia, "Ewe mshujaa, univukishe mimi." Naye akampandisha juu ya bega lake, akaitwaa

Digitized by Google

fimbo, akaingia mtoni. Maji yakazidi yakajaa sana, ikawa thoruba, na mawimbi makubwa, kitoto yule akazidi kuwa mzito sana hatta kumlemea, mshujaa akaogopa atashindwa na maji. Akapepa-pepa, akalevyalevya, kiisha kwa shidda na juhudi akafika ng'ambo. Akamwambia mtoto, "Nani wewe, Ee mtoto? kama ningalitiwa ulimwengu pia begani, singalikuwa na mzigo mzito kupita wewe." Mtoto akajibu, "Ee mshujaa, umechukua begani Aliyeumba ulimwengu na wewe. Walitaka kunitumikia katika kazi hii njema, bassi tazama nimekukubali." Aka-enda zake asionekane tena. Naye yule mshujaa alijua kama amekubalika, akamsujudia Masiya. Kwa hiyo amekwitwa Kristofer, maana yake, mwenyi kumchukua Masiya.

## MAKARIO MTAKATIFU, NA KITWA.

Siku moja Makario anatembea mahali penyi maka-buri ya kale ya Wamisri, ndipo alipokaa mwenyewe, akaona kitwa cha mayiti, akakipindua kwa mko-ngojo wake, akakiuliza, "Cha nani hiki?" Kikajibu, "Cha mshenzi." "Na roho yake iko wapi?" "Iko katika jehannum." Makario akauliza, "Kwapataje kwenda kwake chini?" Kikajibu, "Kwapita mwe-ndo wa tokea mbingu mpaka inchi." Akauliza tena, "Wako watu tena chini yao?" Kitwa kikajibu, "Wako Wayahadi chini bado." Akauliza, "Hatta na chini yao tena wako?" Kikanena, "Wamasihiya Isa Masiya aliyewakomboa, nao wamejionyesha kwa matendo yao kama wamemsahau kabisa, ndio walio-ko chini sana."

Digitized by Google

## NA TENA?

Palikuwa na kijana, ametiwa chuoni, amesoma sana, amehitimu ilmu pia. Akaondoka akienda mjini kutafata kazi, akakuta njiani mtu mzee akasema naye. Yule mzee akamwambia, "Waenda mjini?" Akanena, "Nakwenda." Akamwambia, "Kwa nini?" Akajibu, "Kutafuta kazi." Akamwambia, "Na tena?" "Tena naona nitapata mshaara mkubwa." "Na tena?" Tena nitaweka akiba, nitafanya mali nyingi." "Na tena?" "Tena nitakuwa tajiri na mngwana." "Na tena?" "Tena nitaoa, nitazaa watoto, nitakuwa na jamaa bora." "Na tena?" "Tena watu wote wataniheshimu, labuda nitakuwa mfalme." "Na tena?" "Tena nitakaa raha na mustarehe, ntakuwa mzee." "Na tena?" "Tena, tena naona ntakufa." "Na tena?" "Na tena, na tena, na tena, Ah!" Akanyamaza yule kijana akaenda zake akafikiri mambo ya Muungu rohoni mwake.

## MKUU KATIKA BARRA.

Palikuwa na mkuu katika barra, hodari na mwenyi mali, na Mzungu akikaa pale pale, naye Mmasihiya mpelekwa. Bassi yule mkuu ameonekana amefanya thambi, hatta akayakinia kwa nafusi yake kama amekosa sana kweli kweli. Akaingia mashaka akaenda kwa yule Mmasihiya akamtolea mshipi wake, na ngozi ndizo mateka yake ya kuwinda, apate kupona katika hofu zake. Mmasihiya akamwambia, "Hakuna, Muungu hakubali sadaka

Digitized by Google

kama hii." Mkuu akaenda zake, marra akarejea, akamtolea bunduki nzuri. Akajibiwa vile vile, "Muungu hazikubali sadaka hizo." Akaenda zake tena, asikae sana. Hana buddi kurudi marra ya tatu, akamtolea na kibanda chake, mkewe, mtoto, killa alicho nacho, kwa amani na samehe. Akaambiwa, "Hakuna, Muungu harathi sadaka kama hizo." Mkuu yule akalemewa na shangao na huzuni kwa kitambo, hatima akamwinulia Mmasihiya macho yenyi machozi, akamlilia kwa moyo, "Ee Bwana, tazama, kanitwae mimi hapa maskini tena."

## DAWA YA UGOMVI.

PALIKUWA na mwanamke amegombana na mumee amepigwa naye. Mtu akamjia akamwambia, "Usipopenda pigwa, ntakupa dawa ya ugomvi." Akamwambia, "Haya." Akampa dawa, ndio maji matupu, katika chupa, akanena, "Tia kinwani tu, usiyameze, mumeo hatakukaripia. Naye marra ya kumwona mumee na uchungu akaitia kinwani mwake. Hasira yake ikapoa upesi, akamwacha amani. Baadaye mwanamke akamwuliza mtu yule aliyempa maji, "Dawa yako imefaa sana ajabu. Inapatikana wapi?" Akajibu, "Kisimani mo mote."

## KUNGU.

PALIKUWA na nokoa, aliyeleta mjini kungu tano nzuri kuliko awezazo kupata. Ndio awali hii, watoto wake kuyaona matunda kama haya, nao waka-

Digitized by Google

chekelea sana kwa matunda yale kuwa mekundu na laini kama machavu yao. Na babao aliwapa watoto wa'nne moja moja, na ya tano mama yao.

Usiku wakati wa kulala baba yule alisema, " Niambieni mmetakaje matunda yale mazuri." Mtoto aliye mkubwa wao akamwambia, " Sana, baba, ina maji tele na tena tamu. Nimeweka kokwa yake nitaipanda niotesbe mti." " Heri sana," alisema baba, " Una akili na busara." Kitinda mimba akajibu, " Yangu naliila pale pale, nikatupia mbali kokwa. Mamangu akanipa nussu. Ah! tamu sana, imeyeyuka kinwani mwangu pia." " Bassi, " alisema baba, " hukufanya busara, lakini kwa utoto wako, kama tuwaonavyo watoto." Yule wa pili akaanza, " Nikaiokota kokwa ile aliyoitupa ndugu yangu, nikaivunja. Ulikuwa mbegu ndani, utamu wake kama njugu, lakini nikauza kungu yangu nikapata pesa nyingi, hatta nikienda mjini nitaweza kununua sita kwa mali yake." Baba akatikisa kitwa akasema, " Ndio busara halisi, lakini si ya utoto hiyo busara. Hasha usikue na choyo kama bakhili." Akamwuliza mtoto wa tatu, " Na wewe je? " Alijibu, " Naliichukua kungu yangu kwa yule kijana maskini, mtoto wa jirani yetu, hawezi, ana homa. Naye akakataa, bassi nikaiweka kitandani pake nikatoka." " Je, enyi watoto? " akasema baba yao, " Nani kati yenu aliyetumia vema kungu yake?" Wakasema wote watatu, " Huyu ndugu yetu." Yule akanyamaza kimya. Mamaye akambusu sana na machozi machoni pake.

## SULTANI HAKKUM.

Palikuwa na Sultani, jina lake Hakkum, akatwaa kwa nguvu shamba dogo la mjaani mmoja maskini, sababu alitaka kuiongeza bustani yake. Na yule maskini akaenda zake kwa kathi, apate kuhukumiwa haki yake. Naye kathi akamtandika punda yake, akaweka kapo kubwa juu yake, akapanda akaenda zake kwa Sultani, na yeye alikuwa anatembea katika shamba lile ndilo bustani yake mpya. Akamwambia, "Nataka ruksa nijaze kapo hili udongo wa shamba hili." Sultani akampa ruksa, tena yule kathi akajaza kapo udongo, akamtaka Sultani amsayidie kuliweka juu ya punda. Likawa zito sana. Akasema Sultani, "Lanishinda, haiwezekani kabisa." Kathi akamwambia, "Tazama, kapo hilo laweka kipande kidogo tu cha shamba, ulilomtwalia mjaani yule maskini. Bassi utawezaje kuchukua begani shamba lote pia, ndio mzigo utakaowekwa na Mwamuzi Mkuu siku ya mwisho?" Sultani akasangaa, akatubu, akamrudishia mjaani urithi wake.

## SULTANI ORUNGZEBI.

Uko katika Hindi mji mdogo, unaokwitwa Tolapur, maana yake pa kupima. Umehadithiwa hivi, ya kwamba palikuwa na Sultani, jina lake Orungzebi, akawa anapita katika inchi yake na asikari wake, akafika mjini mle, napo na mto na mashua ya kuvukisha watu. Akangoja pale penyi kivuko, wakivuka asikari wake, akaongea na mwenyi mashua. Mtu

Digitized by Google

yule akawa na sifa nyingi kwa kuwa mwerevu sana. Akamwambia Sultani, "Hatta hapana nyama yo yote nisiyoweza kuipima uzito wake barabba." Sultani akasema, "Bassi unipimie tembo huyo niliompanda." Akamwambia, "Kwanza mweke katika mashua yangu." Wakamweka. Mashua ikazama sana kwa uzito wake, mtu yule akapiga mstari katika mbavu za mashua sawa sawa na maji yalipofika juu. Wakashusha tembo pwani, akapakia mawe mengi makubwa, hatta mashua ikazama tena mpaka mstari ule ule. Tena akayapima mawe yale moja moja, akahesabu jumla la uzito wao, akamwambia Sultani, "Hiyo ndiyo apatayo tembo wako kwa uzito wake." Sultani yule akapendezewa sana na werevu wake akampa mji ule Tolapur.

## SULTANI MAHMOUD.

Palikuwa na Sultani mmoja wa Ajjemi, jina lake Mahmoud. Akafanya vita nyingi akaonea rayia zake, hatta inchi ya Ajjemi imekuwa kama jangwa, haina miji illa haba tu, ukiwa pote na maanguko matupu, na watu wachache.

Na waziri wake akajifanya anasikia lugha ya ndege, hatta ndege yo yote akilia, yule waziri hujua kufasiri maneno yake. Hatta siku moja jioni anatembea na Sultani, wakaona bundi wawili wametua mtini penyi kuta zilizovunjika. Sultani akamwambia waziri, "Nataka jua wanazumgumza nini wale." Waziri akakaribia mtini, akawasikiliza bundi, akarudi, akasema, "Nimewasikia kidogo, lakini kufasiri, Ah! hatta sithubutu mimi." Sultani hakuwa

Digitized by Google

rathi, akamwamuru ampashe habari. Waziri akamwambia, "Bundi mmoja ana mtoto mume, naye wa pili ana mtoto ndiye mke, wanafanya shauri la kuwaozana. Nikamsikia yule wa kwanza mwenyi mtoto mume akinena, "Bassi, rafiki yangu, nakubali mimi, lakini nataka umpe binti wako miji hamsini iliyoharibika." Yule mwenzake akajibu, "Inshallah! Hatta nampa hamsi mia, ukipenda mwenyewe. Amilikipo Sultani Mahmoud, miji iliyoharibika tele mno ajabu." Maneno haya yakamwingiza uchungu Sultani katika moyo wake, akaitengeneza miji aliyoiharibu, akawatendea watu wake vizuri.

PRINTED BY WILLIAM CLOWES AND SONS, LIMITED,
LONDON AND BECCLES.

Digitized by Google